

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 9 Novemba, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona kwenye *Order Paper* yetu leo tuna vitu ambavyo sio vya kawaida, ni siku maalum. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu?

KAULI ZA MAWAZIRI

**Utata Katika Upangaji wa Madaraja
ya Ufaulu Katika Mitihani**

SPIKA: Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Naibu Waziri?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:
Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge la jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Mwaka 2007.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

Kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa Kauli ya Serikali, kuhusu utata uliokuwa umejitokeza katika upangaji wa viwango vya alama na madaraja ya ufaulu katika mthani wa Kidato cha IV na Kidato cha VI.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 30/10/2013 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ilitoa Taarifa kwa umma kuhusiana na upangaji wa viwango vya alama, matumizi ya alama endelevu ya mwanafunzi na ufaulu katika Mthani wa Taifa wa Kidato cha IV na Kidato cha VI. Taarifa hiyo, pamoja na masuala mengine, ilibainisha kuwa Daraja sifuri (yaani 0) litafutwa na badala yake litawekwa Daraja la V. Aidha, kufwatia swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, siku ya Jumatatu tarehe 4 Novemba, 2013 kuhusu mfumo mpya wa kupanga madaraja, nilitoa ufafanuzi kuhusu upangaji wa viwango vya ufaulu katika mitihani hiyo, ambapo Mheshimiwa Spika, ulitoa agizo kwa Serikali kuleta taarifa sahihi kupitia Kauli ya Mawaziri ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi zote ziliamsha hisia na mjadala kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Wadau mbalimbali ambao wanafwatilia maendeleo ya elimu nchini. Kutokana na kauli hizo zilizojitokeza siku ya Jumanne, tarehe 5 Novemba, 2013 Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Kawe, aliomba Mwongozo wa Kiti chako kuhusu suala hilihili, ambapo Mheshimiwa Naibu Spika alisisi tiza tena na kuiagiza Serikali Kauli Bungeni, ili kutoa ufafanuzi kuhusu utata uliojitokeza.

Mheshimiwa Spika, madaraja yanayotolewa na Baraza la Mitihani Tanzania huanzia daraja la I hadi daraja la IV, ambayo ndio madaraja ya Watahiniwa wanaostahili kutunukiwa vyeti; Watahiniwa ambao hushindwa kupata kati nya madaraja hayo huwekwa katika kundi la Watahiniwa walioshindwa (*Failures*), ambao kimsingi wamekuwa hawatunukiwi vyeti. Hata hivyo, jamii imezowea kuita kundi hili kuwa ni watahiniwa waliopata Daraja 0 (*Zero*). Daraja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]

ambalo katika vitabu vya matokeo vya Baraza la Mitihani huwa linaandikwa ni Watahiniwa walioshindwa, *failures*.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Wizara iliyotolewa kwa umma na Katibu Mkuu, tarehe 30/10/2013 alilitaja kundi hilo la Watahiniwa kama Daraja la V kwa kuzingatia mpangilio wa namba ambao utakuwa na Daraja la I mpaka la IV kwa Watahiniwa waliofaulu na Daraja la V kwa Watahiniwa walioshindwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kuzingatia hisia tofauti zilizojitokeza miongoni mwa Wabunge na jamii kwa ujumla na mazowea yaliyojengeka miongoni mwa jamii kuhusu matumizi ya Daraja 0 kwa Watahiniwa walioshindwa mtihani, Serikali inatamka rasmi kuwa kundi la Watahiniwa walioshindwa mtihani na ambalo awali lilikuwa likiandikwa kama *failures* litaendelea kujulikana kama Daraja 0 (*Zero*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Nakuombeni, Kauli za Mawaziri hatuzungumzi. Nasema hivi kwamba, Kauli za Mawaziri hatuzijadili mpaka zitolewe kwa utaratibu maalum.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu?

HOJA ZA BUNGE

A Z I M I O

**Azimio la Kupongeza Tamko la Rais wa Jamhuri
ya Muungano wa Tanzania
Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**

SPIKA: Azimio.

Mheshimiwa Mtoa Hoja? Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Kamati ya Ulinzi na Usalama?

MHE. EDWARD N. LOWASSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Azimio la Kumpungeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu msimamo wake kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya juhudi za Serikali za kutekeleza Mkataba wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Bunge lako Tukufu kuthamini umuhimu wa Jumuiya hiyo, yamekuwepo maelezo mengi yanayotolewa kuhusu msimamo wa Tanzania juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alipolihutubia Bunge lako Tukufu tarehe 7 Novemba mwaka huu (2013), aliufafanua msimamo wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo alieleza kwamba, Tanzania haitajitoa katika Jumuiya hiyo. Msimamo huu unapaswa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Mamabo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuzingatia jukumu lake kwa mujibu wa Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama zinaliomba Bunge lako Tukufu lipitishie Azimio lifuatalo:-

Kwa kuwa, tarehe 7 Novemba, 2013 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Na katika Hotuba hiyo, pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Rais alilihutubia Bunge kuhusu msimamo wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Na kwa kuwa, Tanzania imekuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu mwaka 1999.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. N. LOWASSA]

Na kwa kuwa, nchi za Kenya, Uganda na Rwanda zimekuwa zikifanya vikao na majadiliano mbalimbali bila kuishirikisha Tanzania.

Na kwa kuwa, Tanzania haijawahi kufanya jambo lolote la kuashiria kutaka kujitoa wala kutamka kuwa inataka kujitoa kwenye Jumuiya hiyo.

Na kwa kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Hotuba yake aliyoitoa tarehe 7 Novemba, 2013 alisema kuwa Tanzania haina mpango wa kujitoa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa hiyo, basi Bunge linaazimia kwamba, linamuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Linaunga mkono msimamo kwamba, Tanzania isijitoe kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na linawataka watu wa Afrika Mashariki kuulinda, kuitetea na kujenga Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Anna Abdallah!

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia Hoja hii muhimu. Na mimi naungana kabisa na Azimio hili kwamba, si Bunge peke yake, bali Watanzania wote tunaiunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais wetu kwamba, sisi ni wanachama waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. tutaendelea kuwemo humo na hatutatoka kwa sababu, yeyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nieleze jambo moja kwamba, wakati tunaona boriti katika macho ya Viongozi wale watatu, sisi wenyewe humu ndani tuna vijibanzi kwenye macho yetu. Vijibanzi hivi tusipoviondoa basi tunawapa nafasi wasiotutakia mema kuendelea kutuona kama sisi ndio hatutaki Jumuiya.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. M. ABDALLAH]

Mheshimiwa Spika, sisi wenzenu tumepata bahati kuunganika na Kamati ya Mambo ya Nje kuuliza ni yepi haya yanayolalamikiwa? Wanayofikiri kwamba, sisi tunafanya mambo polepole?

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana kwamba, yale mambo madogomadogo, tatizo liko ndani ya utekelezaji hasa kwamba, kila Wizara ya Serikali ina Sheria zake, inaamua mambo yake yenyewe. Hata kama jambo limekubaliwa Kitaifa kwamba, jambo hili tulisuluhishe hivi, utekelezaji unakuwa sifuri, kila Wizara inafanya mambo yake; mambo haya yako 8, madogomadogo, lakini tusipoyaondoa hivi vibanzi ndivyo vinavyosababisha wengine kufikiri kwamba, sisi hatutaki kuendeleza Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vijibanzi hivi, wenzetu wa kamati labda nimwombe pia na Mwenyekiti wa Kamati, katika taarifa atakayoileta hebu watwambie ni mambo gani yaliyokubaliwa, mambo gani Serikali imetekeleza na mambo gani bado na sababu zake ni nini? Kwa sababu, mambo yenyewe ni madogo mno.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sisi Afrika Mashariki, eneo letu lote linaonekana ni sehemu yenye ugonjwa wa manjano, lote kabisa. Kwa hiyo, sisi tunapotoka humu ndani kwenda nje ya Afrika Mashariki, tunapaswa kuwa na cheti cha ile chanjo ya homa ya manjano, lakini tuna sababu gani sisi mtu anatoka Uganda, anatoka Kenya, anatoka Rwanda anaingia ... *(Hapa sauti ilikatika)*

Mheshimiwa Spika, imetokea na tumeambiwa kwa masikitiko kwamba, hata baadhi ya Wabunge wan chi wanachama walipofika KIA wakazuiwa, eti hawana cheti cha kinga ya manjano; jamani, haya mambo madogomadogo ndio yanayotuletea haya maneno.

Kwa hiyo, mimi naomba, pamoja na kuunga sana-sana Azimio hili, hatutatoka tutaendelea kuwemo, lakini hebu tuondoe yale mambo madogomadogo yanayotufanya hata

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. M. ABDALLAH]

heshima yetu inapungua mbele ya Afrika mashariki kwa sababu, ni madogo mno, hayahitaji Sheria, kinachotakiwa ni utashi wa kisiasa wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono. Ahsante sana.
(*Makofi*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Ninaunga mkono Azimio kwa kuwa, Tanzania kwanza, mengine baadaye.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa dira katika ukanda wetu huu wa Afrika zaidi ya miaka 50 iliyopita. Mheshimiwa Lowassa, nakumbuka tarehe 9 mwezi wa 4 mwaka huu (2013) wakati Rais wa Kenya anaapishwa, ulipopigwa wimbo wa Bara la Afrika ilipigwa beti ya kwanza ya wimbo wetu wa taifa na wote walishangilia kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Samwel Sitta tulikuwa wote, ikaonesha kwamba, Tanzania tumeweza kutoa Wimbo wa Bara la Afrika na Ukanda huu ukaukubali; ni kati ya vielelezo tunu kubwa Tanzania wanaonesha katika Bara letu hili la Afrika.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kiswahili *origin* yake ni Tanzania. Tunaendelea kukienzi namna gani?

Mheshimiwa Spika, na kabla sijasahau, Kauli aliyoisema Mama Abdalla, nakubaliananae. Mheshimiwa Samwel Sitta, tarehe 6 ya mwezi wa 4, tukiwa *Intercontinental Hotel*, tulilalamikiwa na Wabunge wetu *KIA*, wamefika pale mpaka Mheshimiwa Sitta ikabidi umpigie Waziri wa Afya baada ya kukueleza hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa yako mambo madogomadogo hata kwenye Idara za Uhamiaji ambayo ni ukweli humu ndani hatutekelezi inavyohitajika na wenzetu wanatuona kana kwamba, kuna urasimu wa hali ya juu sana hapa na kwamba, hatuwezi tukaenda kwa *speed* ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

wanakwenda. Lakini Watanzania siku zote tangu wakati wa Mwalimu Nyerere, tumekuwa ni Kituo cha Ukombozi wa Kusini mwa Bara la Afrika; na sifa tuliyonayo Duniani, ukisema wewe umetoka Tanzania, wanasema Tanzania ya Nyerere?

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize, tangu mwaka 1999 na mambo haya yote ya mchakato wote yanayoendelea, ni kweli hata katika Ukanda huu wetu wa Afrika Mashariki, Tanzania tuna eneo kubwa kuliko wenzetu wote. Sisi tuna zaidi ya kilometa 945,903 ukilinganisha na wenzetu wote, tunawazidi kwa zaidi ya kilometa za mraba 73,000; sasa tunatumiaje nafasi hii kuendelea kuwa Kiongozi kwa Nyanja zote? Iwe ni rasilmali, iwe ni uelewa, iwe ni sekta zote na hasa kwenye sekta kama ya elimu; namna gani tunaangalia miaka 50 ijayo, ili tuendelee kuongoza katika nchi zetu hizi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 24 na 25 walipokutana kule Uganda, tulianza kuona hapa panatokea nini? Na tulizungumza, lakini niombe basi kwamba, yale tunayoyazungumza tunayoyaona Serikali ifanye *speed*, ifanye kasi. Serikali ione kesho kuna nini, ili tuendelee kuwa kiongozi hata kama ni masuala yanayolalamikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ile tarehe 28 ya Agosti mwaka huu (2013), siku ya Jumatano, walipokutana pale Mombasa wakazungumza, wakakubaliana mambo ya reli haya, mambo ya bandari haya, basi tuone ni changamoto chanya kwetu sisi kwamba, wametuamsha. Badala ya sisi kulalamika, tuone kwamba, ni nafasi pekee ya kufanya kazi kwa kasi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kauli za Wanasiasa. Unajua kuna mambo mengine madogomadogo sio vizuri sana Wanasiasa linapotokea jambo kwamba, ni letu la Taifa kutafakari yakinifu kabla ya kutoa kauli. Kutafakari yakinifi kwa sababu, kauli hizi ndio zinaanza vita ya maneno-maneno, huyu kasema hiki, huyu anamrudishia yule. Ili Tanzania yetu humu ndani, hata kama tunabishana humu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

ndani, lakini linapotokea suala kwamba, ni Tanzania inaguswa tunakuwa ni kitu kimoja kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe kwamba, Bunge letu la Afrika Mashariki, kwa kiasi kikubwa ukiongea na Wabunge hawa hata wakati mwingine walijitokeza kwenye vyombo vya habari, inaonekana hawapati maelekezo sahihi wanaenda kufanya nini ndani ya Bunge letu la Afrika Mashariki. kwa hivyo, unakuta Wabunge wetu wa Afrika Mashariki kila mtu anatoka nyumbani kwake anaenda kwenye Bunge na akitoka kwenye Bunge anarudi nyumbani kwake, hawafanyi mrejesho sahihi, hawapewi maelekezo sahihi.

Mheshimiwa Spika, hebu niombe Mheshimiwa Sitta na Wizara, hebu sasa changamoto hizi tuzione ni chanya sasa, tuamke, ili tuweze kuwa na kitengo maalum. Iwe ni Muswada unapelekwa kule, iwe ni chochote kinachotakiwa kufanyika kule, tunakuwa *up to date* na tunapata mrejesho humu ndani. Na ndio maana unaweza ukaona hata Hotuba ya Mheshimiwa Rais, juzi tarehe 07, Wabunge wetu wa Afrika Mashariki hawakuandaliwa wakawemo humu wakapata Tanzania msimamo wake hasa ni upi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikubaliane kabisa na Mama Abdalla kwamba, japo wenzetu naona ni boriti kwetu ni vibanzi na tufikirie kwa makini je, ni vinginevyo au ni hivyo? Lakini kwa kuwa, Tanzania uwezo tunao, nia tunayo, Mheshimiwa Rais, Kauli aliyoitoa ni Kauli inayoonesha ukomavu mkubwa wa Kiongozi wa kisiasa na ukomavu mkubwa wa Kiongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumuunge mkono tuhakikishe kwamba Tanzania yetu hii ambayo sote tunaipenda imekuwa ndiyo kituo cha Wakimbizi kwenye ukanda wote huu ni Tanzania, ikitokea tatizo lolote ni Tanzania basi amani tuliyonayo, uwezo tulionao, nguvu tulizonazo tuzitumie na tuone haya yote yanayotokea wala yasisuyumbishe sana. Tuone wametuamsha tuanze kuchapa kazi tuhakikishe

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. JAMES F. MBATIA]

kwamba lolote lile linalotokea jumua hii haiwezi ikaondoka Watanzania tumo kwa gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuzungumza kuhusu jambo hili ambalo nafikiri ni muhimu sana.

Nikiri mimi binafsi nilikuwa kama mgonjwa baada ya kuona mwenendo wa Serikali yetu na kauli za viongozi, kauli za Wabunge kubeza *East Africa* na nilikuwa najuliza mimi sijui nifanye nini katika nafasi yangu yoyote ile pengine kusaidia jambo hili lakini kwa kauli ya Mheshimiwa Rais ambayo ina msimamo wa Serikali yetu ambao aliutoa rasmi hapa kwenye Bunge hili na kufuatiwa na azimio ambalo limewasilishwa hapa na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Usalama kwa kweli nina kila sababu ya kumpongeza Rais, kuipongeza Kamati na kulipongeza Bunge lako Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, kujitoa Afrika Mashariki ni *unthinkable* wala siyo jambo la kutafakari wala la kifikiri na tumejenga Taifa lenye uwoga lazima tujiangalie wenyewe tujitathmini. Tunawaogopa jirani zetu, tunakosa *courage* kama Taifa kwa hiyo tunakuwa tuna hofu ya wenzetu badala ya kuwafikia namna ya kuwa-*engage* wenzetu. Kwa hiyo wazo lililoletwa hapa na Kamati ya Azimio lililoletwa hapa na Kamati kama alivyosema Mheshimiwa Mbatia hebu iwe *wake up call* yetu tusilalamike tu na sisi tukae ndani tutafakari *where have we gone wrong*. Kenya watache, Uganda watuache, Rwanda watuache haiwezekani ikawa hatuna tatizo la ndani tuna tatizo na tuwe na *courage* ya kuona tatizo letu na kulifikiria namna ya kuli-*engage*.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwa mtazamo wangu na *my political analysis* wenzetu katika Afrika Mashariki wana malengo ni nini malengo yetu katika Afrika Mashariki kama Taifa na nini *strategy* yetu ya ku-*achieve* malengo yetu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. MBOWE]

katika Jumuiya *what do we want to achieve* na tuna *strategy* gani. Wakenya wakija katika vikao vya Jumuiya Wabunge wao wanakuwa wamepewa maelekezo vizuri sana *they exactly know what they want* lakini Watanzania watu wanakwenda kivyao, Bunge letu la Afrika Mashariki Wabunge wetu hawaripoti Bungeni, hawaleti *feedback* hatujui wanafanya nini kule, wanakutana na nini, kwa nini hatuna *early warning system* matatizo yanaweza kutokea kwenye Bunge la EALA kumekuwa kuna mvutano kwenye Bunge la AR, Bunge hili halijapewa taarifa yoyote na sisi Bunge hili ndiyo tunalochagua Wabunge wa EALA.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameanza kuziriana, Wabunge wameanza kugoma vikao hakuna ripoti imekuja Bungeni, hakuna taarifa ambayo tumekuwa na *courage* ya kui-*discuss* tunatatizo gani, *early warning system* zimeanza kuonekana kwenye Bunge, Wabunge wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu mno na hakuna *connectivity* na Bunge lako haya ndiyo matatizo yanayopelekea wenzetu wanatuona pengine tuko *slow* katika kufanya maamuzi na ni kweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alizungumza mambo manne hapa kwanza tulikuwa tuna *entry point* ambapo tulikuwa tunakwenda katika hatua ya pili ya *common market*, *entry point* ilikuwa ni *custom*, ya pili ni *common market*, ya tatu ni *monetary union*, *ultimately political federation*. Ni miaka 14 leo tangu tumeanza hii *process* bado tuko namba *two*, bado tuko namba *two* ni kweli tulitengeneza *road map*, tumetengeneza *road* miaka 14 bado tuko namba *two*. Sasa ukiangalia tulichoki-*achieve* katiika jumuiya na muda wa miaka 14 unaona kuna tatizmo sasa tatizo ni la Kenya peke yake ama tatizo ni la Tanzania peke yake ama la wenzetu wa Uganda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba hii iwe ni *wake up call*, hii iwe ni *wake up call* na sisi tuwe na mikakati kwa sababu *at the end of the day* Tanzania tungekuwa *strategic* tungekuwa na fursa kuliko wengine wote kwa sababu sisi kwa sababu nchi kama Burundi ina-*boarder*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. MBOWE]

Rwanda, ina-*boarder* Tanzania kwa upande wa huku katika *members wa East Africa* lakini sisi *members* wote hawa tuna *boarder* nao tuna *boarder* na Kenya, tuna *boarder* na Uganda, tuna *boarder* na Burundi, tuna *boarder* na Rwanda yaani tuna *advantage*, tuna *linkage* na kila nchi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani ndiyo tuko *the most strategically position* lakini hatutumii fursa halafu tunalalamika.

Mheshimiwa Spika, tukubaliane katika jumuiya ya diplomasia kauli ni jambo la msingi sana. Kauli wakitoa kina Mbowe utasema kina Mbowe hawa ni wapinzania lakini kauli zinapotoka kwa *cabinet ministers*, kauli zinapotoka kwa Wabunge, tena Wabunge ambao wanachama tawala kuishiria ubabe katika masuala ya kidiplomasia hakuna ubabe hapa katika diplomasia na tuiseme tu azimio hili na Rais anasema tutakwenda kuji-*engage* katika kikao ambacho wanakutana tarehe nafikiri alisema tarehe 28 au *something*.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni delicate tunahitaji kuliundia timu ya Kidiplomasia kuanza kutengeneza *ground* tukifika kwenye kikao siyo tukaelezane kwenye kikao haya mambo Serikali itumie fursa itengeneze timu ya kidiplomasia ikarekebishe mambo haya mkifika kwenye *summit* watu mnachekeana, mnakunywa maji mnamaliza kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuisubiri mpaka kwenye kikao ndiyo mkangojee kina Mzee Sitta mweleze ni kwa nini wenzenu wamefanya vikao vya siri, fanyeni mipango ya *lobbing mapema and that is political management, diplomatic management* ya hii *crisis* ambayo tuko nayo sasa hivi.

Lakini niombe sana kwa Watanzania wote *including the media, media ime-hike* sana hili tatizo nje na huu ugomvi umekuwa *deepen* na *media* yetu. *Media* imeripoti vibaya sana yaani *media* imesimama upande wa Serikali ikaanza kuona majirani zetu ni wabaya hatukuwa *objective* kama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. MBOWE]

Taifa hatutaki ku-*admit mistake* zetu, hatutaki ku-*admit weaknesses* zetu tunakuwa na *pride*, tunakuwa na utaifa ambao unazidi mipaka ya kutafakari kwa kina *where have we gone wrong* kwa hiyo *media* nayo ikaendelea ku-*hike* ukisoma mitandao ya social media nayo inaendelea ku-*hike* imeendelea kuwatukana wenzetu, tunaendelea kuwabeza na kuwadharau wenzetu tunataka kuwaona kwamba *they are nothing, no*.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tukubaliane kama Taifa jamani tunawahitaji sana sana wenzetu kama vile wao wanavyotuhitaji *at the end of the day* ni kwa fursa na *advantage* yetu. Tuna uhusiano wa Kimataifa wa kihistoria ukizungumza utalii 60% ya watalii wanaokuja *northern circuit* wana *land* Nairobi, ukileta mgogoro wowote wa kimaslahi pale ama wa kidiplomasia kati ya nchi hizi mbili tunaua uta, lii wetu, utalii wa Zanzibar unategemea kwa kiasi kikubwa sana *linkage* yake na Mombasa huwezi ukakataa hiyo *facts*.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia biashara ya Mwanza, Mkoa wa Mara dhidi ya Kenya, Arusha, Manyara Kilimanjaro, Tanga ile zone yote ya *North linkage* yake na Kenya ni kubwa mno *investment* za Kenya nchi hii na Kenya ni *trading partner* mkubwa kuliko wote kuzidi *South Africa* katika nchi yetu. Hatuwezi tukafika wakati tukapuuza hili jambo lisionekane ni jambo la maana.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa ili pengine niache fursa na kwa wenzetu vile vile waweze kuchangia. Serikali itusaidie tunataka nini *East Africa*, tunataka nini katika jumuiya na niseme tu hili ugomvi wetu na wenzetu hauko tu kwenye *East Africa* kuna hata ukweli kwamba katika *SADC* nako hatueleweki vizuri sasa tunalalamikiwa kwenye *SADC Block*, tunalalamikiwa kwenye *East Africa what is wrong with us*. Sisi tuko katika *partner* na nchi na 13 za *SADC* sisi ni *partner* lakini hebu tuangalie sisi *direct link* yetu na Namibia, *link* yetu na Madagascar, *link* yetu na Swaziland, Lesotho, Botswana tuna *trade partnership* gani pale hakuna *basically*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. MBOWE]

Lakini sana sana tunayefanya naye katika SADC ni Kongo, Malawi, Zambia na Mozambique lakini nchi zingine zote za SADC hatuna *boarder* nao kabisa na wao *interest* yao *focus* yao ni *South Africa*.

Mheshimiwa Spika, hebu tuchague tunamtaka *partner* gani, tusiwe mke mmoja waume wengi tuko kote halafu tunakosa kote *why*. Hebu tu-*decide* tunataka sisi tukae kwenye *partnership* gani. Tanzania tunajaribu kwenda kila mahali kum-*please everybody* halafu *at the end of the day* hatuwezi ku-*perform* kokote na kote tunaonekana kwamba *we are non starters*.

Mheshimiwa Spika, naomba tujifunze nina hakika wenzetu kama wanajua haya mambo hawajatuambia kama mnajua mkakati wa Serikali yetu dhidi ya faida gani tunazipata katika jumuiya hazijafanywa *public* dunia haijui sina hakika kama *business community* inajua unajua watu wepesi mno kuona Wakenya ni watu wabaya, Waganda ni watu wabaya lakini tuko tayari kuwakumbatia Wachina, tuko tayari kuwakumbatia Wahindi au mataifa mengine yoyote ya mbali lakini hawa waswahili waliotuzunguka hebu tujiangalie wametuzidi nini, tujifunze nini kwao ni kwa nini tunaogopa kufungua *labour market* kwa nini tunawaogopa Wakenya, Wakenya sasa hivi tupende, tusipende wamechukua *managerial position* kwenye makampuni mengi sana katika nchi yetu, kwa sababu kwa mujibu wao waajiri wa nchi hii wanaamini Wakenya wana-*provide a better job market*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutafakari, tujipange tu-take *advantage* ya mambo yaliyopo tusilalamike tukalia tuwe *bold and courageous* tusonge mbele. Hongereni sana kwa kubaki kwenye *community*, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante nilisema Mheshimiwa Eng. Mnyaa kwanza ndiyo utaratibu. Kwa kawaida hotuba ya Mheshimiwa Rais huwa tuna ipangia muda wa kujadili na hii hatuwezi kufanya kipindi hiki itabidi tufanye tutakaporudi pale ndiyo tunajadili kwa kirefu. Leo tuwe ni azimio tu-*capture*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

pale aliposema hatuondoki. Naomba mnaochangia muende kwa mtindo huu.

Kwa hiyo, suala la kujadili hotuba hii lipo bado pale mtaenda kwa kirefu zaidi. Sasa Mheshimiwa Mnyaa atafuatiwa na Mheshimiwa Makilagi.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi niipongeze kwanza kamamti ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa hatua hii ya kufikiria kuleta azimio hili ili tuitendee haki hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba muda wa kujadili pengine ni Bunge Iijalo na leo kuna mpango wa kuhairisha Bunge isingekuwa ni busara tundoke hivi hivi bila ya kusema chochote. Kwa hiyo, kwanza nipongeze Kamati hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Mheshimiwa Rais kuja kulihutubia Bunge au kulihutubia Taifa kwa ujumla ni kitendo ambacho kimetufungua macho kwa wale ambao walikuwa hawajafahamu nini kinaendelea na kimentuweka sawa sisi ambao tulikuwa tunafuatilia mambo yanavyokwenda na zile taharuki tulizokuwa nazo. Kwa hiyo, tumpongeze Mheshimiwa Rais kutuwekea sawa mambo haya na kwamba Tanzania imetufanya kuwa *united* zaidi kuliko mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 7 Mheshimiwa Rais alipolihutubia Taifa moja katika kauli alizozitamka kwamba hatutajitoa katika Jumuiya ya Afrika mashariki ni kauli ya kupongezwa. Hata ile jumuiya ya Afrika mashariki iliyovunjika mwaka 1977 Tanzania hatukuwa wa mwanzo kujitoa wengine ndiyo waliosababisha na safari hii msimamo wetu ndiyo huo huo na tunaomba Mwenyezi Mungu ajalie na wenzetu awape moyo wajjue makosa yao na ili tudumishe jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

Mheshimiwa Spika, tumekuwa katika wimbo wetu wa Taifa huwa tunaizungumza Tanzania na bara zima la Afrika ndani ya wimbo wetu wa Taifa. Aliyozungumza Mheshimiwa Rais ni kielelezo tosha kwamba misingi ile ile ya wenzetu viongozi wa Afrika waliotangulia akina Kwame Nkhuruma na Mwalimu Nyerere na Mheshimiwa Dkt. Jakaya amefuata nyayo zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Tanzania tutaendelea kupigania umoja wa Afrika, Umoja wa Afrika Mashariki, Umoja wa *SADC* na kadhalika kwa maendeleo ya nchi hii na hatutakuwa wa mwanzo na tunaungana naye mkono kwamba sisi mhatutakuwa wa mwanzo kujitoa.

Mheshimiwa Spika, labda niseme neno moja ambalo Mheshimiwa Mbowe kidogo ameligusia. Yapo matatizo mengine yanakuwa aggravated au yanachochewa na baadhi ya vyombo vyetu vya habari kwamba baadhi labda kwa sababu ya uhuru wa magazeti na labda wapo waandishi wengine wa nje ambao wapo hapa nchini vitendo hivi vya kuchochea kukuza hata jambo dogo kulikuza likaonekana kubwa hili ndiyo jambo moja ambalo linatuharibia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani kwa hotuba aliyotoa Mheshimiwa Rais vyombo vyetu vya habari sasa vitaona ule umuhimu wa ku-*unit* vizuri na kwamba Tanzania mbele.

Mheshimiwa Spika, kuna Profesa mmoja, Profesa Mazrui akizunguka katika *university* tele duniani huko Marekani na wapi huwa anazungumzia hali ya Afrika kutawaliwa kulitokana na ukarimu wetu na ile *access* ya kwamba hatuna shida ya mboga, ukizunguka nyumbani kila aina ya mti ni mboga, wanyama, mito, maziwa, bahari ile Afrika wakati huo kuna kila kitu kiasi ambacho hatuna shida ya kutafuta maisha yalikuwa mazuri wazee wetu waliotutangulia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

Mheshimiwa Spika, kitendo hicho cha kwamba tuna *access* ya kila kitu mpaka *mineral resources*, madini hiyo zamani wanavyosema dhahabu watu walikuwa wanachezea kete kwenye bao ndicho kitendo kilichosababisha wageni kuja kututawala Afrika.

Sasa hivi imekuwa sasa ukiacha wageni kutoka Ulaya kuivamia Afrika, Tanzania kuwa na *access* ya kila kitu na kuwa shida zetu siyo kubwa sana, shida zetu sana sana ni za kiutawala lakini tuna chakula cha kutosha, tuna maziwa ya kutosha, tuna samaki wa kutosha, tuna madini ya kutosha kitendo hiki na ule ukarimu wetu na upole wetu ndiyo unaosababisha majirani au mataifa mengine kutuona labda sisi sijui tukoje au ndiyo kile kinachopelekea wenzetu kutaka kutupandia juu ya vichwa vyetu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hizo hotuba hii ya Mheshimiwa Rais iwe ni funzo kwa Watanzania kwamba sasa na sisi tuwe *aggressive* kibiashara. Hatuwezi kubakia hivi sasa tulivyo tu kwamba sasa na sisi tujifunze Watanzania sijui neno zuri lipi hapa lakini tuwe *aggressive* sasa na sisi kibiashara tusionekane hii *access* ya kila kitu tulichonacho tukaacha nafasi hizi waje wageni zaidi kuzitafuta kwa njia na hila sisi wenyewe tumekaa tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hotuba hii ya Mheshimiwa Rais aliyoitoe tarehe saba iwe ni kielelezo kwetu na Mungu akijalia Mheshimiwa Spika uje utapatie nafasi rasmi kuijadili hotuba hii katika Bunge lako Tukufu hapo ndipo tutakapokuja kupata nafasi nzuri ya kusema mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache napongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais na Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika asanteni sana.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuunga mkono azimio hili la kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Bunge letu la jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe saba hotuba ambayo kwa kweli ilikonga nyoyo za Watanzania na hasa wanawake.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba na mimi nianze kuzungumza kwamba kwa kweli kile kilichokuwa kikiendelea katika nchi yetu na hata kupitia vyombo vya habari kilianza kututia mashaka na hasa wanawake walianza kujawa hofu wakiamini kwamba pakitokea msukomsuko wa kutengana na hizi nchi ambazo zinazunguka inaweza ikaleta kuvunjika kwa amani kwa nchi yetu na kama amani ingevunjika wanawake ndiyo wangukuwa waathirika wa kwanza kwa kweli hotuba ya Mheshimiwa Rais imekonga nyoyo zetu.

Mheshimiwa Spika, ninasema hivyo kwa sababu nchi yetu ya Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo kwa kweli zimebaki kuwa visiwa vya amani na utulivu. Kuna kiongozi mmoja amezungumza hapa kwamba wapo watu wanaotunyemelea pengine sisi tunawakosea mimi nataka niseme hatuwakosei hata wazungu wanatamani kuja Tanzania na nchi zote zinazozunguka na nchi zote zinazozunguka wanatamani kuwa Watanzania na Mnyaa hapa amezungumza hata ule ukarimu wetu tulionao kila mtu anaitamani Tanzania kwa sababu Tanzania ni Tanzania yenye amani na utulivu kwa hiyo ndiyo maana wakati wote hata watu ambao hawatutakii mema wanaweza wakatumia fursa mbalimbali kubomoa amani tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono hotuba ya Mwenyekiti kwa sababu na naunga mkono kauli yake kwamba Tanzania haitajitoa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu sisi Watanzania ni miongoni mwa waanzilishi hata kabla Jumuiya haijavunjia tumetoa mchango mkubwa sana wakati ule ilipokuwa imeanza na hata iliporudia mara ya pili sisi Watanzania tumetoa mchango mkubwa sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. N. MAKILAGI]

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kitendo cha Rais kuendelea kuweka msimamo katika nchi yetu kwamba Tanzania hatufikirii na hatutegemei kujitoa katika umoja huu ambao tumeupata kwa tabu kwa kweli mimi naomba niunge mkono azimio hili kwa asilimia mia moja kwa mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi ambacho nataka nishauri ni kwamba Tanzania hii na hata ndiyo maana unaona wenzetu wana harakisha nchi yetu ya Tanzania ndiyo imebaki na ardhi yenye rutuba, nchi yetu ya Tanzania ndiyo imebaki watu wanaweza kwenda popote wanaweza wakafanya chochote, wanaweza kusema chochote bila kuvunja sheria na wakaenda sawasawa. Tanzania hii ndiyo imebaki kuwa kisiwa cha amani na utulivu ambacho mim nataka nishauri hapa kama ambavyo Kamati ya mzee wangu ilisema kwamba Jumuiya hii tusiharakishe katika mambo ya msingi. Na mimi naunga mkono hotuba ya Rais kwamba kuna Taifa ambalo linafikiria tuvuke kipengele kwenda kwenye kipengele cha pili kwa kweli mimi napingana nacho na naomba niunge mkono kabisa lile tamko kwamba twende hatua kwa lengo la kutufikisha pale tunapohitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja hii ahsante sana.

SPIKA: *Fifty, fifty* Mheshimiwa Jenista, naanza na *fifty* humu humu.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuanza kuona umuhimu wa *fifty, fifty* katika Bunge letu ahsante sana. (*Makofi*)

Mimi naomba niseme nasimama kwa nguvu moja kuunga mkono Azimio hili lililoletwa hapa mbele yetu kwa asilimia mia moja. Lakini mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais ametimiza majukumu yake ya kikatiba kama Kiongozi Mkuu wa Nchi, masuala ya Kitaifa na masuala ya mahusiano ya kimataifa yanapotokea na kulikumbuka Taifa letu, mahali anapoweza kuja na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

kuzungumza maneno mazito kama aliyoyafanya juzi ni ndani ya Bunge ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amefanya sawasawa ziara zake zimejizhirisha wazi katika suala hili zito na ametekeleza wajibu wake wa kikatiba.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kitu kimoja Mheshimiwa Rais kitendo chake cha kuwaambia Watanzania atahakikisha hatuondoki katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki ameonyesha ni kiongozi anayetambua maana ya umoja kuliko Utengano. *(Makofi)*

Ingekuwa ni kitu cha ajabu sana katika haya yaliyotokea halafu Rais wetu ambaye amekuwa ni kielelezo cha umoja katika umoja wa Mataifa akaingia hapa na kuanza kuteteleka katika umoja wa Afrika Mashariki kule anakotoka ingekuwa ni kitu kingine kabisa.

Kwa hiyo ninawaomba Wabunge wenzangu kwanza tumpongeze Rais wetu kwa kitendo hicho na maamuzi hayo aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja alizozitungumza Mheshimiwa Rais, wala siyo hoja za kuzipuuza. Mheshimiwa Rais anaposema umuhimu wa umoja, ana maanisha kitu kimoja kikubwa hiki nitakachokitungumza.

Nchi za Afrika Mashariki si kwamba sisi tunawategemea wao tu wa Kenya na wa Uganda na wengine hata wao wanatategemea sisi ndiyo maana ya umoja. Tulipokuwa tunaunda jumuiya hii ya Afrika Mashariki tulijjenga katika misingi ya umoja kwa maana ya kwamba tutategemea na si kwamba Tanzania itawategemea wao. *(Makofi)*

Sasa kama wote tulikubaliana tunategemeana umuhimu wa wale wenzetu watatu kuona na sisi Watanzania wanatategemea hilo ni jambo ambalo walipaswa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

kulitambua kwa nguvu zote. Kwa hiyo, hoja zile ambazo Mheshimiwa Rais alizitungumza hapa kwa mfano masuala ya Ardhi, unamwona kabisa Rais wetu alivyo makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme hoja si kuchelewa tu kufikia makubaliano si lazima makubaliano hayo ya Afrika Mashariki yote tuyaingie tu kwa haraka bila kuyafanyia upembuzi yakinifu, ni lazima tutafakari katika haya tunayokwenda kuyakubali ni mambo gani yana tija na maslahi kwa Taifa la Watanzania na mambo gani yanatakiwa yafanyiwe kazi ya kutosha na mimi namuunga mkono sana kwenye suala kama hili la Ardhi. Hivi kweli tunaweza kweli tukakurupuka tu sisi tumeshajipanga namna gani ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nadhani iko haja kwa kweli kama ulivyo sema kwanza ya kuhakikisha tunafanya kazi ya kutosha ya kuona ni namna gani masuala haya ya ardhi yanafanyiwa kazi ya kutosha ndani ya nchi kabla hatujakubaliana na Shirikisho letu hili la Afrika Mashariki kwa ujumla wake. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Rais nampa moyo na kumtia nguvu yote afanye kila linalowezezana kuwasaidia na wenzetu watambue nini tunachokifikiri halafu twende pamoja katika umoja. Wakati nchi nyingine zinapambana kudumisha umoja sisi tusiubomoe umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Azimio hili namtakia Rais wetu kila la heri aendelee na busara hiyo ya hali ya juu na Marais wengine waone busara ya Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete na umoja huu uimarike badala ya kuvunjika kama ilivyokuwa mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja nampongeza Mheshimiwa Rais na ninawapongeza wajumbe wa Kamati waliona umuhimu kwa kutuletea Azimio hili ndani ya Bunge leo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, kwa kurejea Ibara ya 63(1) na 63(2) ya Katiba ya Nchi pamoja na kuunga mkono msimamo wa Rais kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*), ni muhimu Azimio liboreshwe ili kuwezesha Bunge kutimiza wajibu wake wa kuishauri na kuisimamia Serikali. Hivyo, Maazimio yafuatayo yaongezwe pamoja na pongezi kwa Rais:-

(I) Baada ya mazungumzo ya Mawaziri wa *EAC* ambayo Serikali imeeleza yatafanyika baada ya Mkutano huu wa Bunge, Serikali iwasilishe taarifa katika Mkutano ujao wa Bunge juu ya maendeleo ya mazungumzo hayo;

(II) Katika Mkutano ujao wa Bunge kuwasilishwe taarifa ya Wabunge wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) ili Bunge lichukue hatua zinazostahili kutokana na mapendekezo yao juu ya yaliyojiri katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*); na

(III) Baada ya kupitia taarifa hizo zote mbili, Kamati za Bunge za Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama ziliwezeshe Bunge kupitisha Maazimio ya ufumbuji endelevu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais juu ya alivyoviita ni vyanzo vya migogoro, vipo vyanzo vya ziada ambavyo havisemwi. Mfano, mahojiano kati ya Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Membe, juu ya kuihusisha Rwanda na kuunga mkono M23 kwenye mgogoro wa DR Congo. Hivyo kuna haja ya Bunge kubaini vyanzo vya kina ili kuiepusha nchi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

kufanya maamuzi kwa taarifa za upande mmoja tu kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali iondoe udhaifu katika utekelezaji wa miradi ambayo inawezesha Tanzania kutumia fursa za kiuchumi na kupata tija ya kijiografia. Katika miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Reli ya Kati na kuiwezesha kufika nchi ya DRC, Rwanda na Burundi. Pia Tanzania iharakishe kushughulikia ucheleweshaji kwenye usafiri wa barabara na kwenye usafiri wa nchi kwa nchi (*Transit Cargo*).

Mheshimiwa Spika, katika kujiandaa na Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge utakaojadili suala hili, Wabunge tupewe nakala ya ripoti za Amos Wako na ripoti ya Wangwe ili kuweka msingi wa kurejesha heshima ya Taifa katika diplomasia na utangamano kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*).

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote tunaunga mkono, sasa nitawahoji wanaoafiki kumpongeza Rais naomba ninazungumza. Wanaoafiki kumpongeza Rais kuhusu msimamo wake kwamba Tanzania haitajitenga na Afrika Mashariki waseme ndiyo.

Mmeogopa kuitwa wachawi anayepinga, ahsanteni sana. Tunawapongeza Kamati ya Ulinzi na Kamati ya Mambo ya Nje kwa kukaa kwa pamoja na kuweza kuleta Azimio hili. Kama nilivyosema, kama kawaida yetu, Rais akishatoa hotuba hutengeneza utaratibu Bunge Iijalo tunajadili. Sasa pale ndiyo mtajadili kwa kirefu zaidi. Kwa hiyo, baada ya kusema hivyo, Katibu tuendelee.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013 (*The Constitutional Review (Amendment No.2) Bill. 2013*)

(Majadiliano yanaendelea)

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu ya ziada juu ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 22 (a) yenye kuainisha aya (c) kifungu kidogo cha (i) kinachoainisha idadi ya Wajumbe wa Kuteuliwa na Rais kuwa 201, napendekeza idadi ya Wajumbe wa Kuteuliwa iwe walau mia nne. Tukumbuke Katiba hii ni ya wananchi na hivyo hatuna budi kutoa wigo mpana kwa ushiriki wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongezwa kwa makundi mengine ambayo ni ya Wajumbe kutoka kundi la Wanawake au Taasisi zinazojishughulisha na masuala ya Wanawake. Ikumbukwe kuwa wanawake ni kundi ambalo lipo *vulnerable/victims* kwenye aina mbalimbali za *violence* (ukatili). Pia wanawake inapaswa wapewe *special group/category*, hii itasaidia sana. Hivyo, napendekeza wajumbe wasiopungua 30 kwenye kundi hili la wanawake, ambalo litajumlisha wajane.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napendekeza kuwepo na kundi lingine litakalokuwa linawakilishwa na taasisi zinazoshughulika na masuala ya watoto. Ikumbukwe kwamba watoto wanapaswa kupewa wawakilishi ambao watawasemea mambo gani yaingizwe kwenye Katiba na kundi hili laweza kuwa na idadi ya walau ya wajumbe wasiopungua 20. Hili ni kundi maalum sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ESTER N. MATIKO]

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuhusiana na Wajumbe, napendekeza pia kuwepo na wajumbe kutoka kundi la wafanyabiashara. Hawa pia ni wadau wakubwa sana katika mustakabali wa nchi yetu na hasa kiuchumi. Hivyo, kada zote za wafanyabiashara, wadogo, wa kati na wakubwa nao wawe Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napenda pia kuwepo na wajumbe kutoka katika kundi la wazee/taasisi zinazoshughulika na masuala ya wazee. Hili ni kundi muhimu sana na tunashuhudia wazee wanaachwa nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia katika Muswada huu muhimu wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona na kuleta tena Mabadiliko ya Sheria ambayo tumepitisha 2013. Upungufu ambao Serikali imeuona na kuamua kuleta Bungeni mabadiliko ambayo yatatuwezesha kuundwa na kuendesha Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza idadi ya wajumbe kutoka makundi mbalimbali kutoka kila upande wa Jamhuri. Muhimu hapa ni kuzingatia namna hawa wajumbe watakavyopatikana kwa uwazi toka makundi hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine muhimu ni kwamba elimu itolewe kwa wajumbe wote wa Bunge la Katiba namna ya kufanya kazi katika Bunge la Katiba. Tueleweshwe na pia tupatiwe elimu ya Kanuni ili pasiwe na mabishano wakati wa Bunge la Katiba kwa sababu ya muda mfupi tutakaokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kuwa Wajumbe wa Tume wapewe fursa ya kukutana na Wabunge wa Katiba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. V. SONI]

kutoa elimu pana ili tuingie ndani ya Bunge la Katiba tukiwa na maelewano juu ya kupata Katiba ya leo na siku nyingi zijazo. Pia pawe na mafunzo maalum kwa Waandishi wa Habari juuya Katiba/Rasimu ili na wao waweze kutoa habari juu ya ni nini kilichojiiri Bungeni na kutoa habari kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuona Taifa juu ya masuala ya kisiasa na kukutana na vyama vyote vya siasa vyenye Wabunge Bungeni na kupata maridhiano, ili nchi iwe na amani na umoja. Naipongeza pia Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri iliyoifanya na kutuelimisha juu ya marekebisho haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naamini tutapata Katiba mpya yenye manufaa kwa nchi yetu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa busara zake alizotumia kwa kuweka saini Muswada wa Mabadiliko ya Katiba baada ya kuridhia robo tatu ya mapendekezo na kurekebisha robo tu ya mapendekezo, kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wetu. Mabadiliko ya idadi ya Wajumbe watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais kutoka idadi ya 166 na kuongezeka kuwa 201, ambayo ni idadi iliyopendekezwa na Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria. Niwaombe Watanzania waelewe kuwa Wabunge watakaoingia kwenye Bunge Maalum la Katiba hawataingia na imani ya vyama vyao, kwani Katiba tutakayoionda itatoa haki kwa Watanzania wote. Tutambue kuwa haki, amani, uhuru na mshikamano kwa wote ndiyo msingi wa kila mjumbe atakayeingia kwenye Bunge hilo. Sitegemei Wajumbe kuingia na imani ya chama chochote.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nchi yetu ina idadi ya watu zaidi ya 45,000,000. Ni matumaini yangu kuwa kundi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D. M. CHILOLO]

kubwa la wajumbe siyo msingi wa kupata Katiba yenye kuwafaa Watanzania, bali wale wachache kutumia busara wakijua kwamba wakifanya makosa watakaoumia ni dada zetu, kaka zetu, wajomba zetu, shangazi zetu, mama zetu, baba zetu na kadhalika. Hivyo, lazima tuwe makini, tunapaswa kuondoa tabia za kuipotosha jamii.

Mheshimiwa Spika suala la ukumbi, idadi kubwa na kadhalika isitupotezee muda.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii na wote walioshiriki kufanya marekebisho kwa kushirikiana na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa nchi yetu ya Tanzania.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru Rais na Serikali kwa ujumla kwa kukubali Muswada huu kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, marekebisho yandefanyika vizuri zaidi iwapo Muswada ungerejeshwa Bungeni bila kusainiwa na Rais kwa mujibu wa Ibara ya 97(2) ya Katiba ya Nchi. Aidha, kasoro zilizojitokeza wakati wa kutungwa kwa Sheria Novemba, 2011 na wakati wa kufanyiwa marekebisho mwaka 2012 mwezi Februari na Septemba, 2013; inadhihirisha haja ya hoja ambayo niliwasilisha taarifa yake mwanzoni mwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mara baada ya Mheshimiwa Rais kukubali nchi kwanza, mchakato wa Katiba katika hotuba yake kwa Taifa tarehe 31 Disemba, 2010; mwezi Januari, 2011 nilipinga uamuzi wa Mheshimiwa Rais kuunda Tume bila kwanza sheria kutungwa na Bunge. Nilieleza kwamba ni muhimu suala hilo lijadiliwe Bungeni, Serikali iwezeshe kuelewa mwelekeo wa muda mrefu wa Katiba na hatimaye Bunge lipitisha Azimio la kutaka Muswada kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, Serikali ingeandaa Muswada kwa kuzingatia maoni ya wadau wote

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

na nchi ingeepushwa kufanya makosa na marekebisho ya mara kwa mara. Aidha, Serikali ingewezesha kuitishwa kwa Mkutano wa laivu wa Katiba (*Constitutional Convention*) ambao ingewezesha nia ya kupata maoni ya wadau ya mwelekeo mzima wa mchakato.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, ndipo ingetungwa sheria yenye kuongoza hatua zote tatu za ukusanyaji maoni (kupitia Tume ya Wadau) na kuandaliwa kwa rasimu, kujadili na kupitisha rasimu ya Katiba (kupitia Bunge maalum), na kuridhia na kuidhinisha Katiba mpya (kupitia Kura ya Maoni). Hivyo, marekebishwa yatapaswa kuendelea kujenga kuaminiana na muafaka wa Taifa kuwezesha nchi kupata Katiba mpya bora.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Muswada huu uliowasilishwa, napendekeza katika kifungu cha 2(a) kwa kurekebisha kifungu cha 22 cha sheria mama kwa kuongeza idadi ya wajumbe kufikia 292, ambayo ni theluthi mbili ($\frac{2}{3}$) ya Wabunge na Wawakilishi ambao jumla yake ni 438, ili kuepusha Bunge kuhodhiwa na Wajumbe ambao ni Wanachama wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 2(b), idadi ya mapendekezo yawe si chini ya manne (4) na si zaidi ya tisa (9) na majina yatoke kwenye Taasisi, Asasi na makundi yenye malengo yanayofanana kwa mujibu wa Jedwali la marekebisho nililowasilisha.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mapendekezo ya kifungu cha (3) na kifungu cha (4) cha Muswada.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kuwapongeza Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kupitisha Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 katika Bunge lililopita.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A.N. MAKILAGI]

Pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kusaini Muswada huo na sasa ni Sheria iliyofanya marekebisho katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83.

Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuitisha Mkutano Ikulu wa Viongozi wa Vyama vya Siasa kwa lengo la kusikiliza maoni yao juu ya Sheria iliyopitishwa na Bunge na baadaye kufikia maamuzi kuwa Viongozi wa Vyama vya Siasa kupitia Taasisi ya *TCD* wakutane na kutoa maoni yao juu ya sheria hiyo na mchakato wa Katiba Mpya na kuyawasilisha kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Viongozi wa Vyama vya Siasa kwa kukutana na kutoa maoni yao na kuyawasilisha Serikalini. Nawapongeza na waendeleo kufanya hivyo katika masuala muhimu yanayoigusa nchi yetu badala ya kutoa lugha zenye uchochezi.

Naunga mkono marekebisho ya Kifungu cha 22 kwa kufuta kifungu kidogo cha (1) na kukiandika upya kwamba sasa idadi ya Wajumbe watakaoteuliwa wawe 201 badala ya 166. Hii inaongeza wigo wenye tija katika yale makundi ya wenye mahitaji maalum kama vile wajane, yatima na watu wenye ulemavu na makundi mengine yote ambayo yana malengo yanayofanana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Kifungu cha 2A kinachompa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kualika kundi litakalotajwa katika kifungu kidogo cha (1)(c) kutoka kila pande ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nashauri makundi haya yaalikwe kutoka katika mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuepukana na uteuzi wa Wajumbe kutoka mkoa mmoja tu au maeneo ya mijini tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi kwa Taasisi wakati wa kuwasilisha majina kwa Mheshimiwa Rais, naomba sana Taasisi zote zizingatie kupeleka orodha ya uwakilishi ulio sawa kati ya wanaume na wanawake. Katika kuwapa nguvu hizi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A.N. MAKILAGI]

Taasisi, nashauri pia namba itakayowasilishwa kwa Rais kutoka katika hizi Taasisi kuwa kati ya sita hadi 10. Ili kutoa mwanya kwa baadhi ya Taasisi kupendekeza majina kwa usawa 50/50 kati ya wanaume na wanawake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Rais, wakati wa uteuzi wa Wajumbe wa Bunge la Katiba, azingatie uteuzi ulio sawa kati ya wanaume na wanawake kama ambavyo Sheria hii inatamka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kifungu cha 22(c) kinachotaja idadi ya wajumbe, kipengele (iv) kirekebishwe badala ya kusomeka Wajumbe 20 kutoka Taasisi za Elimu ya juu kisomeke wajumbe 20 kutoka Taasisi za Elimu ili kutoa nafasi kwa wajumbe toka Vyuo, Sekondari, Elimu ya Msingi na kadhalika.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na kuunga mkono hoja, lakini napendekeza Wajumbe wa *EALA* Watanzania wawe Wajumbe wa Bunge la Katiba. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa mtoa hoja sijui mmejipangaje anaanza Naibu, Mheshimiwa mtoa hoja ameanza kujibu zile hoja.

WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuja kuhitimisha hoja niliyoileta na imejadiliwa na Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa jinsi ulivyoweza kuisimamia Bunge lako hili na kuisimamia hoja hii na ikaendeshwa kwa jinsi ilivyoendeshwa.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

Hoja imeendeshwa vizuri sana, niendeleo kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye kwa kutukutanisha Serikali na vyama vya Serikali alitumia busara kubwa sana. Wakati alipofanya jambo lile kulikuwa na tension kidogo katika nchi na kama asingefanya alivyofanya sijui kama tungekuwa tuko leo hapa katika hali hii tuliyonayo. Kwa hiyo, namshukuru sana ameonyesha ukomavu mkubwa wa kisiasa, ameonyesha uongozi ambao kwa kweli unamstahili.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nitoe shukrani zangu kwa viongozi wote wa vyama vya siasa walioshiriki katika mchakato huu niwashukuru sana, nimshukuru sana Mheshimiwa James Mbatia ambaye ndiyo alikuwa kiongozi kwa upande *TCD*, amekuja na wenzake na wamekuja na mawazo mazuri mengi manzuri ambayo tulichukua muda wa kuyajadili.

Lakini nimpongeze zaidi kwa sababu pale tulipofikia tumeridhiana na amekubali hivyo. Nimpongeze Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa mara ya kwanza nimeona Muswada wa Serikali akiuunga mkono kwa nguvu zake zote napenda nimpongeze sana. *(Makofi)*

Hakuupinga ameunga mkono na pamoja na haja ya mambo mengine lakini ameelewa kwamba tunapozungumza yako mambo mengine unapata mengine unakosa lakini huu ni mwanzo mzuri sana wa kujenga maridhiano baina ya vyama na nafikiri huko tunakokwenda tutahitaji sana spirit hii kwa sababu tuko katika kujadili hatima ya nchi yetu. tunajadili hatima ya wajukuu zetu, lazima tukae tuelewane ili tutakapotoka tumalize vizuri tupate kitu kizuri.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Eng. Mnyaa vilevile naye amepata uongozi huu si muda mrefu lakini ameonyesha kwamba ni kiongozi mzuri sana, na amekiongoza chama chake katika majadiliano haya na tumefikia mwafaka mzuri. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

Kwa upande wetu nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi, ambaye naye alikuwa ndiye kiongozi katika timu yetu naye alikuwa mvumilivu, msikivu na mwisho wa siku tumefika mbele ya Bunge lako Tukufu na Muswada ambao unawakilisha mawazo yetu wote. Ndiyo maana hakuna kiongozi aliyesimama hapa akaupinga Muswada huu. Lakini nyuma ya shughuli zote hizi tulikuwapo na viongozi wengine ambao walikuwa wanashiriki kikamilifu katika kuongeza chachu na kuongeza mawasiliano mazuri ili tuweze kuelewana.

Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Abubakar Bakar, Waziri wa Sheria na Katiba Zanzibar ambaye mpaka sasa yupo hapa nasi ameshiriki nasi vizuri, akiwakilisha Serikali ya Zanzibar nimshukuru sana, tumeshirikiana vizuri mpaka tulipofika hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba niseme mjadala wa jana umejaa hekima, umejaa busara nyingi sana umeonyesha mshikamano mkubwa baina ya Wabunge wa pande zote unanitia matumaini makubwa sana kwamba mjadala ujao huko mbele nayo itakuwa mizuri na itaishia vizuri katika kupata maelewano na muafaka mzuri.

Mheshimiwa Spika, wapo wachangiaji ambao wametoa hoja mbalimbali na mimi nakusudia kuzizungumzia chache tu. Kubwa sana katika majadiliano haya kutoka huko mwanzo ilikuwa ni suala zima la mamlaka ya uteuzi katika watu hao 201 je, wateuliwe na nani. Hili lilikuwa limezunguzwa sehemu nyingi na sehemu nyingi tumezitolea maelezo. Tulisema kwa vile watu 201 hawa watakapokuwa ndani ya Bunge lile wanatakiwa wawe ni watu ambao wanaonyesha uasili wa nchi yaani wanaonyesha mgawanyo na mtawanyiko wa jiografia, mgawanyo na mtawanyiko wa kijinsia ujuzi na kadhalika. Maana nia ya watu hawa 201 siyo sana sana kuwa wawakilishi.

Katika Bunge maalum la katiba wawakilishi wamejaa tupo Wabunge ambao ndiyo tunawakilisha

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

wananchi wote, wapo watu wa Baraza la wawakilishi ambao wanawakilisha wananchi wote, tukasema waongezwe watu wengine ambao wenye busara, watu ambao wenye ujuzi na kwa kweli hatukumaanisha wanawakilisha watu wengine hapana, ila wanawakilisha mawazo ambayo pengine atakuja kutuchangia sisi humu ndani ili tuweze kutoa katiba nzuri katiba ambayo itakuwa imesheheni umahiri mkubwa.

Kwa hiyo, tukasema basi tutangaze watu hawa tuwapate kutoka sehemu gani, tuwapate kwenye makanisa, kwenye misikiti, kwenye vyombo vya dini, kwenye NGOs, kwenye makundi ya wakulima, wavuvi, wafanyakazi na kadhalika, basi tukasema tutumie utaratibu kwamba itatangazwa katika magazeti na mara tu mkishapitisha sheria hii nafikiri ndiyo kazi kubwa itakayokuwepo kwa hiyo wale ambao watataka kupata wawakilishi watapeleka mapendekezo yao na Rais atateua watu kwa msingi huo.

Wazo lilikuwepo kwamba kila chombo ama NGO wapeleke wenyewe waseme sisi tumemteua Mheshimiwa fulani basi awe ni huyo huyo. Hilo ni wazo zuri lakini utekelezaji wake ulikuwa hauwezi ku-guarantee ule mtawanyiko wa kijijografia tunaouzungumzia ulikuwa hauwezi ku-guarantee jinsia, ulikuwa hauwezi ku-guarantee mambo hayo yote maana ungesema NGO walete watu 20 italeta wote wanaume.

Basi hakuna mtu ambaye anaweza akafanya ile *natural mix* akasema aah! Jamani wote wanaume halafu wote hawa wanatokea Nachingwea tu itakuwaje.

Kwa hiyo, lazima awepo mtu mahali aseme hebu tujaribu ku-*balance* wanaotokea makanisani, misikitini, wanaotoka Nachingwea wanaotoka Musoma tukasema basi Rais afanye kazi hii na ndiyo baada ya mazungumzo marefu likakubalika kwamba basi mteuzi awe ni Rais ni kazi ngumu, kazi ngumu sana, lakini Rais huyu aliomba kutawala nchi hii hiyo pia ni kazi ngumu zaidi haiwezi kushindwa na hii ndogo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

Kwa hiyo tumekubaliana mteuzi atakuwa mmoja, tukasema okay tupeleke majina wangapi kwake, ubishani ukawa kati ya matatu, baadaye ikawa sita mpaka tisa. Mwisho baada ya baada ya majadiliano tumekubaliana ni watu wanne mpaka tisa, NGO itapeleka huko mashirika ya dini yatapeleka huko watu wanne mpaka tisa, basi Rais atakaa na vyombo vyake mwisho wa siku atatuteulia watu kutoka mapendekezo hayo haitakuwa nje ya mapendekezo hayo.

Kwa hiyo, suala hili la nani ateue tukawa tumelimaliza ateue kutoka wapi, pia nalo tukawa tumelimaliza. Kubwa jingine ambalo lilikuwepo ni hoja ya uhai wa tume ya katiba. Kukawa na mapendekezo kwamba tume hii iendelee mpaka siku ile tutakapotangaza katiba mpya. Mapendekezo hayo yalikuwepo na yalijadiliwa katika ngazi zote hizi. Lakini mwisho wa siku ikakubalika kwamba tume hii ina kazi maalum, na tume hii chini ya kifungu cha tisa cha sheria ilipewa majukumu ambayo yako wazi kabisa, kwamba itafanya kazi ya kukusanya maoni itatoka mwisho na taarifa na rasmu ya katiba ikishafanya hivyo itakuwa imemaliza muda wake na ndiyo maana ya tume hizi unapoteua tume unaipa kazi maalum na ikamilisha kazi ile tume ile ina since kuwepo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukasema jamani lazima tufanye hivyo ifike mahali tume hii imefanya kazi, tume ya watu 32 ilizunguka nchi nzima ikakusanya maoni ya watu, maoni yale yakapelekwa kwa watu takribani 15,000 wakayajadili kwenye mabaraza yao ya katiba. Sasa maoni haya na wale watu 15000 hawakuendelea kuwepo walishafanya kazi yao wamemaliza. Sasa maoni haya yakapelekwa 630 na ushee, hawa nao watayajadili, wakishayamaliza kuyajadili na wenyewe kazi yao itakuwa imekwisha sasa yatapelekwa kwa wananchi wote ili wayapigie kura. Huu ni mchakato na kwa hiyo kila chombo kinapokwenda halafu kazi yake ikiisha na chombo kile kinaisha tukasema kwamba Tume nayo iishe wakati ikishamaliza tu kutoa taarifa na kutoa rasimu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

Lakini pia kuna suala lingine wazungu wanaita *principle of bias*, anapotakiwa uandike wewe *document* yako umpelekee mtu ukipeleka kule kama hatakuuliza yule mtu lazima wewe utakwenda kuitetea, unaiona hii ni ya kwako na *principle bias* inasema lazima utaenda uitetee. Tumeona hata haya katika mabaraza ya katiba wapo wajumbe wengine wa tume, walikuwa wanakwenda kutetea badala ya kwenda kutetea, wakawa wanatetea sana hoja yao. kwa hiyo ni kitu *natural* kwa binadamu, nimeandika hiki changu ukiniuliza nitakwambia this is the best kwa hiyo, itaendelea kuwa hivyo.

Sasa tukifanya hivyo tunawapa nafasi gani wajumbe wa Bunge, Wabunge la Bunge la Katiba kujadili kwa uhuru na kwa uwazi jambo hili. Nafikiri Tume, iishe pale itakapoisha na ndiyo tulivyokubaliana na tumeleta katika mapendekezo ya waraka wetu. (*Makofi*)

Nikumbushe tu makubaliano haya ni muafaka wa majadiliano ya muda mrefu, baina ya vyama na baina ya Serikali. Kwa hiyo, hapa yalipo ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wasilete mabadiliko makubwa makubwa sana, ila intake kuzingatia kwamba yako mabadiliko ambayo ni muhimu ambayo nadhani sisi tunaweza kuyakubali *immediately*. Kwa mfano, lipo pendekezo lilitolewa na ndugu yangu mama Margreth Mkanga kwamba, tufute maneno *person's with special need*, badala yake tuweke maneno, *people with disabilities*.

Sasa hili mimi nalikubali moja kwa moja kwa sababu ni matumizi tu ya *terminology* hizi. *Persons with disabilities* na *person's with special needs*. Maana hawa watu wenye *special needs* ni nani? Ni hawa hawa, watu ambao wana *disabilities*. Nitakachojaribu kusema na nitawataka waandishi wa Sheria, pale wanaposema *people with special need*, badala yake waseme *persons with disabilities*, na ndiyo hasa inavyotumika, badala ya *people with disability* iwe *person's with disabilities*.

Jingine ambalo nitalikubali moja kwa moja nalo ni katika kifungu cha 22(2)(c) iv, kinasomeka kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

wajumbe kutoka taasisi za Elimu ya juu. Sasa kuna wajumbe wanatoka kwenye Taasisi za Elimu, lakini pengine siyo Elimu ya Juu. Watu kama wanaotoka VETA. Sasa wale wataingiaje? Kwa hiyo, tuseme badala ya taasisi za Elimu za juu, tuseme taasisi za elimu. Tuziache hivyo na pendekezo hili nitalikubali limeletwa na Mheshimiwa Lukokola, naliona linafaa na ni zuri sana.

Nieleze tu kwamba, makundi haya yatakapoalikwa yataalikwa kutoka nchi nzima, na msingi wa wale 201, ni kwamba, nusu yake watakuwa wanawake na nusu yake watakuwa wanaume. Sasa kwa vile ni watu 201, nataka niamini kwamba wanawake watakuwa 101 na wanaume watakuwa 101. *(Makofi)*

Tutawapa *advantage* akina mama. *(Makofi/Vicheko/Vigelegele)*

SPIKA: Hawa watakuwa na hatari kama watakuwa na Bunge baadaye watakuwa wanapiga vigelegele. *(Kicheko)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, sasa yapo mapendekezo ambayo yamependekezwa na rafiki zangu wawili ambayo ni makubwa kidogo na mimi nimejaribu kuongea nao binafsi. Binafsi nimeongea na Mheshimiwa John J. Mnyika, ambaye amependekeza namba ile ibadilike kutoka 201 iwe 292. Nimejaribu kuongea naye sana, kwa kweli ametengeneza kesi yake amejenga na imezungumzwa katika hatua zote za mjadala huu. Kwa bahati mbaya haikufanikiwa na mpaka juzi haikufanikiwa hata katika Kamati ya Bunge.

Sasa ningemwomba kwa kuokoa muda, ataileta tena, ataizungumza tena, lakini ningemuomba tu kwa kuokoa muda na nilimuomba jana, nataka niamini kwamba kwa sababu ni mtu ambaye tunaelewana sana, basi ataitoa iliisiendelee.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

Kama vile ambavyo nilimwomba Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka naye amejaribu kuleta hoja ya mugawanyo wa nafasi za wajumbe wale 42 wa vyama vyenye usajili wa kudumu, akajaribu kuleta hoja ambayo nilidhani kidogo inaweza ikaleta mjadala mrefu sana. Hata hivyo, ningependa kumkumbusha tu kwamba, hii iliyoletwa hapa ndiyo makubaliano tuliyoyafanya huko ya vyama. Ni makubaliano ambayo tumeyafanya baada ya mazungumzo ya muda mrefu na maridhiano ambayo tumeyafanya.

Kwa hiyo, ningemuomba na yeye pia, kama nilivyomuomba jana kwa kuwa hakunikatalia, basi tukifika wakati huo aondoe suala hili ili tuendelee tuzingatie maelewano tuliyoyafanya kivyama.

Lipo moja limeletwa na Mheshimiwa Jenista J. Mhagama ambalo nafikiri lilikuwa ni tatizo la uandishi kwenye kifungu cha Muswada, kifungu cha tatu(a) lakini kwenye sheria ni kifungu cha 24, ambacho kinapaswa kusema kwamba, *notwithstanding the provisions of* badala yake kimeandikwa kinamna namna hivi ambayo sasa haiteti maana. Nia ilikuwa kutoa madaraka kwa Makatibu wetu wa Bunge na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kufanya kazi zao katika kipindi hiki cha maandalizi ya kufikia hapo tutakapokuwa tunaanza Bunge Maalum. Yapo maandalizi ya muhimu ya kufanyika, kwa mfano kama tutakuja kufanya kwenye ukumbi huu, itabidi ukumbi huu urekebeshwe na kuna maana ya *contracting*, kuna mtu aje kufanya hayo. Kama kuna haja ya kuandaa makaratasi yoyote, *documentations* na nini na vitu kama hivyo, inabidi vifanyike mapema, lakini hawa wasingeweza kufanya bila kupewa madaraka hayo na sheria. Kwa hiyo, nakubaliana na mapendekezo yale ya Mheshimiwa Jenista J. Mhagama. Kifungu hicho kitarekebishwa *accordingly* ili tuweze kuwapa haya madaraka hawa wenzetu viongozi wa Bunge ili waweze kufanya maandalizi ambayo tutayahitaji yafanywe kabla Bunge Maalum la Katiba halijakaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli naomba niseme tu, mjadala umekuwa mzuri, umeonyesha ukomavu, mjadala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA]

umeonyesha hekima kubwa na watu wengi waliochangia wameunga mkono. Nisipende kuchukua muda mwingi sana ila tu nitoe rai kwa Waheshimiwa wabunge wote kwamba, tupitisha sheria hii ili tuanze kuifanyia kazi kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo machache na kwa vile Muswada wenyewe una vifungu vitano tu, nategemea hakutakuwa na mjadala mrefu sana. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo machache, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)
(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka, 2013 [The *Constitutional Review (Amendment No.2) Bill, 2013*]

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na
Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Ibara ya 2

JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA MHE.
MATHIAS CHIKAWA, WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA WAKATI WA
KUSOMWA KWA MARA YA PILI MUSWADA UITWAO "SHERIA YA
MABADILIKO YA KATIBA (MAREKEBISHO NA. 2) YA MWAKA 2013

Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 86(10)(b)

Muswada wa Sheria uitwao Mabadiliko ya Katiba
(Marekebisho Na. 2) ya mwaka 2013 unafanyiwa marekebisho
ya ujumla.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

A: Katika Ibara ya 2(a) kwa: (a)kufuta neno "sita" linaloonekana kwenye kifungu kidogo cha (2A) na kulibadilisha kuwa "nne";

(b)kufuta maneno "Chama kinachowakilisha" yanayoonekana katika aya ndogo ya (vii) na kuyabadili na maneno "vyama vinyowakilisha";

(c) Kufuta maneno "Chama kinachowakilisha" yanayoonekana katika aya ndogo ya (viii) na kuyabadili na (d) maneno "vyama vinyowakilisha".

Dodoma
8 Novemba, 2013

MC
WKS

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MATHIAS CHIKAWA, THE MINISTER FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND READING OF A BILL TITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT NO. 2) ACT, 2013"

Made Under Section 86(10)(b)

A Bill titled the Constitutional Review (Amendment No. 2) Act, 2013 is generally amended as follows:

A: In clause 2 (a) by:

(a) deleting the word "an" appearing in item (vii) of paragraph (c) and adding a letter "s" at the end of the word "association";

(b) adding a letter "s" at the end of the word "association" appearing in item (viii) of paragraph (c); and

(c) deleting the word "six" appearing in subsection (2A) and substituting for it the word "four".

Dodoma
8th November, 2013

MC
MCLA

MWENYEKITI: Tuanze na Mheshimiwa Mkanga!

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON.
MARGARETH AGNES MKANGA A MEMBER OF
PARLIAMENT SPECIAL SEATS AT THE SECOND READING OF
A BILL ENTITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW
(AMENDMENT NO.2) ACT, 2013

[Made Under S. O. 86(9) & (11)]

A Bill entitled "The Constitutional Review
(Amendment No. 2) Act, 2013 is amended as follows-

- A. In clause 2(a) (v)
- B. By deleting the words "special needs" and substituting for them the word "disabilities"

HON. MARGARETH AGNES MKANGA (MP)
SPECIAL SEATS
7/11/2013

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuhitimisha suala langu. Kwa kweli bila kupoteza muda niseme naishukuru Serikali kwamba iliweza kukubaliana na kuona uzito wa kurekebisha hiyo ibara ya 2(a) kifungu cha tano (v) cha kirumi. Sasa badala ya yale maneno ya *special needs*, tuweke peupe kabisa *disabilities*, ninashukuru sana na ninaomba Waheshimiwa wenzangu wote hili tuliunge mkono kwa sababu tutawapa nafasi waandaji wa Ukumbi na kila kitu kuweza pia kufikiria kuweka wazi yale ambayo yanawahusu hawa wajumbe watakaokuwa wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli nisipoteze muda, naendelea kushukuru na kuwaomba wenzangu kwamba hili tukubaliane ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwishasema kwamba hilo tumelikubali na tatalirekebisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Litakaaje sasa kwenye Sheria?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Maneno ni kwamba, *persons with disabilities*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa sawa, kwa hiyo inaingia wapi? *Roman five* (v) naomba mtusomee kama itakavyokuwa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: *Roman five* (v) tunasema, *twenty members from groups of persons with disabilities*, badala ya inavyosomeka sasa, *twenty members from groups of people with special needs*. *Isomeke twenty members from groups of persons with disabilities*.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

MBUNGE FULANI: Hayupo.

MWENYEKITI: Badala yake, Mheshimiwa Lediana M. Mng'on'go!

MHE. LEDIANA M. MNG'ON'GO: Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kwanza naomba niipongeze Serikali, nampongeza Waziri kwa kukubali kwamba kati ya Wajumbe 201...

MWENYEKITI: Fanya *amendment!*

MHE. LEDIANA M. MNG'ON'GO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* yangu ni sehemu ya pili (a) kifungu 2(b) kipengele (b). Ningependa tubadilishe neno pale inaposema, *taking into consideration gender balance*, napenda tuondoe neno *balance* tuweke neno *parity*. Ninasema hivyo kwa sababu, katika tafasiri ya Kiswahili imeleeza vizuri kwamba, usawa wa kijinsia, lakini ukija

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. L. M. MNG'ON'GO]

kwenye Kingereza inasema *gender balance*. *Gender balance* inategemea na mtu atakavyotafasiri. Kwa hiyo, ndiyo maana inategemea na mtu atakavyotafasiri, ndiyo maana nimeona tuweke *parity* badala ya *balance*.

Kwa kuzingatia yale yote ambayo tumeshaeleza huko nyuma ili nisirudie kueleza upya, kwamba wanawake hata humu ndani Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano; tuko asilimia 36 na tukiwaongeza wale wa Serikali ya Baraza la Wawakilishi bado pia ni wachache. Kwa hiyo, tukipata asilimia 50% ambayo, itakuwa imeongeza wale wanawake kwa hiyo, tutakuwa tumeongeza namba, tukizingatia kwamba wanawake ni asilimia 51, sauti yao inatakiwa isikike humu ndani na tunajua kwamba tukifika kwenye kura za maoni watakao toa nafasi wengi ni wanawake. Kwa hiyo, naomba ionekane wazi kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza wakati nafanya majumuisho, hili tulikubali na *infact* tutashindwa tu jinsi ya kuandika yule mmoja anampataje maana atakuwa ni mia moja na moja, itazidi hata hiyo *gender parity*, lakini tunakubali kwamba sasa, kifungu kile (d) kisomeke *take into consideration gender parity* badala ya *balance*. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mnyika!

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina mapendekezo ya marekebisho kwenye kifungu hicho na marekebisho hayo ni ya kuongeza idadi ya wajumbe, kutoka 201 mpaka 292. Idadi ya wajumbe wanaotoka nje ya vyama vya siasa. Ningependa maelekezo yako, iwapo katika hatua ya sasa niwasilishe kuhusu kipengele (a) cha jedwali langu na kipengele (b) ama niwakilishe kipengele (a) peke yake cha jedwali kinachohusu idadi.

MWENYEKITI: Naomba uanze na kimoja tu, wafanye maamuzi halafu tuendelee.

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN
JOHN MNYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE CONSTITUTIONAL REVIEW
(AMENDMENT NO. 2) ACT, 2013

Made Under Standing Order 86(11) and 88(2)

A bill entitled "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT NO. 2) 2013" is amended as follows:

A: In Clause 2(a) amending newly introduced sub section "c" by deleting the words "two hundred and one" and substitute with the words "two hundred and ninety two."

B: In clause 2(a) which introduces new subsection (c) i, ii, iv, v, vi, vii, viii, ix and x by:

(i)Deleting the word "twenty" replace with "thirty one."

(ii)Deleting the word "twenty" and replace with "thirty one."

(iv)Deleting the word "twenty" and replace with "thirty one."

(v) Deleting the word "twenty" and replace with "thirty one."

(vi) Deleting the word "nineteen" and replace with "thirty."

(vii) Deleting the word "ten" and replace with "sixteen."

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(viii) Deleting the word "ten" and replace with "sixteen."

(ix) Deleting the word "twenty" and replace with "thirty one."

(x) Deleting the word "twenty" and replace with "thirty three."

.....
JOHN JOHN MNYIKA (MP)
UBUNGO CONSTITUENCY
8. 11. 2013

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hapa ni kuongeza idadi kutoka 201 mpaka 292. Jana nilitambua na nilishukuru Serikali kwa kuongeza idadi kutoka 166 mpaka 201. Hata hivyo, nilieleza kwamba, pendekezo hili bado halijakizi mahitaji.

Wakati Waheshimiwa Mawaziri wanachangia hoja jana, ilielezwa kwamba, hoja hii ya kuongeza idadi ya wajumbe ni kwa sababu tu ya kutaka usawa na hadhi sawa katika Bunge la Katiba. Hii ni kati ya sababu moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya maelezo ya jana, nimekwenda kufanya rejea ya waraka ambao wakuu wa vyama vya siasa walimwandikia Mheshimiwa Rais. Wakuu wa vyama vya siasa vyote kwa ujumla wake walimueleza Mheshimiwa Rais kuhusu namna ambavyo Bunge la Katiba litahodhiwa na wanasiasa na vyama vya siasa. Likatoa rai, kwa Mheshimiwa Rais, kwamba hali hii, rai ambayo sasa naomba nitoe kwa Waheshimiwa Wabunge wezangu.

Kwamba, rai hii isiporekebeshwa, itakuwa na maana ya kwamba, Katiba mpya itatokana na matakwa ya vyama vya siasa ambavyo idadi yao ya jumla ya wanchama wao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

haifiki milioni kumi kati ya Watanzania zaidi ya milioni 45 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Kwa sababu hiyo, wadau karibu wote, iwe ni taasisi za dini, vyama vya wafanyakazi, vyama vya taasisi ya elimu ya juu, vyama vya walemavu. Wadau karibu wote waliokuja mbele ya Kamati ya Katiba na sheria, walipendekeza idadi ya wajumbe wasiokuwa Wabunge na wawakilishi, iongezwe hadi kufikia theluthi mbili ya wajumbe wote wa Bunge maalum.

Kama haiongezwi basi wakatoa pendekezo wadau kwamba idadi ya Wabunge na wawakilishi ipunguze kufikia theluthi moja ya Wajumbe wa Bunge Maalum. Sasa kwa kuwa pendekezo la kupunguza Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi haliwekezani kutekelezeka, suluhisho pekee, kwa maoni mbalimbali yaliyotolewa ni kuongeza idadi ya wajumbe wengine nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo msingi wa pendekezo wa 292. Hii nambari 292 ni mbili ya tatu ya jumla ya Wabunge na wawakilishi ambayo jumla yake ni 438. Mbili ya tatu ya hawa wote kwa ujumla wake ndiyo 292.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lina *implication* kubwa sana kwenye upitishaji wa Katiba. Kwenye maamuzi juu ya Katiba tutakapokaa kama Bunge maalum la Katiba, wakati wote, tutakaa pande mbili za Muungano kwenye kuamua. Tutakapokaa upande wa Tanzania Bara na upande wa Zanzibar peke yao. Waheshimiwa Wabunge mnaweza mukanza kufikiri kuanzia sasa.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Kengele hiyo, ni dakika tano umemaliza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono sauti hii ya makundi mbalimbali ya kijamii nchi nzima.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesikiliza vizuri maelezo ya Mbunge mwenzangu, kijana mwenzangu Mheshimiwa John Mnyika ambaye namuheshimu sana kwa uwezo wake. Hata hivyo, kama ambavyo tumesema, siyo kila kitu ambacho katika makubaliano ya kwako yakapita yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa naamini kama mimi pia, ningependa labda wajumbe wangebaki wale wale 161. Lakini kwa ajili ya kutengeneza muafaka wa Kitaifa, Serikali na yenyewe ikakubali kuongeza kufikia wajumbe 201.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kusema kwamba sisi vyama vya siasa wanachama wetu hawazidi milioni kumi, jambo hilo nalikubali. Lakini Wabunge humu ndani wote mitakubaliana na mimi hatukuchaguliwa na wanachama wetu peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechaguliwa na watu wengi ambao wengi hao hawana vyama. Sasa sioni hofu ya uwakilishi wa Wabunge sisi tuliokuwa humu ndani, kwa ajili ya kuleta mawazo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya kwamba Wabunge wa CCM tuko wengi, katika suala la Katiba, mutakubaliana na mimi Wabunge wenzangu misimamo tunatofautiana. Kwa hiyo, kuna mambo ambayo tutakubaliana tu kwa maslahi ya Taifa katika kutunga Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona kwamba, bado idadi ya 201 inatosha kwa sasa, tukubaliane tuvuke salama ili tuweze kutengeneza Katiba ambayo itakuwa bora kwa Taifa letu. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imengonga.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi, mimi nasimama kutoa maoni kwamba mapendekezo yaliyoletwa na Serikali yabakie vilevile kwa sababu kubwa tatu.

Sababu ya kwanza, sababu iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu ya kwanza wanaongeza idadi ili mchakato usihodhiwe na wanasiasa na Vyama vya Siasa, inapingana na msimamo ya kwanza. Niwakumbushe Wabunge na Watanzania kwamba katika Muswada wa kwanza ambao tulipokuwa tunajadili Upinzani ukatoka, moja ya hitaji lao ilikuwa ni kwamba wanasiasa wahusishwe kwenye suala hili kwa sababu suala la Katiba ni suala la wanasiasa. (*Makofi*)

Ndipo Serikali ikafikiria kuwaweka wanasiasa, kulikuwepo na mambo mengi sana yaliyokuwa yanataka tuwaweke pembeni wanasiasa, lakini madai yao yakawa wanasiasa wahusishwe. Niwaombe tu tuwe tunakumbuka vitu tunavyodai ili kuepusha kudai vitu vilevile ambavyo tulishavipigia kelele na hasa kutishia Usalama wa Taifa.

Jambo la pili, mimi niwahakikishie Watanzania, kwenye hili jambo la Katiba, kuna watu wana *allergy* na hili neno CCM, wanasema labda wana CCM humu ndani wako wengi. Hivi majuzi tulienda kwenye Mabalaza ya Katiba mpaka Vijijini, asilimia 90 ikawa CCM. (*Makofi*)

Kwa hiyo, popote utakapokwenda kuwavua Watanzania utakutana tu na wana CCM. Hata leo hii tukamua Bunge la Katiba tutafanya Mikutano ya Hadhara ya kila Wilaya, tukitafuta theluth Mbili asilimia kubwa itakuwa ni wana CCM, kwa sababu ndiyo hali halisi, hili halikwepeki. Tuzingatie hoja, msingi wa hoja ndiyo utakaofanya watanzani waegemea kwenye ile hoja ya msingi, tukiwa na vitu moyoni mwetu ambayo inalengalenga mambo tuliyonayo kifichoni yanayohusu uanasiasiasa hatutafika na hatutaweza kupata Katiba iliyo nje, tuzingatie jambo la msingi la namna hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. N. MADELU]

Kwa hiyo, naomba mapendekezo ya idadi ile iliyoletwa iendelee kuwa vilevile.

MWENYEKITI: Waheshimiwa mjue anayetoa hoja ana dakika tano, ninyi mnaoungamkono ni tatu tatu. Kwa hiyo, mkijipanga mjipange kwa tatu maana naona *arguments* zinakuwa hazijamalizika dakika zimekwisha. Maana yake hamjipangi vizuri. Mheshimiwa ambaye hajazungumza sana, Mheshimiwa Pindi Chana.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubaliana na kwamba tunapaswa kuwashirikisha Watanzania na ninaomba niseme kwamba ni jambo la msingi, na Kamati ililiangalia hilo la kuwashirikisha Watanzania, lakini siyo kwa mtazamo wa kutoka 201 kwenda 292 kama maelekezo ya mtoa hoja anavyoweka. Kamati ililiona katika *angle* ifuatayo. Wanashirikishwa Watanzania wote wenye umri wa zaidi ya miaka 18, wenye sifa ya kupiga kura kutipitia *Referendum*. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukiwaongeza hawa wachache, bado kutakuwa kuna maoni kutoka kona nyingine kwamba hata tunaotaka kuwaongeza 35 bado ni wachache. Kwa hiyo, mimi naomba Bunge lako Tukufu likubaliane kwamba baada ya Bunge la Katiba, tunakwenda *Referendum*. Daftari la Kudumu, linaboreshwa. Pale ambapo tuna Mtanzania mwenye umri zaidi ya miaka 18, mwenye sifa za kupiga kura atakuwa ana haki ya kutumia haki yake ya kupiga kura.

Kwa hiyo, suala la kuongeza wale watu haki yao inabaki kwenye suala zima la *Referendum*. Idadi ya watu wa Bunge la Katiba inatosha kama ilivyoletwa na Serikali. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tangu jana Bunge hili linakubaliana kwamba tufanye maamuzi kwa kutazama nchi na tusifanye maamuzi kwa kutazama vyama vyetu. Kuna kila hisia na wachangiaji waliotangulia wameeleza kwamba inawezekana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. D.Z. KAFULILA]

wakiongezwa watu kutoka nje huenda wakawa ni watu ambao hawaambatani na misimamo ya Chama fulani.

Hisia hizo amezungumza Mheshimiwa Ester Bulaya. Mimi naomba tukubaliane, kwamba mchakato wa Katiba ni zaidi ya Vyama, ni zaidi ya wanasiasa. (*Makofi*)

Tusijjaminishe kwamba sisi wanasiasa tuna uwezo mzuri, au ni wazalendo sana kuliko walioko nje ya siasa. Hapa ndipo maeneo ambapo tunapaswa kuonyesha kwamba hii nchi sasa imekutana kufanya mwafaka wa Kitaifa na siyo mwafaka wa Vyama. (*Makofi*)

Bunge la Katiba likijaa Vyama, utakuwa ni mwafaka wa Vyama katika nchi hii na siyo mwafaka wa Kitaifa. Naomba tujiulize hiyo nyongeza ambayo Mheshimiwa Mnyika anasema ya kufikia 292 tukiipitisha, CCM inapoteza nini! (*Makofi*)

Tujiulize kwamba tunaunga mkono hoja hii ni kwamba tunahisi kwamba hoja hii isipopitisha tutapoteza wa tu muhimu watakaolingia kwenye Bunge la Katiba ambao wanatoka nje ya siasa na siyo kweli kwamba *Referendum* kule ndiyo wakashirikishwe wote kwamba inatosha, Bunge la katiba litafanya kazi kubwa ambayo kimsingie kwenye *Referendum* ni kupiga kura tu. (*Makofi*)

Kuna kila umuhimu wa kuhakikisha tunaongeza idadi ya kutosha ili kusudi Bunge hili la Katiba lichukue sura ya nchi na siyo sura ya Baraza la Wawakilishi na sura ya Bunge la Muungano. Hiyo ndiyo nasaa yangu kwao ambao wanapinga hoja hii.

Hoja ya Bajeti.....

MWENYEKITI: Waheshimiwa, kinacholeta ukakasi ndani ya vichwa hivi mnapozungumza habari ya Vyama, mimi napata shida kweli, kwa sababu hapa ni Katiba, tuzungumze mantiki, lakini ukinza kuingiza Vyama mtafanyaje? Nasema kwa wote, Mheshimiwa Wenje, sikiliza,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI]

nasema kwa sisi, sisemi kwa mtu, nasema sisi sote humu tukizungumza habari ya vyama inakuwa inaleta ukakasi kabisa. *Impression* mnayotoa hawi nzuri. Sisemei kwa mtu yeyote nasema sisi wote, tuzungumze mantiki ya kubadilisha historia. Naombeni sana Waheshimiwa Wabunge, *impression* mnayopeleka, kama mnakwenda kujadili kule mambo ya vyama, *honestly* siyo siyo nawaombeni Wabunge wote *without exception* tafadhali. Alisimama nani huku nilimwona, Mheshimiwa Tundu Lissu, dakika tatu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema jana nimesema mara nyingi sana kwamba tunahitaji kujifunza siyo kutokana na historia yetu peke yake lakini vilevile tutahitaji kujifunza kutokana na historia ya jirani zetu. Kenya ilipitisha Katiba mpya mwaka 2010, Bunge la Katiba la Kenya lilikuwa na wajumbe 629, kati yao Wabunge walikuwa 222. Wajumbe 407 waliobaki walitoka nje ya Bunge na nje ya vyama vya siasa. (*Makofi*)

Nafikiri pamoja na kwamba ina miaka mitatu tu, Katiba ya Kenya ni moja ya *the best Constitutional documents around*. Sasa watacheka lakini ndiyo hivyo. Hapa tunataka tupitisha Katiba mpya kwenye Bunge la Katiba ambalo asilimia zaidi ya 70 ya Wajumbe wake watatoka kwenye Vyama vya Siasa Bungeni. Watatoka kwenye vyama sita vya siasa, wengine wote watakuwa nje. Sasa.....

MWENYEKITI: Haya, kengele tayari, hatuanzi mjadala upya, tunataka...Mheshimiwa Mbowe unajibu kwa niaba ya Mnyika? Maana yake kuna kujibu, mimi nataka kumwita Mheshimiwa Mnyika ajibu, kama unajibu mjibie.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niongee tu hoja ndogo sana hapo, kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzetu. Kwa ajili ya *spirit* ile ile ambayo tulishajaribu kujenga, naomba nizungumze jambo moja muhimu sana, *Constitution* ni matumaini yangu kwamba Katiba yetu haitaangalia tu masuala ya kisiasa na kiutawala, itaangalia masuala ya *economic well being* ya nchi yetu. Ukiangalia hata haya makundi yote

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. F.A. MBOWE]

yaliyoainishwa hapa, ambayo yameshapewa *allocation* ya Wajumbe, kuna *very little consideration* imefanyika kwa *private sector*. Wakati wote tunakubaliana kwamba kama kweli tunataka kuangalia nchi yetu *economically* na *utilization* na *resources*, hatuwezi tukaipuuza *private sector* katika Taifa letu.

Tutajazana wanasiasa, wanasiasa tutapiga kelele, lakini kama kweli tunataka kuweka *focus* kwenye *economics*, tunataka kuweka *focus* katika masuala ta *integration*, hatuwezi tukafika hatua tukaendelea kupuuza nafasi ya *private sector* katika *Constitution making process*.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana, hiyo idadi iongezwe, ili pamoja na mambo mengine yote, hilo kundi la *private sector* lipewe *consideration*, haya ni mambo muhimu sana sana. Watu walioko kwenye *mining*, kwenye *financial institutions*, watu walioko kwenye masuala ya, hawa ma-*CO Round Table*. Kuna watu wengi sana katika *private sector* ambao hawako *considered* kabisa katika makundi yoyote, ningeomba sana hiyo idadi iongezwa ili tujumuishe kundi hili muhimu mno, kwa faida ya *economy* ya nchi yetu, ahsante sana.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa ili kuweka rekodi sawa. Mheshimiwa Mnyika amerudia maneno ya jana, kwamba hiyo nyaraka aliyoitumia yeye ni nyaraka iliyotolewa na Wenyeviti kwa Rais, sawa nakubali, tuligawiwa wote Mheshimiwa Mbowe alitupa, lakini baada ya pale, nyaraka tuliyoifanyia kazi siyo ile, nyaraka tuliyoifanyia kazi ni hii aliyoitoa Mheshimiwa Mbatia. Ile ilikuwa *consumption* ya *principals*, hawa wakubwa zetu wamepeana wenyewe, lakini baada ya pale, akaagizwa Mheshimiwa Mbatia atengeneze *working document* ya *technical committee*. Kwa hiyo, nataka kuweka rekodi sawa, sababu zilizotajwa ndani ya Bunge lako siyo sababu zile zilizotakiwa kufanyiwa kazi. Sababu zilizotajwa ndani ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

working document tuliyoifanyia kazi na kutengeneza marekebisho haya, ni zile ambazo ziko kwenye waraka wa Mheshimiwa Mbatia na siyo walaka anaousema Mheshimiwa Mnyika, nilitaka kuweka rekodi sawa. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE. B. SIMBACHAWENE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida kama kinachosemwa na Mheshimiwa Mnyika kina akisi *formula* yoyote. Yaani unaweza ukasema, waliposema 166, zilielezwa sababu. Waliposema iongezeke 35, zilielezwa sababu. Hii sababu ya Mnyika anayoficha kwenye sababu ambazo siyo halisi, ni ipi? Kama siyo siasa. (Makofi)

Sisi ni watu wazima, *let us be serious. We have said let us go beyond our political parties*, na Watanzania watuelewe, kwamba kama ukisema suala la uwiano, hao mnaoseme 600, haiwezi kuakisi, idadi ya Watanzania milioni 46. (Makofi)

Haiwezekani, kwa sababu hata mtu yeyote, mimi ninaweza nikasema basi tuwe 10,000 kutoka kwenye hiyo idadi ya Watanzania milioni 46, basi wawe 10,000, halafu na yenyewe hiyo itakuwa hoja hapa itatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa mtu yeyote anaweza akaja na idadi yake kwa sababu zake, na wote tunazo sababu hapa tunaweza tukaja na hoja hizo. Kwa hiyo, mimi ninasema hoja ya Mheshimiwa Mnyika, kwa sababu imepita katika kila *forum* ya iliyojadili Muswada huu na ilikuwa inaanguka, na taarifa zimesemwa. Mjumuishaji Waziri mwenye hoja amesema kila *stage* imepita na ilikuwa inaanguka hiyo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haina mashiko na haina sababu ya kulisumbua Bunge lako kwa sababu, kila *stage* iliyopita imekuwa ikianguka, na hiyo Bunge halifanyi kazi hapa ndani. Bunge lina *process* yake, utungaji wa Sheria *it is a process*, lazima tuiheshimu hiyo *process*. Kama hoja imekuwa ikianguka katika kila *stage*, inakujaje hapa ituchukulie muda, ichukue, waonekana Watanzania kama

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE. B. SIMBACHAWENE)]

vile kuna jambo kubwa wakati mambo makubwa ya maana yamekwisha amuliwa. (*Makofi*)

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru Waheshimiwa hoja inaweza ikapita mahali kwingi, ikakataliwa na wengi, kwa sababu tu wengi wameamua kuikataa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwana falsafa alikuwa anaitwa *Socrates*, alikuwa na hoja kwamba dunia iko kama duara. Watu walikuwa wanaamini dunia iko kama meza. Waliikataa ile hoja na hatimaye wakamlisha sumu, lakini baadaye ikaja kugundulika kwamba kumbe dunia iko kama duara, na inazunguka. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuitazame hoja kama hoja, tusitazame mtoa hoja wala Chama anachotoka Mtoa Hoja. Hoja yenyewe nimeshaielezea, lakini kwa sababu kuna majibu yametolewa kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu ya kwamba. Mosi, kwamba huko nyuma tulizungumza wanasiasa wawakilishwe. Tulizungumzia katika mchakato wa uundaji wa Tume ya Katiba na wazo lilitoka pande zote na hata upande wa CCM na hata upande wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa Wajumbe wa Bugne la Katiba, mkirudi kwenye kumbukumbu za Bunge mwaka 2011, siyo tu tulizungumza kuhusu nyongeza ya idadi, bali tulitaka wachaguliwe moja kwa moja Wajumbe maalum watakaofanya kazi ya kutunga Katiba peke yake, wazo hili lilikataliwa. Wazo ambalo ni mbadala sasa wa wazo hilo, ni kuwa na mchanganyiko kati ya Wabunge na Wajumbe wawakilishi na Makundi mengine katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nambari hii ya mbili ya tatu ni nabari hii ya 292, haikutoka kutoka hewani. Katika *spirit* ya *give and take*, hoja yetu sisi ilikuwa idadi ya Wabunge na Wajumbe wawakilishi ambayo ni 438, tuongeze kutoka nje

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

ya Bunge watu 438. Serikali ikakataa, kwa *spirit* hiyo hiyo ya *give and take*, tukasema basi ipunguzwe walau iwe mbili ya tatu ya Wajumbe wa 438, ndiyo hiyo 292, ndiyo asili ya hiyo 292.

MJUMBE FULANI: Hajui.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Hayo ni mahesabu rahisi sana.

MJUMBE FULANI: Waziri hajui.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ambazo sisi kwa kweli tulikuwa na misimamo sana. Sisi tulikuwa tuna msimamo ya kwamba Mamlaka ya uteuzi isiwe Rais. Sisi tulikuwa na msimamo ya kwamba orodha ya Taasisi zitajwe. Tukakubali kuachia hoja zote hizo ambazo ni hoja muhimu na hoja kubwa tu. Sasa hoja hii ambayo ni ya makundi ya nje yetu sisi ya kijamii huko. Siyo CHADEMA, siyo CCM, siyo nani, kuongeza tu watu 90 kutoka nje, kwa nini inakataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ukiniuliza nitakuambia nimesikia maelezo ya Mheshimiwa Ester Bulaya, akizungumza kwamba, malalamiko ni kuwa CCM wako wengi. Nimesikia melezo ya Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, kwa watu wana *allergyna* CCM. Maelezo haya na mimi sikuzungumza kuhusu CCM hapa. Maelezo haya ya kuzungumza kuhusu CCM, yanajenga sasa imani ya watu ambao wanaamini kwamba siri ya CCM kukataa watu wengine kutoka nje ni kwa sababu Katiba inapitishwa na mbili ya tatu ya wapiga kura. (*Makofi*)

Kwa hiyo, maana yake wakikaa makundi ya Kijamii, changanya wawakilishi wa Asasi. Changanya na hivi vyama vyote vya upinzani vilivyopo, wakikaa kwenye Bunge la Katiba, CCM, ikiamua kupitisha kwa asilimia 66, wakikaa upande wa Bara peke yake CCM, inaweza.

Sasa kama mnaikataa hoja hii kwa sababu hiyo ni vizuri mkasema wazi. Sisi tunataka hoja hii ipite kwa maana tu ya kuwakiisha makundi mbalimbali katika jamii kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

upana wao. Iwe ni wakulima, iwe ni wafanyakazi, iwe ni walemavu, iwe ni wafanyabiashara, iwe ni asasi za kirai. Sisi Wabunge tunawakilisha hayo makundi kuotoka katika maeneo yetu. Hayo makundi yanapaza sauti ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wabunge, kwa niaba ya makundi yote yanayotoka katika maeneo yenu. Wakulima, wafugaji na makundi yote haya ili yawe na uwakilishi mpana, tutaweka pembeni misimamo ya vyama vyetu na tutafanya uamuzi huu wa kuongeza idadi ya wajumbe kwa maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, hatuendelei, huyu ndiye aliyekuwa mwenye hoja. Kwa sasa tutafanya uamuzi.

*(Hoja ya Mheshimiwa Mnyika
iliamuliwa na Kukataliwa)*

MWENYEKITI: Uamuzi ni kwamba tunaendelea na ilivyokuwa kwenye mchango wa Serikali, tunaendelea. Mheshimiwa Mushashu, utakumbuka kwamba, maelezo yako wewe unasema *fifty, fifty*. Mabadiliko tumesema *gender parity*. Kwa hiyo, badala ya kusema *fifty, fifty*, tumesema *gender parity*, tumeishasahihisha.

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. BERNADETA KASABAGO MUSHASHU, MEMBER OF PARLIAMENT WOMEN SPECIAL SEATS THE SECOND READING FOR THE BILL TITLED THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT NO. 2) ACT 2013

(Made under Standing Order 86 (11) and 88 (2))

The Bill titled the Constitutional Review Act, Cap 83 is amended as follows:-

In clause 2

(a) By adding immediately after subsection 2(a) the following new subsection.

2 (b) In appointing the members in section 2 (a) The President shall ensure that fifty percent of each ground are women.

(b) By renumbering subsection 2 (b) as 2 (c) accordingly.

Hon. Bernadeta Kasabago Mushashu

MEMBER OF PARLIAMENT WOMEN SPECIAL SEAT KAGERA

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimeamua kuleta *amendment* katika sehemu hii kwa sababu nimegundua kwamba sehemu hii kifungu cha 2 kina sehemu kuu mbili. Ukiangalia sehemu ya 2(b) inazungumzia *list* zitakazotoka kwenye makundi mbalimbali kwenda kwa yule mteuzi ambaye ni Rais ambayo inasema sasa pale kwamba tutazingatia usawa wa kijinsia ambayo sasa hivi imekuja kuweka *parity*. Hapo tunazungumzia zile *list* zitakazotoka kwa yale makundi kwenda kwa mteuzi. Lakini ukiangalia 2(a) inazungumza sasa kuteua wale wajumbe ambao watatoka kwenye makundi mbalimbali.

Pamoja na mawazo mazuri aliyotueleza hapa Mheshimiwa Waziri, kwamba tusishangae kati ya wale watakaoteuliwa, 201, 101 wakawa wanawake. Tunataka tuione sasa hapa kwenye sheria, ndiyo maana nikaleta ile *amendment* kwa ajili ya uteuzi sasa, kwamba atakayeteua nimeweka *amendment* kwamba tuongeze sehemu ya 2(b) kwamba *in appointing the members in section 2(a) the President shall ensure that 50 per cent of each group are women*, yaani kati ya yale makundi yote. Sawa ile ya kwanza ilikuwa inazungumzia ile *list* itakayoletwa, sasa na huyu anayeteua a-ensure kwamba anachagua 50 per cent. (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. B.K. MUSHASHU]

Nimesema hiyo kwasababu *list* zinaweza zikawasilishwa lakini wale wanawake wasionekane, lakini tunajua kwamba wanawake wenye uwezo wapo. Kwa hiyo tuiweke kwenye sheria hii kusudi iwasaidie wale watakaokuja kuteua waweze kuizingatia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, tunaomba maelezo kutoka kwenu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaendelea kuwasiliana hapa, kwenye uteuzi tumeandika chini ya *section* ya sheria hii tuliyoipitisha mwezi uliopita kifungu cha 4 (2) (b) kuna (b) sasa ndogo ambayo inasema; *in appointing members of the constitute assembly under sub section 1(c) the President shall have regard to qualifications and experience of persons nominated and be gender balance*, ambayo ndiyo tumesema *gender parity*. Hii ni kwenye *appointing* ambayo Rais atakuwa ana-*appoint*. Kwa hiyo nafikiri iko *covered* katika sheria tuliyoipitisha *last time*.

MWENYEKITI: Mseme kwa sauti tusitumie muda *double*.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli hoja ya Mheshimiwa Mushashu ina mantiki katika marekebisho aliyofanya Mheshimiwa Waziri ni katika *list* zile zitakazowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais, zile taasisi zizingatie usawa wa kijinsia.

Ukiangalia katika kifungu namba 4 tulichopitisha katika Bunge la Mwezi Septemba, 2013 ilikuwa pia inazungumzia Rais anapoteua azingatie usawa wa Kijinsia. Kwa hiyo, katika lugha ya Kiingereza bado ilikuwa inasomeka *gender balance*, tunaomba waandishi walizingatie hilo ili kote kuwili, katika uteuzi lakini pia katika orodha zitakazowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais zizingatie usawa wa kijinsia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Sasa mnaeleza tu, tunatunga sheria, wapi mnabadili nini, siyo maelezo tu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenye Muswada, baada ya ibara ya 2(a), baada ya (x) tuweke masharti kwamba makundi na hapa ndiyo ingawa hajafika nawahisha hoja pendekezo ambalo ametoa Mheshimiwa Mnyika, kwamba wakati makundi haya au taasisi hizi zinapofanya uteuzi zizingatie, na narudia, zizingatie usawa wa jinsia. Kwa Kiingereza, hili ni neno langu nililisema juzi, sizungumzii *gender balance*, nazungumzia *gender parity*. Kwa hiyo, ni baada ya (x) tutakupa maneno (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, kuna nani mwingine, Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru na mimi nafikiri hoja ambayo wameijenga wenzangu na mimi nilikuwa najaribu kuijenga hoja hiyo hiyo kuhusu uwakilishi halisi wa wanawake. Kwa sababu hoja yangu nafikiri imekuwa *reflected* na hoja ya mama Mng'ong'o na hoja ya mama Mushashu.

Kwanza kabisa nishukuru, lakini nilikuwa naomba tu kutoa angalizo wakati wa uteuzi kwamba tuangalie na wanawake ambao wako vijijini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabati sasa angalizo wakati wa uteuzi ni wakati gani, sisi tunatunga sheria, hapo siyo sisi, hebu sema *amendment* yako, naona inafanana sana na ya Mushashu.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana nimesema kwamba imekuwa *reflected* kwenye hoja hizo mbili.

MWENYEKITI: Haya, basi ahsante sana.

MHE. RITTA E. KABATI: Ahsante sana.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitshwa na Kamati ya Bunge zima Pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 3

MWENYEKITI: Ibara ya 3 inaafikiwa? Mheshimiwa Chengé ndiyo, wataalamu muangalie ule mstari una matatizo.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Nilivyomwelewa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati anafanya majumuisho ilikuwa ni kwamba katika kifungu cha 3 kifungu kidogo cha 2, ili kuwezesha Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi kuanza maandalizi kabla ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuteua au kutangaza rasmi ujio wa Bunge Maalum la Katiba.

Kwamba ni vyema tukafanya marekebisho katika hicho kifungu kidogo cha pili ili tuyaondoe yale maneno *subject to the provisions of sub section (1) and without prejudice to the provisions of this section*. Alitumia maneno ambayo nayakumbuka, ya Kiingereza, kwa kusema *notwithstanding the provisions of this section*. Kama ni sahihi naiomba tu Serikali sasa iyaseme hayo ili sasa mtiririko wa hiyo shabaha iliyokusudiwa ipatikane. Ahsante Mwenyekiti. Mheshimiwa Jenista alisema hivyo hivyo. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na kwa hiyo kifugu hiki tunakibadili na tunasema kwamba *notwithstanding the provisions of sub section (1) notwithstanding the provision of sub section (1) the Clerk of The National Assembly and The Clerk of the House of Representatives shall, before the proclamation of the Constituent Assembly make necessary preparations for better carrying out of the Constituent Assembly business.*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Tunafuta nini hapo.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Tunafuta, *subject to the provision of subsection one and without prejudice to, tunaweka neno notwithstanding* badala ya hayo yote.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitshwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 4

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitshwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 5

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MATHIAS CHIKAWA, THE MINISTER FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND READING OF A BILL TITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT NO. 2) ACT, 2013"

Made Under Section 86(10)(b)

B: In clause 5 by deleting paragraph (a) and substituting for it the following:

(a) deleting the heading and substituting for it with the following new heading:

"GENERAL PROVISIONS"

Dodoma
8th November, 2013

MC
MCLA

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA
MHE. MATHIAS CHIKAWA, WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA
WAKATI WA KUSOMWA KWA MARA YA PILI MUSWADA
UITWAO "SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA
(MAREKEBISHO NA. 2)
YA MWAKA 2013

Imetengenezwa chini ya Kanuni ya 86(10)(b)

B:Katika Ibara ya 5 kwa kufuta aya (a) na kuibadilisha
kama ifuatavyo:

(a)kufuta kichwa cha habari na kukiandika upya
kama ifuatavyo:

"MASHARTI YA JUMLA"

Dodoma
8 Novemba, 2013

MC
WKS

SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON JOHN
JOHN MNYIKA MEMBER OF PARLIAMENT FOR UBUNGO
CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL
ENTITLED THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT
NO. 2) ACT, 2013

Made Under Standing Order 86(11) and 88(2)

A bill entitled "THE CONSTITUTIONAL REVIEW
(AMENDMENT NO. 2) 2013" is amended as follows:

D: In clause 5 in sub section "c" by deleting the renumbered
section 37 and substitute with the new section as;

“31; - (1) Upon declaration of the results of the referendum by the National Electoral Commission, the President shall, by order published in the Gazette, dissolve the commission.

.....
JOHN JOHN MNYIKA (MP)
UBUNGO CONSTITUENCY
8.11.2013

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kupendekeza marekebisho kwenye kifungu cha 5 cha sheria hii.

Naelewa kwamba mapendekezo ya Serikali yalikuwa ni kwa ajili ya kubadi nambari kama zilivyo baada ya marekebisho yaliyofanyika pamoja na ku-*repeal* vifungu ambavyo vitakwenda kuingizwa kwenye kura ya maoni vinavyohusu masuala ya kura ya maoni. Kwa sababu mapendekezo haya ya Serikali yamegusa kifungu cha 37 ambacho ni kifungu kinachohusika na masuala ya Tume, ambacho ni kifungu katika marekebisho yaliyopita kilifanyiwa marekebisho ya kuifuta Tume ya Katiba na kuhitimisha ukomo wa tume ya Katiba mapandekazo ninayopendekeza ni ya kurejesha kifungu kilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kilivyo kuwa awali kinasomeka hivi, 37(1), *upon declaration of the result of the referendum by the National Electoral Commission, The President shall by order publish in the Gazette dissolve the Commission.* Kwa maneno mengine, Serikali ilipoitunga hii sheria mwaka 2011 iliamua kwamba Tume ya Mabadiliko ya Katiba itavunjwa baada ya matokeo ya Kura ya Maoni kutangazwa. Huu ndio ulikuwa uamuzi wa Serikali ulipotunga sheria November 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi huu unaelekea bado kuungwa mkonoo na Serikali, kwa maana ya mtizamo wa Serikali. Kwa sababu Mheshimiwa Rais katika hotuba

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

yake kwa Taifa tarehe 4 Oktoba, 2013, hotuba kwa taifa, tarehe 4 Oktoba, 2013 alisema yafuatayo juu ya mambo yanayohusiana na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

‘Katika orodha ya madai ya ndugu zetu wa upinzani lipo suala la uhai wa Tume ya Katiba. Wanataka usiishie wanapokabidhi rasimu ya pili kwa Bunge Maalum bali waenendee mpaka mwisho wa mchakato.

Nimeuliza ilikuwaje, nimeelezwa kuwa jambo hili halitokani na mapandeko ya Serikali, wala ya Kamati ya bunge ya Katiba ya Sheria na Utawala, limetokana na mapandeko ya Mbunge katika Bunge wakati wa kupitia vifungu na kuungwa mkono na Wabunge wengi, kwa hiyo, kuilaumu Serikali si haki, Serikali inaweza kuwa mshirika katika hoja hii. Nami naiona hoja ya wajumbe wa Tume kuwa na wajibu wakati wa Bunge Maalum hasa wa kusaidia kufafanua mapandeko ya Tume.

Je Ushiriki wao uwe upi? Uwe vipi? Je ni wajumbe wote, au baadhi ya wajumbe; jambo hili linaweza kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimewasilisha jedwali hili la marekebisho kwenye jambo hili ili jambo hili liweze kujadiliwa tuweze kutimiza hii dhamira ambayo Mheshimiwa Rais alizungumza kwenye hotuba yake kwa taifa tarehe 4 Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini, naamini, kwa sababu Mheshimiwa Rais alisema kwa Taifa, tarehe 4 Oktoba, 2013, kwamba Serikali ni Mshirika wa hoja hii naamini Serikali itakuwa mshirika katika hoja hii kwa kukubali kuunga mkono marekebisho ili kurejesha kazi ya Tume kuendelea na ukomo wa Tume uwe baada ya kutolewa matoleo kwenye *referendum* kama ambavyo mapandeko yametolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja mbili jana na leo kupinga hoja hii. Hoja ya kwanza ni kwamba kuna *principles of bias*, kwamba, kwa kuwa wao wameiandaa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

ripoti basi watafanya kazi ya kuitetea ripoti. Kwa kuwa wao wameandaa rasimu, watafanya kazi ya kuitetea rasimu. Hiyo ni hoja ya kwanza inayotolewa kuipinga hoja hii.

Hoja ya pili inayotolewa ni kwamba kifungu cha 9 cha sheria kama ilivyo sasa, kinasema majukumu ya Tume, na katika kifungu hicho hakujatajwa majukumu ya Tume yanayohusiana na kazi za mbele isipokuwa kazi ya ukusanyaji maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hizi si hoja sahihi kama ambavyo iwapo hoja hizi zitaendelea kutumika katika kuhalalisha kuikomesha Tume uhai wake. Nitatoa ufafanuzi kwenye majumuisho, au wajumbe wenzangu watakaochangia wataeleza ni kwa vipi hizi hoja za *bias* na hoja majukumu ya kifungu cha 9 hazipaswi kuwa msingi wa kukiuka hii azma nzuri ya Mheshimiwa Rais ya kutaka Tume iendelee na wajibu. Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianzie kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Mnyika kwa jitihada. Lakini pia naomba nisisitize kwamba, kimsingi, lazima turudi katika *spirit*, si tu ya kutaka lazima kila hoja ipite, kwa sababu tungeenda hivyo, hata sisi wana CCM labda tunganese basi Muswada usiletwe kabisa. Lakini tuko pamoja kwa ajili ya kuona tunachokifanya ni sahihi kwa mustakabali wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu wangu Tume huwa inapewa kazi maalum; na hapa katika sheria mama ukurasa wa 11 kifungu cha 9 kinatamka wazi majukumu ya Tume. Kufikia Tume kukabidhi taarifa yake ya Rasimu ya Mwisho kwenye Bunge itakuwa imemaliza majukumu yake. Kwa misingi hiyo, kubaki na hiki kitu kinachoitwa Tume itakuwa hakina mantiki na ikizingatiwa kwamba hata katika sheria inayofuata kazi ya kutoa elimu haiko tena katika Tume badala yake inahamia katika sheria zile zinazohusiana

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. S.M. MANYANYA]

na tume za uchaguzi. Kwa hiyo, kutunza hii ni kama vile labda mtu unaamua tu kuwa na kitu ambacho kiko pale lakini hakina mantiki.

Kwa kutambua kwamba tunapofanya shughuli hii ya kutengeneza Katiba yetu Mpya tutahitaji utaalim ndiyo maana tumeweka *provision* ya kuweza kumpata mwenyekiti au katibu, au mjumbe yeyote, au mtaalam yeyote ambaye ataweza kutusaidia wakati tunatunga Tume. Kwa maana hiyo, kama watu hawajawekwa pembeni, ila kama Tume ndiyo tunasema hatuwezi kuendelea kuwa na Tume kwa sababu kuwa na Tume ina masharti yake ya kuitunza Tume na kuilea Tume. Kwa hiyo, mimi nadhani hili suala halina *logic*, halina *logic* kabisa na wakati huo wa kuwaita wataalam siyo lazima wawe kutoka kwenye Tume tu, nchi hii ina wasomi wengi na tunahitaji kila ngazi tupate jitihada zinazotoka katika maeneo mbalimbali.

Ukifuatilia hapa, mimi kwanza najaribu kuona , kama mtakumbuka wakati tunatunga hii sheria mwanzo kabisa tulikataa *interference* ya kila *stage* na ndiyo maana hata wenzetu Tume wakati wanakusanya maoni hata wakuu wa Mikoa, wakuu wa Wilaya, Vyombo, tulisema msiingilie, acheni Tume ifanye kazi yake vizuri. Tunashukuru nakuipongeza itakuwa imefanya.

Baada ya hapo Bunge tunataka liwe huru, lifanye kazi yake vizuri, hawa wamemaliza siyo ifikie sasa kuja hapa mtu anaona labda pengine kile alichokiletea amekuwa *offended* anahangaika kutokukitetea, hapana, tutamhitaji nje kama ambavyo tunatumia watendaji wetu makatibu wakuu na viongozi wengine ambao wanatupa ushauri wakati wa kutunga sheria. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana tena kwa kunipatia nafasi hii, nimshukuru sana Mheshimiwa injinia Eng. Manyanya kwa maelezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti tunatunga Sheria, sheria mama ipo, na mtiririko wa Sheria hii kila sehemu ya Sheria hii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A.J. CHENGE]

ina maana yake. Unanza na Tume yenyewe, *establishment of the Commission* ina sehemu zake na majukumu yametajwa, unamaliza hiyo unakuja kwenye eneo la *convening*, kuitishwa kwa Bunge Maalum la Katiba, unakuja kwenye sehemu ya 5 *validation* yaani kuhalalisha utaratibu mzima, yaani kupitia sasa umetoka kwenye Bunge maalum kwenda kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kuliona hili. Kulikuwa na mkanganyiko katika kufungu cha 33 kifungu kidogo cha 2 ambapo neno *Commission*, neno *Commission* kwenye sheria mama limepewa tafsiri katika ukurasa wa 6 na inasema, '*Commission means the Commission established for the purposes of coordination and collection of public opinions and on constitutional review.* Tume ya uchaguzi haikupewa tafsiri ila kila mahali ambako imepewa jukumu hilo inatajwa katika urefu wake katika sheria mama.

Katika kifungu cha 33 kifungu kidogo cha 2, ambapo inasema, '*for the purposes of sensitization of and public awareness on the referendum for the proposed Constitution the Commission* sasa hapa ndiyo ilikuwa mkanganyiko.

The Commission, ilikuwa Tume yenyewe, *shall*. Lakini hapa tulipaswa tuseme, Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri na ile ya Zanzibar, kama inavyoendelea kusema, tukisha sahihisha haya kama Serikali ilivyofanya hakuna mkanganyiko, tumeishamaliza imeshawasilisha ripoti yake, wataitwa Mwenyekiti na Wajumbe kama watahitajika kwa shughuli hiyo. Lakini nnashukuru sana Serikali kwa kuliona hilo. (*Makofi*)

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba nchi hii kama wanavyosema Wabunge wenzangu kuna watalaam wengi. Lakini Tume hii ya Katiba, ndiyo waliokwenda *field*, wakakusanya maoni ya Watanzania, wana ile *experience* na ile *test* ya kule kwenye *field*. Sasa hata Rais wa hii nchi, hili suala aliona, na akajaribu kushauri kwamba kama Tume. Kwa sababu Tume kuja humu, siyo kwamba wanakuja kupiga kura,

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[MHE. E.D. WENJE]

tutakapokuwa tunapitisha vifungu. Ila watakuwa kama *Consultancy*, katika yale maeneo ambayo ni *contentious* watakuja kutoa ushauri. Sasa kuruhusu Tume kuja hapa kama alivyosema Mheshimiwa David Kafulila, kwani Bunge litakuwa limefungukiwa na nini, watachukua nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba.

MWENYEKITI: Unamanisha Mheshimiwa John Mnyika, siyo Mheshimiwa David Kafulila.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema Mheshimiwa David Kafulila wakati anachangia hapa alisema.

MWENYEKITI: Aaha. *Okay.*

MHE. EZEKIA D. WENJE: Ninajaribu tu kutoa reference. Alitushauri kwamba tunaogopa nini. Tume kwa mfano wakija humu ndani katika yale mambo ambayo ni *contentious* wakati ushauri na *experience* waliokuwa nao kwenye *field* na kwa nini kwa mfano hili limependekewa. Kwa sababu wao ndiyo wanayo *actually experience* kwenye *field*. Ni kweli kwamba kuna Wasomi wengi lakini hawakwenda huko kwenye *field*. Kwani wakiingia humu tatatupotezea nini?

Ni kwamba kama *issue* ni gharama wanavyosema wengine, Mheshimiwa Manyanya anasema kuwa-*maintain*. Tunaelewa kwamba *Constitution Making Processes* lazima iwe na gharama na tumeshauri kila siku bora tutumie gharama kubwa leo. Kuliko kuja kutumia gharama nyingi huko baadaye kuwa na Katiba mbovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa John Mnyika tuiangalie kwa mamkini. (*Makofi*)

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S.S. JAFO]

Kwanza ninaomba niwe *clear* kabisa. Kuna watu humu, wanazungumza jambo ili mradi nje wapate kusifiwa. Kama kiongozi sahihi, unatakiwa usimame katika hoja sahihi. (Makofi)

MWENYEKITI: Mawazo yake.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono. Kwa sababu ndiye niliyetoa hoja toka mwanzo ya kusema kwamba hii Tume iishe muda wake kwa sababu ikishakamilisha kazi yake hatutaki *Consultant* aje katika Bunge hili la Katiba. Kuna *segregation of duties*. Hata Wahasibu wanajua, akisha saini cheki kuna sehemu nyingine watu wanakwenda wana-*approve* na kila kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Tume ikisha kamilisha kazi yake, ina maana Bunge la Katiba linatakiwa liwe na uhuru wa kutosha kutoa mawazo yake. Haiwezikani mtu amekusanya maoni halafu aje ku-*influence* kwamba sisi hatukutaka hiki haiwezikani litakuwa siyo Bunge la Katiba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini, hawa Wazee wetu, kwa kweli wana nafasi kubwa baada ya hiyo kuendelea kutoa mchango wao katika fani mbalimbali. Lakini kwa mujibu wa sheria, kwamba hii Tume kama tulivyokubaliana mwanzo. Mheshimiwa Rais, siyo kwamba ana maana ya kushauri kwamba, alikuwa anasema hivi, mjadala wenye ni huu tuna sema kwamba Tume, kama tulivyokubaliana kwamba Tume muda wake umefika na kazi yake imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A.M. ABDALLAH]

Kwanza ninaomba hivi, hili suala la Hotuba ya Rais, alisema, alisema. Mimi ninafurahi kwamba watu kumbe wanajua kwamba alisema kitu cha maana. Lakini wakati mwingine akisema jambo hao hao watu wanapinga. Wanampinga kweli kweli. Ila linapowafaa wao, ndipo linaonekana zuri. *(Makofi)*

Mimi nataka niseme hivi, hili tumuondoe kabisa, yeye alisema jambo hili linazungumzika, ndiyo hivi tunazungumza sasa. Kwa hiyo, hajasema kwamba lazima lirudi Bunge. Haya aliyo tuomba tuyarudishe Bungeni yalikwisha rudi na siyo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri hivi, hebu tuache Tume imemaliza kazi yake ya kukusanya maoni. Sisi tuzungumze. Hilo Bunge la Katiba lizungumze na kama Bunge litataka ufafanuzi, litafute lenyewe, siyo wao wakae mle ndani. Hicho ndicho mimi ninafiiki, tunachozungumza ni nini. Lakini ninasema tumuondoe kabisa Rais katika hili. Hajatulazimisha, yeye alitoa maoni yake na alisema tu kwamba linazungumzika, ndiyo tunazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninashauri, kwa mantiki tunavyoendelea hapa, mimi ninaona watu wote tunakubaliana kabisa waache Tume wamalize kazi yake kwa muda ule uliowekwa kisheria. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kunako mwezi Juni, wakati tunapitisha Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, kulikuwa kuna mgogoro mkubwa sana juu ya uwepo wa Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nilitoa hoja kwamba, kwa nini tunatenga mabilioni. Shilingi bilioni 4.6, kwa ajili ya Tume wakati ikishawasilisha taarifa yake inakuwa *funguts-official*, nilitumia maneno hayo. Upande wa pili huu walizomea walipiga makofi wakasema Tume ni muhimu. Leo wanasema Tume ife. Kitu gani kilichobadilisha msimamo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. T.A.M. LISSU]

ni Rasimu ya Katiba. Rasimu ya Katiba, imetoka kwa namna ambayo hawakutegemea. Sasa Tume inauwawa kwa sababu imefanya kazi ambayo hawakuitazamia, ni hicho tu.

Wanam-*disown* Waziri Mkuu, Jaji Warioba, kwa sababu ameleta rasimu ambayo hawakuitaka ya Serikali tatu. Mheshimiwa Salim Ahmed Salim, mnam-*disown* leo kwa sababu amefanya kazi ambayo CCM hawakuitaka ndiyo hicho tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Rais, amesema, sisi tumependekeza Tume iwe sehemu ya Sekretarieti ya Bunge Maalum la Katiba, Mheshimiwa Rais akasema hapana, mkafanya utaratibu Wajumbe wa Tume wawe sehemu ya Bunge la Katiba. CCM imem-*disown* hata Rais wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnam-*disown* hata Mwenyekiti wenu, kwa sababu tu, Tume ya Jaji Wairoba imependekeza kile ambacho si maslahi ya CCM. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ngoja tuwe *records* sahihi. Ninaomba tuweke record sahihi. Waheshimiwa Wabunge ninaomba niweke *record* sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, suala ambalo Mheshimiwa Tundu Lissu, alikuwa analizungumza wakati wa Bajeti na nimefurahi amelisema. Alikuwa anasema tupunguze gharama za Tume. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa wakati ule.

Ndivyo ilivyokuwa. Siyo haya mnayozungumza. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaka kutoa siri hii. Sasa ninaitoa. (*Kicheko/Makofi*)

WABUNGE FULANI: Toa.

Hii ni Nakala ya Mtaandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA URATIBU NA BUNGE): Tulipokuwa tunazungumzia na tunafanya harakati hizi za maridhiano. Kuanzia hatua ya kwanza, ya pili na ya tatu. Tulikubaliana twende kwa hatua. Mara ya kwanza tulishughulikia Tume. Mara ya pili tukaja kuzungumzia masuala ya Bunge la Katiba.

Mara ya pili, tulipokutana kwa Rais tulikubaliana sasa vyama vilete mapendekezo yao kwangu. Halafu mimi nikutane kwenye *technical committee* tujadili mawazo ya vyama na tulifanya. Mimi nikiwa Mwenyekiti na wakati huo tulikutana na Chama kimoja kimoja.

Mheshimiwa John Mnyika alikuwepo, na Julius Itatiro kwa upande wa *CUF*. Ninataka kusema hapa ambalo sikutaka kulisema. Waliopendekeza Tume hii iondoke mara mbili kwa maandishi niliyo nayo kwa *signature* ya Naibu Katibu Mkuu wa *CUF*. Ni *CUF*. Chama cha *CUF*, ni miongoni mwa washirika muhimu katika harakati hizi. Katika maoni yao mara mbili walitoa mapendekezo kwamba Tume hii ikimaliza kazi yake iondoke na inaongeza gharama. Sisi kama mnavyotujua viongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi tulivyo wasikivu, tulifikiri maoni yao ni mazuri. (*Makofi*)

Hii sikutaka kuitoa hii siri, maana mnarukia tu kwa Rais. Lakini tuliokuwa pamoja, juu ya yaliyotokea. Viongozi wa *CUF*, kama sehemu ya mapendekezo na kama washirika wakuu, ndiyo waliopendekeza.

Tulivyofika, ninazo *document*. Ushahdi ninao, kama anakataa aseme. Hata kwa Mheshimiwa Rais pale mlivyokuwepo, Mheshimiwa Mnyikka na Tundu Lissu, niliisoma. Niliisoma ndiyo.

Mheshimwia Mwenyekiti, nilitaka kusema kwamba ingawa hapa anatajwa Rais, sawa kwenye hotuba. Lakini walioanza kupendekeza kwamba jambo hii liondoke, ni washirika wakuu katika harakati hizi ambao tulipewa kazi ya kufanya. Lakini ndani ya Bunge sasa likaja likaungwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)]

mkono na Wabunge wote, baada ya hoja ya Mheshimiwa Selemani Jafo kutokeza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, hili ni la Wabunge wote, na limepitia *process* zote. Wala hakuna sababu ya kwamba eti kwa sababu Mheshimiwa Warioba ametoa ripoti gani. Lilianza hata kabla ya Mheshimiwa Jaji Warioba hajatoa hata ile Rasimu ya Kwanza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nadhani tufike mwisho.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kufuatilia, mjadala wa hoja muhimu kabisa mbele yetu. Nilikuwa ninamsikiliza vizuri sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mstaafu, Mheshimiwa Andrew J. Chenge.

Ili kudhibitisha kwamba nimeelewa alichosema nimemsogelea pale dakika kama moja iliyopita, kwenda kuhakikisha kwamba nilimwelewa alichosema, na akanikubalia kwamba hivyo ndivyo alivyokuwa amesema na ndivyo anavyoamaanisha.

Kwamba Sheria Mama, ambayo ndiyo tunapendekeza *Amendment* yake hapa. *Amendment Number Two*. Yenyewe imeisha-*provide* maelekezo yanayoonyesha kwamba Tume tunayoizungumzia, inakuwa haina kazi tena baada ya kukamilisha kazi ambayo imeisha *submit*. Sheria iliyopo. (*Makofi*)

Sheria mama iliyopo, tayari ina vipengele vinavyoonyesha kwamba Tume hiyo itakuwa imefikia ukomo baada ya kukamilisha kazi ambayo imeisha kabidhi. Sasa kama hivyo ndivyo. Ukweli ni kwamba hata hii sehemu ya Tano (5) tunayo ijadili sasa hivi inaweza hata ikaondoka kwenye mapendekezo kwa sababu haina umuhimu. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Kwa sababu Sheria ile Sheria mama imeshaeleza tayari Tume inafika ukomo. Hata ku-*propose* tena *Amendment* kwamba Tume ifike ukomo ni kama vile tunarudia sasa kufanya marekebisho ambayo yameishakuwa *provided for* kwenye sheria mama. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nimelizungumza wakati ninafanya *Winding-up*, na nikaeleza msingi wake. Nikaeleza haya ni makubaliano yaliyokwishafanywa na Ndugu yangu Mnyika aliyeleta hoja hii, anafahamu kabisa, kwamba jambo hili lilikwisha isha.

Lakini bado amelileta na ataendelea kulileta nafikiri hata huko nje ya Bunge, lakini na majibu ni yale yale tu. Tume ina kipindi chake cha kufanya kazi. Tume imekwisha kufanya kazi yake, inakwisha. Hatumchukii mtu, wala hatuzungukmzii Tume kama Watu fulani, ila tu tunaweza kujuliza haya. Bunge halikuwahitaji mmewaweka wa nini. Maana si lazima tukawahitaji hata kidogo. Tunaweza Bunge tukakaa, tukaendelea na shughuli zetu, hatuwahitaji hata siku moja ushauri wao, lakini bado tumewaweka wa niini?

Sheria sasa ilivyo ina-*provide* kwamba tunaweza kuwaita. Mimi ninafikiri ni *fare*. Bunge liendelee, likiwahitaji litawaita na hivyo ndivyo sheria inavyosema. Lakini tuwaweke tu wawepo, ili iweje. Tume hii imefanya kazi imemaliza, tunaishukuru sana. Tutaishukuru sana tena vizuri sana. Kazi waliyofanya ni nzuri. Mapendekezo yake ni mazuri, si ndiyo mapendekezo ya wananchi?

Sasa tuache na Bunge nalo lifanye kazi. Nilisema pale watu 32 wamezunguuka nchi nzima kukusanya maoni. Watu 15,000 wamechangia maoni hayo mapendekezo yao. Watu watu 600 na kitu sisi tutakwenda kutoa mengine ya kwetu. Lakini maamuzi bado huu ni mchakato tu. Maamuzi ni kule mwisho. Tume imemaliza kazi yake tuiache ipumzike.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninafikiri sheria ibakie kama ilivyo kwa sababu inatoa uwezekano wa kuwaita Wajumbe wa Tume kuja kushiriki katika Bunge hili watakapohitajika. *(Makofi)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, nimalizie kwa nukta ambayo Mheshimiwa ameizungumzia ya kwamba Sheria kwa sasa inatoa fursa ya kuwaita.

Mheshimiwa Spika, Sheria kwa sasa Kifungu Cha 3, kama ilivyo sainiwa na Rais, inasema; *“The Clerk of the Constitution Assembly, may appoint consultation with the Chairman of Constitution Assembly, invite the Chairman, Vice Chairman, of ordinary Member of the dissolved Commission to give clarification which may be during the debate of the Constitution Assembly.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hiki Kifungu kitazua utata sana katika utekelezaji. Tume umeishavunja, halafu unamwita Mwenyekiti wa Tume. Makamu Mwenyekiti wa Tume, na anakuja kama Mwenyekiti wa Tume na Makamu Mwenyekiti, wa Tume, wala maneno hayatumiki aliyekuwa, na anapokuja mtu ambaye tena si tena Mwenyekiti wa Tume, wala siyo Mjumbe wa Tume kuja kutoa ufafanuzi, anatoa ufafanuzi kama nani? Kwa hiyo, katika mazingira kama haya tunatengeneza sheria ambayo ita *creat confusion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuna maamuzi tunafanya. Lakini tuna maamuzi ambayo tunayarekebisha kwa maslahi ya Taifa. Nisema kwamba, ninakubaliana na Waziri wa Katiba na Sheria, kwamba hili jambo tulilijadili sana. Lakini hili jambo tulilijadili, tukakubaliana kutokubalina. Kwa hiyo, kama tumekubaliana kutokubaliana, na tulipiga mpaka kura. Kura zikawa tatu kwa tatu, katika kura maana yake ni kwamba hili jambo linajadilika na ndiyo maana ninaomba Wabunge wenzangu tulitafakari tulijadli. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

Ukweli ni kwamba na hapa ninaomba nitofautiane kabisa na Mheshimiwa Andrew J. Chenge. Sheria hii ilipotungwa, ilitoa majukumu ya Tume katika Kifungu cha 9. Lakini ikaendelea kutoa majukumu mengine ya Tume kwenye Vifungu mbali mbali vya Kisheria. Ndiyo maana Sheria ilipotungwa, Kifungu Cha 37 cha Sheria hii, mbele huko, kina tamka yafuatayo.

Sheria ilipotungwa pale awali kabla ya kurekebishwa kwenye mkutano uliopita wa Bunge. *“Upon declaration of the result of the referendum by the National Electoral Commission. The Present shall by the order published in the Gazette dissolve the Commission.”*

Sasa kama hii, *Commission*, kazi yake ilikuwa inaishia, inapo-*submit report* yake, ni kwa nini *spirit* ya Sheria ilikuwa Tume inavunjwa baada ya matokeo ya Kura ya Maoni kutangazwa?

Kwa hiyo, hili jambo liko wazi. Lakini Kifungu ulichokitumia Mheshimiwa Andrew J. Chenge, na hapa tunafanya uamuzi mzito sana sasa hivi. Hiki Kifungu cha 5, kinakwenda ku-*repeal* vifungu vya 31 mpaka 36, sina tatizo sana na *repeal* inayofanyika.

Lakini *implication* yake ni nini hii *repeal* tunayoifanya sasa hivi. Vifungu vyote hivi tukishapitisha hapa kwamba vimefutwa, tunakwenda kuvijadili wakati sheria ya kura ya maoni. Sisi wengine tuna msimamo tofauti kuhusu sheria ya Kura ya Maoni, hilo tutalijadili litakapokuja.

Tuna mtizamo kwamba, Tume hii ya sasa ya Uchaguzi, siyo huru na haki kwenye kusimamia kura ya Maoni na kama siyo huru na haki, kwenye kusimamia kura ya maoni haiwezi kuwa huru na haki kwenye kutoa elimu ya Katiba ya Kura ya Maoni. Katika mazingira kama hayo tunarudi kwenye *spirit* ya sheria ilivyokuwa zamani. (*Makofi*)

Sheria ilivyokuwa zamani, na hapa tusipotoshe tafsiri ya hii sheria. Sheria ivyokuwa zamani Kifungu cha 33(2),

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

inatamka bayana na ninanukuu sheria ilivyokuwa: *“For the purpose of exercization and public awareness on the referendum for the proposed Constitution, the Commission shall, and Political and Civil Society, may provide Civic Education and advocacy on the propose Constitution to be conduct, what ever, maelezo yanaendelea.”* Lakini kifungu kilikuwa kinasema nini. Tume ndiyo iliyokuwa inatoa elimu ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazungumza na Serikali. Nimeiliza sana Serikali, Tume hii, iliyokuwa imeandikwa hapa ni Tume gani? Serikali ilisema kwamba Tume hii, ilikuwa ni Tume ya Katiba, ila ilifikiriwa kimakosa wakati huo, kutoa Elimu ya Katiba, sasa Serikali inataka kurudisha jukumu la kutoa Elimu ya Katiba kwa Tume ya Uchaguzi, na ndiyo sababuya *repeal* inayofanyika hivi sasa.

Kwa hiyo kusema kwamba hapa ni tatizo la tafsiri ya neno *Commission* ni *beyond* tafsiri ya neno *Commission*. Hapa kuna kuna *shift of purpose* kutoka kwenye Tume ya Katiba kwenda kwenye Tume ya Uchaguzi jambo ambalo Bunge lilitafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hoja hii, iamuliwe. Tuirejeshe Tume, kwa lengo zuri. Tume iwepo kwenye Bunge la Katiba, wao wamekusanya maoni ya wananchi, hatuwatarajii watoe misimamo yao, ndiyo maana tunataka wawe *Ex-Officio*, tunaratajia tukiwauliza haya maoni ya wananchi mliyoyakusanya tupeni ufafanuzi tupate watu wa kutupa ufafanuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Nchi hii, imeandika Katiba, mwaka 1977 tulipoandika Katiba, hoja kwenye Bunge la Katiba ilitolewa na Serikali. Serikali ilitoa ufafanuzi, Serikali ilihitimisha hoja upande wa Serikali.

Sasa tunaandika Katiba mpya, tuwe na timu hiyo iliyokusanya maoni iwasilishe ripoti Wabunge tujadili kwa uhuru wetu, tukihitaji ufafanuzi kutoka kwao tupate ufafanuzi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kutoka kwa wahusika waliohusika kukusanya maoni kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, sasa tunafanya uamuzi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ya Mheshimiwa Mnyika iliamuliwa na Kukataliwa)

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Bado kidogo. Wakati tunajadili mapendekezo aliyoleta Mheshimiwa Benardetha Mushashu, tulisema tutaingiza maneno baada ya kifungu cha 2(b), Mwanasheria unakumbuka?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho tuliyofanya katika Bunge lililopita kwenye kifungu hicho, tulimpa Mheshimiwa Rais, mamlaka na tukasema kwenye kifungu kile cha 2(b) cha Sheria tuliyobadilisha, kinasema '*In appointing members of the Constituency Assembly under sub section 1(c) the President shall have regard to:*

- (a) Qualifications and experience of persons nominated;*
- and*
- (b) Gender balance.*

Sasa nilivyomwelewa Mheshimiwa Benardetha Mushashu anachotaka kufanya ni kubadilisha ile (b) ambayo haiko kwenye Muswada lakini iko kwenye Muswada kwa upande ule wa makundi yale yanapoleta majina kwa Mheshimiwa Rais, kifungu kilivyo sasa kinajitosheleza kwamba wazingatie hiyo *gender parity*.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba tubadilishe, tutaleta maneno kile kifungu cha 2 (b) yale maneno

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI]

yanayosema *gender balance* na yenyewe yawe ni *gender parity* ili kusudi hata Rais anapokuwa anateua naye azingatie hiyo *gender parity*. Ndiyo hayo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nafikiria kwamba maneno halisi tutakayoweka tuna- *delete the word 'balance' appearing in sub section 2 (b) and substituting for it the word 'parity'*.

*(Hoja iliitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013 [The Constitutional Review (Amendment No. 2) Bill, 2013]

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 89 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 2 wa Mwaka 2013 [*The Constitutional Review (Amendment No. 2) Act, 2013*] Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Na. 2 wa Mwaka 2013 [*The Constitutional Review (Amendment No. 2) Act, 2013*] kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)
(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa
kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoona mmefanya kazi na mimi ninachopenda ni hiki kwamba, mnajadiliana na mnabishana kwa urefu na uzuri. Ninategemea tufanye hivyo siku zijazo na siyo vinginevyo. Tukiondoka hapa basi kila mmoja amejieleza vizuri na nadhani kikubwa ni kule kusikiliza mwingine anasema nini na kupima yale maneno.

Nadhani tukijenga *spirit* ya namna hii tutakwenda vizuri. Kwa hiyo, niwashukuru wote hivyo vyama vilivyohusika, Wabunge waliohusika, Kamati zilizokeshwa, wote mlikesha usiku kucha. Tuwafanye Watanzania waelewe kwamba, tunaenda pamoja, lengo letu ni kufika kule tunakostahili kufika kwa amani, utulivu na upendo unaostahili. Nawashukuru sana na ninawapongeza wote mliofanya kazi kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

TAARIFA YA SPIKA

Kuundwa kwa Kamati Teule Kushughulikia Migogoro ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji na Uwekezaji

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia uamuzi wa Bunge wa kuundwa kwa Kamati Teule, chini ya masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 uliofanywa na Bunge tarehe 1 Novemba, 2013 na kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni ya 120 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 naunda na kuwateua Wajumbe wa Kamati hii ambayo itaitwa Kamati Teule ya Kuchunguza na Kuchambua Sera Mbalimbali zinazohusu Masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji na Uwekezaji ili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

kubaini kasoro zilizomo katika matumizi ya Ardhi na hatimaye kuleta mapendekezo Bungeni ambayo yakitekelezwa na Serikali yatapunguza na kuondoa migogoro ya muda mrefu inayoendelea kati ya Wafugaji na Wakulima, Wawekezaji na Watumiaji wengine wa Ardhi.

Waheshimiwa Wabunge, hadidu za rejea za Kamati teule zitakuwa zifuatazo:-

Kwanza, kuchambua sera mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi ili kubainisha kasoro zilizomo na kuchunguza mikakati ya utekelezaji wa sera hizo iliyowekwa na Serikali;

Pili, kufanya mapitio ya taarifa nyingine za kamati na tume zilizoundwa huko nyuma kushughulikia migogoro ya wakulima na wafugaji;

Tatu, kuchambua mikakati yote ya Serikali ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji;

Nne, kuchambua mikakati ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa mazingira;

Tano, kutoa mapendekezo yatakayoondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri na utengamano kati ya wafugaji na wakulima;

Sita, kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua za kiuwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kiseru zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji; na

Saba, mambo mengine yoyote ambayo Kamati itayaona yanafaa.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona hadidu za rejea na ukubwa wa tatizo lenyewe la migogoro ya ardhi kati ya wafugaji, wakulima, hifadhi, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi. Kama nilivyosema wakati wa kuhitimisha mjadala wa hoja iliyowasilishwa kwamba Kamati Teule itakwenda kuangalia kwa ukubwa wake suala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

zima la migogoro kati ya wakulima, wafugaji na mambo yanayohusu maeneo ya hifadhi na vitu kama hivyo.

Ni dhahiri kazi itakuwa kubwa na inayohitaji umakini wa hali ya juu na muda wa kutosha katika kufikia mapendekezo yatakawasilishwa Bungeni. Hata hivyo, kutokana na uharaka wa jambo lenyewe itabidi Kamati hii ifanye kazi hii kwa kuzingatia kwamba kuchelewa kutoa taarifa yake kunaweza kukuza tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kazi kuwa kubwa Kanuni ya 121(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013 imeweka masharti kwamba Wajumbe wa Kamati Teule wasizidi Watano (5). Hivyo nimewateua wafuatao ili wakaifanye kazi hiyo. Katika uteuzi niliufanya nimezingatia mambo ya muhimu yafuatayo; uwakilishi wa vyama vilivyopo Bungeni, uelewa wa tatizo na migogoro iliyopo na inayoikabili nchi yetu, uzoefu katika masuala ya kilimo na ufugaji na jinsia.

Hivyo wafuatao nimewateua kuwa Wajumbe wa Kamati Teule.

1. Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla;
2. Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama;
3. Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya;
4. Mheshimiwa Joseph Roman Selasini; na
5. Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka wakati tulipojadili hoja hii ya kuahirisha shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura, inayohusu maelezo ya Serikali kuhusu mgogoro kati ya wafugaji na wakulima, hifadhi na uwekezaji, niliipa Kamati yetu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

na Mazingira, jukumu la kutathmini na kuangalia jinsi mpango ule wa kupambana na majangili ulivyopangwa, kasoro zilizojitokeza pamoja na mambo mengine, kutathimini iwapo kulikuwa na uzembe katika kuendesha operesheni hii ambao ulisababisha watu wasio na hatia kupoteza maisha na mali zao.

Ili kuondoa mgongano kati ya Kamati Teule na Kamati ya Kisekta, masuala yote yatakayohusiana na migogoro ya ardhi inayohusu wakulima, wafugaji na wawekezaji kwenye maeneo ya hifadhi, narudia tena. Ili kuondoa mgongano kati ya Kamati Teule na Kamati ya Kisekta, masuala yote yatakayohusiana na migogoro ya ardhi inayohusu wakulima, wafugaji na wawekezaji kwenye maeneo ya hifadhi yaachiwe Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira ambapo itaayangalia kwa upana wake na kutoa taarifa yake Bungeni.

Sasa baada ya kusema hayo Kamati Teule hii ninayoiunda itafanya kazi yake na itatuletea taarifa yake katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge. Huo ndiyo mwisho wa taarifa yangu. Katibu tuendelee.

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kuwa shughuli zilizopangwa katika Mkutano wa Kumi na Tatu zimekamiliika.

KUAHIRISHA BUNGE

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha shughuli za Mkutano wa Kumi na Tatu wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwa kutufikisha salama siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu ulijumuisha kazi kubwa zifuatazo:-

(i) Kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

(ii) Kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2013, *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill 2013]*;

(iii) Kujadili Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaafu wa Mwaka 2013 *[The GEPF Retirement Benefit Bill, 2013]*; na

(iv) Kujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba *(The Constitutional Review Act)* Sura ya 83.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki katika Kamati ya Mipango hapa Bungeni kwa kujadili kwa kina mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2014/2015.

Napenda kuwahakikishia kuwa, maoni na ushauri kama yalivyotolewa na Waheshimiwa Wabunge yatazingatiwa na Serikali kila moja kwa uzito wake wakati wa maandalizi ya Bajeti ya 2014/2015. Vilevile, niwashukuru kwa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaafu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilisha kazi hizo muhimu, pia katika Mkutano huu, jumla ya maswali 120 ya msingi na 305 ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge yalijibiwa na Serikali. Aidha, Maswali 6 ya msingi na 6 ya nyongeza yalijibiwa kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kauli za Mawaziri/Maazimio. Mkutano huu pamoja na kazi za msingi zilizopangwa, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kupata Kauli za Mawaziri ikiwemo Kauli ya Waziri wa Eliumu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu Upangaji wa Madaraja katika Matokeo ya Mitihani katika Shule za Sekondari, na Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

ya Muungano wa Tanzania kuhusu msimamo wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Katika Mkutano huu pia, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kumsikiliza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizungumza na Wananchi kupitia Bunge lako Tukufu. Mtakubaliana nami kwamba hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa nzito na yenye kuonesha umakini, umahiri na busara ambazo ni sifa mojawapo za Rais wetu kati ya nyingi nzuri alizonazo. (*Makofi*)

Tunachotakiwa ni kutumia maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa kuyafikisha kwa Wananchi katika maeneo yetu ili nao waweze kuelewa hali halisi ya yanayotokea katika Jumuiya yetu. Aidha, Hotuba ya Rais imegusa maeneo mengine ambayo sisi Wabunge tunatakiwa kushirikiana na Wananchi katika kujipanga vizuri namna ya kukabiliana na matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2013/2014. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali katika Robo ya Kwanza ya Mwaka 2013/2014. Hotuba yangu kwa leo imejikita zaidi kuelezea utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2013/2014 na maeneo machache katika Sekta ya Kilimo na Nishati. Lakini kabla ya kuelezea mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali katika Robo ya Kwanza ya mwaka 2013/2014, naomba kueleza kwa muhtasari kuhusu mwenendo wa baadhi ya viashiria muhimu vya uchumi hususan Ukuaji wa Uchumi na Mfumuko wa Bei.

Taarifa za awali zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba Ukuaji wa Pato la Halisi la Taifa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2013, ulikuwa asilimia 7% ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Sekta zilizoonesha kuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji ambayo imekua kwa asilimia 18.4, Sekta ya Fedha Asilimia 14.6 na Sekta ya Ujenzi asilimia 8.7.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mfumuko wa bei, takwimu zinaonesha kuwa kasi ya upandaji bei imepungua kutoka wastani wa asilimia 13.5 mwezi Septemba, 2012 hadi asilimia 6.1 mwezi Septemba, 2013. Kushuka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa zaidi na upatikanaji wa chakula cha kutosha ndani ya Nchi. Mwenendo huu mzuri wa viashiria vya uchumi jumla unatupa matumaini makubwa kwamba jitihada za Serikali za kuimarisha usimamizi wa uchumi na kuleta maendeleo endelevu ya wananchi wetu zinaanza kuzaa matunda.

Mheshimiwa Spika, katika robo ya kwanza ya mwaka 2013/2014 kuanzia mwezi Julai hadi Septemba 2013, mapato yote yaliyokusanywa na Hazina yalifikia Shilingi Trilioni 3.08; sawa na asilimia 85.7 ya makadirio ya Shilingi Trilioni 3.59.

Pamoja na mwenendo huo wa ukusanyaji mapato, changamoto kubwa zinazokabili eneo la Mapato ya Serikali ni kuchelewa kuanza kwa wakati kwa ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya vyanzo vya mapato. Changamoto nyingine ni miundombinu isiyokidhi mahitaji ya usafirishaji endelevu hasa reli ya kati, bandari, usafiri wa anga na barabara.

Miundombinu bora ni muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi na kukuza ajira; na hivyo kuiwezesha Serikali kukusanya mapato zaidi kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi. Serikali inafanyia kazi changamoto hizo ili kuzipatia ufumbuzi mapema.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, hadi kufikia mwezi Septemba 2013; matumizi yalifikia Shilingi Bilioni 3,806.5, sawa na asilimia 98.5 ya lengo la kutumia Shilingi Bilioni 3,854.2. Kati ya matumizi hayo, Shilingi Bilioni 3,058 ni matumizi ya kawaida na Shilingi Bilioni 747.9 ni matumizi ya maendeleo.

Katika kipindi hiki, sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali ya kawaida na maendeleo imeelekezwa katika maeneo yenye kuleta ufanisi na tija kubwa kama vile kuboresha miundombinu ya barabara, ambayo mgao wake

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

ulikuwa Shilingi Bilioni 182.5 za matumizi ya kawaida na maendeleo, sekta ya elimu Shilingi Bilioni 229.2; Sekta ya nishati, Shilingi Bilioni 159.9; sekta ya kilimo Shilingi Bilioni 119.6 na sekta ya maji Shilingi Bilioni 51.3.

Vilevile, Serikali imelipa mishahara ya watumishi wa Umma kwa wakati. Changamoto kubwa iliyopo kwenye matumizi ya Serikali ni kuwepo kwa mahitaji makubwa ya matumizi yasiyowiana na mapato; jambo ambalo linailazimu Serikali kukopa kutoka Mabenki ya Ndani.

Serikali itaendelea kuonisha Matumizi na ukusanyaji wa mapato, hasa yale ya ndani pamoja na kuzingatia viwango vya Matumizi vilivyoidhinishwa na Bunge. Aidha, Serikali itaendelea kuweka msisitizo wa kuelekeza matumizi kwenye vipaumbele vilivyoainishwa katika bajeti ya Serikali ambavyo ni vyanzo muhimu vya kuongeza mapato, kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mfumo mpya wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa yaani *big results now (BRN)*. Muundo wa Mfumo. Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Serikali ilianzisha mfumo mpya wa "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa au *Big Results Now (BRN)* ili kuongeza ufanisi katika usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango yetu ya maendeleo, hususan, mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016).

Hatua hii ilichukuliwa baada ya kuona namna Mfumo kama huo ulivyoziwezesha Nchi kadhaa, na hasa Nchi ya Malaysia, kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kiuchumi na kijamii katika kipindi kifupi. Kwa ukumbusho tu, mfumo huo unatekelezwa katika maeneo Sita ya matokeo muhimu kitaifa *national key results areas* katika awamu yake ya kwanza, ambayo ni nishati ya umeme, uchukuzi, kilimo, elimu, Maji na ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya kuahirisha Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, tarehe 6 Septemba, 2013, nilitoa taarifa ya awali kuhusu utekelezaji

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wa mfumo huu Mpya kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2013. Katika taarifa hiyo, nilieleza kuwa tumepiga hatua za kuridhisha katika uundaji wa mfumo wa kuleta matokeo ya haraka, ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuteua uongozi wa juu wa Taasisi Maalum yaani *President's Delivery Bureau (PDB)* inayomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia ipasavyo utekelezaji wa miradi na programu zilizoainishwa.

Hivi sasa zoezi la kuajiri watumishi wa taasisi ya *president's delivery bureau* na vitengo vya Wizara vya ufuatiliaji yaani *ministerial delivery units (MDUs)* watakaochukua nafasi za watumishi walioazimwa kutoka kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali, sekta binafsi, na Asasi zisizo za Kiserikali ambao walikuwepo katika hatua zake za maandalizi limeanza. Ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wote waliotumika katika chombo hiki tangu kilipoundwa kwa uzalendo na weledi waliouonesha katika kipindi hiki cha mwanzo na cha mpito.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hadi sasa vitengo vya ufuatiliaji katika Wizara zote sita (6) zinazosimamia utekelezaji chini ya mfumo huu mpya vimeanzishwa na vinaandaa taarifa za utekelezaji za kila wiki na kila mwezi, na kuziwasilisha kwenye chombo cha *President's Delivery Bureau*. Aidha, Kamati Maalum za kusimamia utekelezaji zinazoongozwa na Mawaziri husika zinakutana kila mwezi kujadili mwenendo wa utekelezaji na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji. Baraza la Kusimamia Mageuzi na Utekelezaji yaani *Transformation and Delivery Council (TDC)* limeundwa na lilikutana tarehe 11 Oktoba, 2013.

Katika Kikao hicho, Baraza lilipokea na kujadili muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa Mfumo mpya wa Kusimamia, Kufuatilia na Kutathmini Miradi ya Kipaumbele katika maeneo sita ya matokeo ya kitaifa. Baraza liliridhika na hatua za awali za utekelezaji na lilitoa mwongozo stahiki wa hatua za kuchukuliwa pale ilipohitajika. Baraza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

litaendelea kukutana mara kwa mara ili kutathmini na kutoa mwelekeo wa utekelezaji wa mikakati iliyowekwa ya mfumo huu mpya.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mikakati katika maeneo makuu Sita ya matokeo kitaifa. Utekelezaji wa mikakati katika maeneo makuu sita ya matokeo kitaifa ulianza mara baada ya uchambuzi wa maabara kukamilika. Mafanikio ya kuridhisha yamepatikana katika kila moja ya maeneo yale sita, hasa ikizingatiwa kwamba mfumo huu ni mageuzi makubwa sana katika utendaji Serikalini. Katika kipindi cha miezi mitatu ya mwanzo ya mwaka huu wa fedha, kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2013; kwa mfano, baadhi ya matokeo yaliyopatikana ni pamoja na yafuatayo:-

Kwanza, katika sekta ya kilimo, Serikali inatekeleza miradi 26 ya umwagiliaji kwa Wakulima wadogo na pia imekarabati maghala 26 ya mpunga kati ya 39 yanayotumiwa na wakulima katika maeneo yaliyopewa kipaumbele hususan katika eneo la *SAGCOT*.

Pili, katika sekta ya nishati ya umeme, jumla ya Wateja wapya 27,494 wameunganishwa na kupatiwa umeme, ikiwa ni asilimia 18.3 ya lengo la kuunganisha wateja wapya 150,000 hadi mwisho wa mwaka 2013/2014. Aidha, vipande vya bomba la gesi 20,491 vinavyotosheleza ujenzi wa kilomita 243.8 za bomba la gesi tayari vimewasili Nchini, na uhomeleaji wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam umekamilika kwa kilomita 124.3. Vilevile, kilomita 447 za njia ya bomba la gesi zimesafishwa.

Tatu, katika sekta ya elimu, shule za msingi 5,916 zilipatiwa mitihani ya marejeo na mazoezi, sawa na asilimia 100 ya lengo la mwaka. Aidha, mafunzo kazini kuhusu ufundishaji yametolewa kwa walimu katika Shule 1,325 sawa na asilimia 65 ya lengo la shule 2,048 kwa mwaka huu wa fedha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Nne, kwa upande wa huduma za maji, wananchi wapatao 752,000 waishio vijijini wamepatiwa huduma ya maji.

Mafanikio haya yanafanya idadi ya wananchi waishio vijijini ambao wanapata majisafi na salama kufikia takribani Milioni 15.9. Kasi hii ya upanuzi wa huduma za maji Vijijini imewezekana baada ya Wizara ya Maji kugatua madaraka ya usimamizi wa miradi husika kwa sekretarieti za Mikoa na halmashauri za Wilaya, jambo ambalo limewafanya watendaji kuwajibika na kuharakisha utendaji wao wa kazi. Aidha, hatua zilizochukuliwa zimeiwzesha Wizara ya Maji kuongeza ufanisi katika masuala ya ununuzi wa huduma, ikiwemo ujenzi na vifaa vyake, kutoka wastani wa siku 265 za hapo awali hadi siku 90 za sasa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya na mengine mengi ambayo sikuyataja hapa yameonyesha kuwa tukidhamiria, tunaweza kubadilisha kabisa matokeo ya juhudi zetu na kuifikia dhamira yetu ya kuwa ni Taifa la Kipato cha Kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafunzo yaliyotolewa mapema mwezi Juni, 2013 kwa Watendaji wa Wizara husika, Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote Nchini, mnamo mwezi Septemba 2013 nilikutana na Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara ili kujadili kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi ya kipaumbele chini ya mfumo huu. Aidha, katika Vikao hivyo, nimezielekeza Wizara, Mikoa na Halmashauri zote Nchini kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kuchambua miradi iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha ambayo ipo nje ya Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa kwa kutambua manufaa yanayotarajiwa baada ya kukamilika na mahitaji halisi;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Pili, kuipanga miradi hiyo kwa kipaumbele ili kuweka mkazo katika miradi itakayokamilika haraka na kuwa na manufaa makubwa kwa Wananchi; na,

Tatu, kuweka utaratibu wa Kimfumo na Kitaasisi wa kufuatilia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, niinafurahi kutoa taarifa kuwa Wizara na Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zimeupokea mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa kwa hamasa kubwa. Ili kuhakikisha azma yao ya kutekeleza majukumu yao katika mfumo huu kikamilifu, ilihamuliwa kuwa viundwe vitengo vya kusimamia utekelezaji katika ngazi ya mkoa yaani *Regional Delivery Units (RDUs)*, sambamba na vile vitengo vya ufuatiliaji vya Wizara ili utekelezaji katika maeneo makuu ya matokeo kitaifa ufanyike kwa ufanisi na umakini stahiki.

Hatua hii inazingatia umuhimu wa kuhakikisha kuwa maeneo kama Elimu na Maji ambayo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zina mchango mkubwa katika utekelezaji yanapata msukumo wa kutosha. Kazi hii imeshaanza, na taarifa zilizowasilishwa ni za kutia moyo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mafanikio ya awali yaliyopatikana, Serikali imetoa maelekezo kwa Wizara, Idara na Taasisi ambazo bado hazijaingia katika mfumo wa tekeleza kwa matokeo makubwa sasa, zisisubiri hadi zitakapoingia rasmi bali zianze kujipanga na kutekeleza mipango, miradi na program zao kwa kutumia mbinu ambazo zinatumiwa katika mfumo huo pamoja na rasilimali fedha na wataalam waliopo.

Msisitizo ni kwamba Wizara zote na Mikoa ijipange upya na kuongeza ubunifu na kufanya vizuri zaidi katika kuimarisha usimamizi wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba Taifa letu linafikia malengo ya maendeleo tuliyojiwekea katika Dira ya maendeleo ya Taifa 2025. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha usimamizi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wa Watendaji wao kwa kuzingatia taratibu za uwajibikaji zilizowekwa chini ya mfumo huu mpya ili kuleta ufanisi na tija ya utendaji Serikalini pamoja na kupata matokeo makubwa tarajiwa ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya taifa wa mwaka 2014/2015. Mwanzoni mwa Mkutano huu wa Bunge Serikali iliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2014/2015. Napenda kutumia fursa hii tena kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa maoni na michango yao mizuri ambayo itatuwezesha kuboresha Mpango na Bajeti ya Mwaka ujao wa Fedha 2014/2015. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Stephen Wasira pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta waliotoa maelezo fasaha ya ufafanuzi wa Hoja zilizojitokeza wakati wa Mjadala wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo. Kwa kuzingatia michango mizuri na yenye tija iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri wakati wa kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2014/2015, nami naomba uniruhusu kusisitiza mambo machache kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakvokumbuka katika majadiliano yaliyokuwa yanaendelea, moja ya jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia kwa kina, ni juu ya wingi wa vipaumbele vya Taifa. Aidha, imeonekana pia kuwa miradi ya maendeleo ni mingi sana kiasi kinachosababisha miradi hiyo kutotekelezeka kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha.

Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa vipaumbele vilivyopendekezwa na Serikali vinategemeana na vinalenga kutanzua vikwazo vikuu vya kiuchumi Nchini ili kufungua fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuharakisha maendeleo na ustawi wa Wananchi wa Tanzania. Pendekezo la Serikali ni kuwa njia bora si kupunguza vipaumbele hivi sasa, bali ni kupanga vizuri mtiririko wa utekelezaji wa miradi ndani ya kila kipengele, kuongeza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

jitihada za kuongeza Mapato, na kusimamia nidhamu ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ni wa kwanza unaojenga msingi wa mipango mingine ya maendeleo ya miaka mitano itakayoandaliwa, ni dhahiri kuwa kasi ya utekelezaji wake itarahisisha utengenezaji wa mipango mingine na kupunguza vipaumbele vya msingi katika mipango ijayo. Hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge washirikiane kwa karibu na Serikali kuhakikisha kuwa miradi iliyopangwa katika ngazi zote inatekelezwa kwa ufanisi ili mpango huu wa mwanzo utekelezeke kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mjadala na hoja nyingine zilijielekeza katika changamoto za upatikanaji wa Ajira kwa Vijana Nchini. Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, asilimia 34.7 ya nguvu kazi ya Tanzania ni Vijana wa umri wa kati ya miaka 15 - 35. Kundi hili la Vijana ndilo lenye kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira cha asilimia 13.4 hapa Nchini. Pamoja na kuwa vijana hawa wamekuwa wakipata kazi hususan katika sekta za ujenzi, kilimo na hoteli, ajira zao nyingi zimekuwa za muda.

Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imeandaa Programu ya Ajira kwa Vijana, itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu. Malengo ni kupatikana fursa za ajira 840,000 kwa kuwezesha jumla ya miradi 10,000 ya wahitimu wa elimu ya juu wapatao 30,000 kutoka vyo mbalimbali ambao watatoa ajira za moja kwa moja kwa wahitimu wengine 270,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 540,000. Programu hii itajengea vijana uwezo katika stadi za kazi; ujasiriamali; na kuwapatia Vijana mitaji, nyenzo na vifaa vya kufanyia kazi; na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Serikali inatarajia kuelekeza fedha zaidi katika kipindi husika ili kuwezesha utekelezaji wa programu hiyo. Aidha, naipongeza sekta binafsi kwa mchango wao mkubwa katika kukuza uchumi wa Nchi na kuongeza ajira kwa vijana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, kilimo ni moja ya maeneo ya kipaumbele katika mpango wa mwaka 2014/2015. Hili ndilo eneo kubwa kwa maana ya kuongeza fursa za ajira na kipato kwa wananchi wanaoishi vijijini, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa namna ambayo ni shirikishi ili kupunguza umaskini.

Hivyo, ili kujibu matatizo ya msingi ya umasikini wa kipato Mpango wa Maendeleo 2014/2015 utatoa kipaumbele katika mambo muhimu yafuatayo:-

Moja, utafiti wa kilimo cha mazao, hasa katika uzalishaji wa mbegu bora, mifugo na uvuvi.

Pili, kuimarisha huduma za ugani kwa kilimo, mifugo na uvuvi na kuimarisha upatikanaji na matumizi ya mbolea kwa ajili ya kilimo.

Tatu, kuimarisha Ushirika wa Wakulima na Wafugaji.

Nne, kuongeza fursa za mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Benki ya Kilimo mwezi Januari 2014;

Tano, kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, na mifugo;

Sita, kujenga na kukarabati skimu za umwagiliaji;

Saba, upatikanaji wa ardhi kwa kilimo na mifugo kwa kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi; na

Nane, kuendeleza shughuli za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo huandaliwa katika ngazi zote Tano za Utawala kulingana na majukumu ya Serikali ambazo ni Vijiji na Mitaa, Kata, Mamlaka za Serikali za Mitaa, yaani Halmashauri, Mikoa na Tano, Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wa Serikali. Mamlaka husika katika ngazi zote zinatakiwa kuandaa Mipango yao kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama yalivyoainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015. Mipango lazima ilenge katika maeneo yenye kuleta matokeo makubwa na ya haraka hasa katika kuchochea maendeleo ya maeneo mengine na Programu nyingine katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Katika kila ngazi, wadau wengine kama vile sekta binafsi, asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya dini na washirika wa maendeleo washirikishwe kikamilifu. Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali ziandae Mpango na kuuwasilisha Ofisi ya Rais, Tume ya Mpango Wiki ya Nne ya mwezi Januari mwaka 2014.

Katika ngazi za Mikoa na Wilaya, uandaaji uanze katika ngazi ya Kijiji na Mtaa, Kata, Halmashauri na hatimaye kwenye Mkoa. Mpango uliopitishwa na Mkoa uwasilishwe Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Fedha, wiki ya nne ya mwezi Januari, 2014. Mpango wa Maendeleo wa Taifa utajadiliwa na Bunge kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2014 na utekelezaji wake utaanza mwezi Julai 2014 hadi Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015 ndiyo yatatumika katika utayarishaji wa mipango ya maendeleo ya Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka ujao wa fedha 2014/2015. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kutumia taarifa zilizotolewa hapa Bungeni kutoa ufafanuzi kwenye Vikao vya Baraza la Madiwani katika Halmashauri zao wakati wa kujadili Mipango yao.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuzihimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuainisha vipaumbele vinavyolenga katika maeneo yenye kuleta matokeo makubwa na ya haraka ya kiuchumi na kijamii; na pia yenye kuchochea maendeleo ya maeneo mengine. Vilevile, vipaumbele vya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Halmashauri vilenge kufungulia fursa za ajira, kuongeza mapato ya ndani na kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya kilimo na hali ya chakula Nchini. Kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula nchini hadi kufikia mwezi Oktoba 2013 ni ya kuridhisha kufuatia mavuno mazuri ya msimu wa kilimo wa 2012/2013 ambapo mazao yake yanaendelea kuingia sokoni kutoka maeneo mbalimbali hapa nchini.

Tathmini ya awali iliyofanyika mwezi Julai/Agosti, 2013 inaonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2012/2013 utafikia tani 14,383,845 za chakula zikiwemo tani 7,613,221 za mazao ya nafaka na tani 6,770,624 za mazao yasiyo ya nafaka. Kiasi hicho cha chakula kilichozalishwa ni ongezeko la tani 2,234,726 za chakula, ikilinganishwa na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2013/2014 ya tani 12,149,120.

Kiwango hicho kinajumuisha tani 354,015 za mahindi na tani 466,821 za mchele. Hivyo napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kuwa tutakuwa na chakula cha kutosha nchini kwa asilimia 118. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tathmini hiyo inaonesha kuwa, pamoja na kuwepo kwa chakula cha kutosha na cha ziada, Halmashauri 61 katika Mikoa ya Manyara, Shinyanga, Simiyu, Arusha, Dodoma, Lindi, Tanga, Singida, Mara, Morogoro, Kilimanjaro, Mwanza, Pwani, Mtwara, Kigoma na Tabora zinatarajiwa kuwa na uhaba wa chakula. Natoa wito kwa Halmashauri zinazohusika katika Mikoa hiyo kufuatilia kwa karibu utaratibu wa kupata chakula kinachotolewa kutoka maeneo yenye ziada na kuhakikisha kuwa kinafika mapema kwenye maeneo yao kabla Wananchi wa maeneo hayo hawajaanza kulalamika.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei za vyakula nchini. Kutokana na hali ya upatikanaji wa chakula kuwa nzuri, bei za wastani za vyakula hasa mahindi na mchele katika soko nchini zimeendelea kushuka. Kwa mfano, bei ya mahindi ilishuka kutoka shilingi 774.30 kwa kilo mwezi Februari, 2013 hadi shilingi 535.40 kwa kilo mwezi Septemba 2013.

Kwa upande wa mchele, bei kwa kilo moja imeshuka kutoka shilingi 1,825.45 mwezi Februari, 2013 hadi kufikia shilingi 1,206.70 mwezi Septemba 2013, na bei ya mchele imeshuka zaidi hadi kufikia shilingi 1,146.70 katika mwezi Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ununuzi na Akiba ya Chakula ya Taifa. Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula imepanga kununua Tani 250,000 za nafaka katika msimu wa 2013/2014. Hadi kufikia tarehe 23 Oktoba, 2013, Wakala alikuwa umekwishanunua kiasi cha tani 218,412 za nafaka sawa na asilimia 87.37 ya lengo lililowekwa ambapo tani 217,919 kati ya hizo ni za mahindi na tani 493 ni za mtama. Aidha, hadi kufikia tarehe 23 Oktoba 2013, maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula yalikuwa na jumla ya tani 232, 921 za nafaka, kati ya hizo tani 232,419 ni za mahindi na tani 493,103 ni za mtama. Kiasi hiki cha nafaka kinajumuisha albaki ya tani 25,452 za mahindi kutoka msimu uliopita wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe katika Halmashauri 61 zilizoainishwa kuwa na hali tete ya chakula kwa lengo la kubainisha idadi ya watu wenye uhaba wa chakula ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili. Nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwahimiza wakulima hasa walioko katika maeneo yenye chakula cha ziada kuhifadhi chakula cha kutosha kwa mahitaji ya kaya zao. Aidha, Wakala wa Taifa na Hifadhi ya chakula wajipange vizuri kuhamisha chakula kutoka maeneo yenye ziada na kupeleka kwenye maeneo yaliyoainishwa kuwa na hali tete mara taarifa ya upungufu itakapotolewa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba kuna chakula cha kutosha, natambua changamoto zilizopo katika ununuzi wa chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Natambua kuwepo kwa madeni yanayotukabili kwenye ununuzi wa nafaka kwa ajili ya wakala yaani *NRFA*. Hata hivyo, mikoa yote ambayo imehusika na uuzaji wa mahindi kupitia chombo hiki ambayo ni Arusha, Dodoma, Njombe, Shinyanga, Ruvuma, Rukwa na Tanga madeni yote ambayo wakulima wanadai yatalipwa ndani ya mwaka huu wa fedha na jambo hili linashughulikiwa hivi sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pembejeo za Ruzuku. Kama nilivyoeleza katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge, katika msimu wa 2013/2014 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 112.564 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, na pembejeo. Aidha, nilielezea kuhusu utaratibu mpya wa kutoa ruzuku utakaohusisha uwiano wa asilimia 80 kwa vocha na asilimia 20 mikopo. Ili kuhakikisha mfumo huu mpya unatekelezwa kikamilifu na kuleta matokeo yaliyotarajiwa, Serikali imetoa mafunzo ya utoaji pembejeo kwa njia ya mikopo kwa Washauri wa Kilimo wa Mikoa, Maafisa Ushirika wa Mikoa na Wilaya na Maafisa Kilimo wa Wilaya kwa awamu mbili: awamu ya kwanza ikihusisha Mikoa ya Shinyanga, Geita na Manyara; na awamu ya pili inahusu mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Iringa.

Uchambuzi wa takwimu za Vyama vya Ushirika na Vikundi vya Wakulima watakaokopeshwa pembejeo za kilimo mwaka 2013/2014 umefanyika katika Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Shinyanga, Njombe, Mbeya, Geita na Manyara. Takwimu zinaonesha kuna *SACCOS* 214, *AMCOS* 163 na Vikundi vingine 51 vyenye wakulima 88,290 watakopeshwa pembejeo za kilimo. Naomba kutoa wito kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuendeleza mafunzo haya kwa Mikoa iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Usambazaji wa Vocha za Pembejeo. Kuhusu hali ya usambazaji wa vocha za pembejeo katika msimu wa 2013/2014 napenda kuliarifua

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Bunge lako Tukufu kwamba, jumla ya vocha 2,796,300 kwa ajili ya kaya 932,100 zikiwemo vocha 932,100 za mbolea ya kupandia, 932,100 za mbolea ya kukuzia, vocha 441,100 za mbegu za mahindi chotara, vocha 432,000 za mahindi ya OPV na vocha 60,000 za mbegu za mpunga zilisambazwa katika mikoa yote hapa Nchini. Nitoe wito kwa viongozi wa Mikoa na Wilaya kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wengine kuhakikisha kuwa Wananchi wanapata na wanatumia vocha hizi kupata pembejeo kama ilivyokusudiwa. Aidha, tushirikiane kuhakikisha kuwa wale watakaokwenda kinyume na utaratibu huu wa usambazaji wa vocha hizo wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, changamoto za mbolea ya Minjingu. Juhudi za Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo za ruzuku ziko dhahiri. Hata hivyo, imebainika kwamba katika mahitaji ya mbolea, kilio kikubwa cha wakulima ni kupatiwa mbolea kwa wakati. Aidha, wapo wananchi wanaolalamikia mbolea ya Minjingu Mazao ambayo ni kweli hapo awali ilikuwa na matatizo. Lakini sasa, mbolea hii imeboreshwa kwa kiwango kikubwa kwa kuongezewa virutubisho.

Mheshimiwa Spika, mbolea ya Minjingu ya awali ilikuwa na virutubisho vya udongo viwili tu vya Kalisiumu na Fosfeti. Mbolea ya Minjingu Mazao imeboreshwa kwa kuongezwa virutubisho vinne zaidi na kufanya virutubisho hivyo kuwa sita yaani Kalisiumu, Fosfeti, Naitrojeni, Salfa, Boroni na Zinki. Kwa msingi huo, Mbolea ya Minjingu mazao inaweza kutumika katika aina mbalimbali za udongo tofauti na ilivyokuwa awali. Aidha, Mbolea ya Minjingu Mazao ni ya chengachenga yaani *granulated* tofauti na ya awali ambayo ilikuwa katika mfumo wa unga yaani *dust* ambapo pengine matumizi yake hayakuwa rafiki kwa mkulima. Baada ya kuboreshwa, kwa sasa mbolea hii ya Minjingu inatumika kwa mazao mengi hasa mahindi, mpunga na alizeti katika sehemu mbalimbali hapa nchini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, mkulima anahitaji kutumia mifuko miwili ya mbolea ya Minjingu Mazao ya kilo 50 kila mmoja kwa wakati mmoja ikilinganishwa na mfuko mmoja wa kilo 50 wa mbolea ya *DAP*.

Hata hivyo, ukilinganisha na mbolea ya *DAP*, mkulima anayetumia Minjingu Mazao anawezesha shamba lake kupata virutubisho zaidi. Kwa hiyo, Mbolea ya Minjingu Mazao ni nafuu ikilinganishwa na Mbolea ya *DAP*. Bei ya mbolea ya Minjingu Mazao kwa mfuko mmoja ni shilingi 32,500/= na kwa hiyo kwa mifuko miwili ni shilingi 65,000/= katika Wilaya zote Nchini ikilinganishwa na bei ya wastani ya shilingi 75,000/= ya mfuko mmoja wa *DAP*.

Aidha, kwa aina zote mbili za mbolea zinapotumika kupandia, lazima mkulima aweke mbolea nyingine ya kukuzia ambayo ina virutubisho vingi vya Naitrogeni kama *CAN* au *UREA*. Majaribio ya kutumia Mbolea ya Minjingu yalianza mwaka 1977 na kuendelea hadi mwaka 2006 ikiwa katika hali ya unga. Mwaka 2007 Mbolea hiyo iliiboreshwa kwa kuiweka katika hali ya chenga chenga (*granulation*) ingawa virutubisho havikuboreshwa. Mbolea hiyo iliendelea kutumika katika hali hiyo hadi mwaka 2009. Hivyo, mwaka 2010 mbolea hiyo iliiboreshwa kwa kuongezea virutubisho nilivyovitaja na kuwekwa sasa katika soko.

Kwa sasa, Mbolea ya Minjingu Mazao inatumika katika Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Njombe, Katavi, Kigoma na Morogoro. Aidha, kuna mikoa mingine ambako mbolea hii imepelekwa pamoja na mbolea nyingine kwa ajili ya Wakulima wenyewe kufanya maamuzi ya kuchagua.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya Mbolea ya Minjingu Mazao katika mwaka 2012/2013 yamewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi, mpunga na alizeti kwa ekari hasa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Changamoto kubwa ni elimu juu ya matumizi sahihi ya mbolea hiyo kwenye baadhi ya maeneo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Katika kutatua changamoto hii, Wizara inashirikiana na mmiliki wa Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu kuendesha mashamba darasa katika Wilaya mbalimbali Nchini. Vilevile, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, inaendelea kufanya utafiti katika maeneno mbalimbali ya nchi ili kuzidi kuboresha matumizi sahihi ya mbolea hiyo katika aina mbalimbali za udongo.

Changamoto zinazohusiana na mbolea ya Minjingu katika wilaya ya Mbozi hizi zitaangaliwa kwa namna yake. Hata hivyo, katika uchunguzi tulioufanya ilibainika kwamba, mmoja wa wakala katika wilaya ya Mbozi alitumia mifuko ya mbolea nyingine akaweka mbolea ya Minjingu, na kwa maana hiyo mkulima aliyenunua mfuko mmoja akidhani amenunua mbolea hiyo nyingine kumbe amenunua Minjingu ni dhahiri kiasi hicho kisingeweza kutosheleza kuweza kuimarisha shamba la mkulima katika ekari yake moja ambayo inahitaji mifuko mwili. Hata hivyo, wakala huyo amekamatwa na amefikishwa kwenye vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kama hili limejitokeza pia mkoani Morogoro ambapo wakala mwingine naye hakuwa mwaminifu, alitumia ujanja huo huo aka- *pack* mbolea hii ya Minjingu katika mifuko ya mbolea ya aina nyingine na kuiuza kwa bei kubwa ili aweze kufaidika zaidi, lakini kwa gharama ya mkulima. Naye huyu amekamatwa na hatua za kisheria zinaendelea. *(Makofi)*

Nataka niwasihi sana wakala wote na Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wasimamie vizuri zoezi hili na watumie wataalam tulionao kuhakiki mbolea yote inapopelekwa kwenye maeneo yao isije ikachakachuliwa na hivyo kuleta malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto zilizojitokeza katika matumizi ya mbolea ya Minjingu katika maeneo mbalimbali nchini Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wakulima kuhusu namna bora ya kutumia mbolea hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Pili, Mamlaka ya Udhubiti wa Mbolea imeagizwa kufuatilia na kufanya uchunguzi wa madai ya wakulima kuhusu changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika za matumizi ya mbolea ya Minjingu pamoja na mbolea nyingine mbalimbali.

Tatu, naomba kuiagiza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuendelea kushirikiana na wadau kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha kwamba mbolea itakayotumika katika maeneo hayo inawiana na hali ya udongo unaohusika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji na Ununuzi wa Mazao ya Biashara. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na changamoto mbalimbali za uzalishaji na ununuzi wa baadhi ya mazao ya biashara hapa nchini ikiwemo kilimo cha zao la Pamba, Korosho, Tumbaku na Kahawa. Kwa kuzingatia ufinyu wa muda, leo naomba uniruhusu nizungumzie kidogo kuhusu kilimo cha mazao mawili; Pamba na Korosho.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji na ununuzi wa zao la Pamba. Serikali inaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa wakulima wa Pamba wanazalisha kwa tija kwa kutumia teknolojia mbalimbali zikiwemo matumizi ya mbegu bora, utumiaji wa pembejeo, kutoa huduma za ugani kwa kupitia Maafisa wa Kilimo katika Halmashauri za Wilaya mbalimbali katika maeneo yanayolima Pamba kwa kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. *(Makofi)*

Katika kilimo hiki cha pamba, zana za kilimo zinazotumika kwa sasa ni majembe ya kukokotwa na wanyama pamoja na majembe ya mkono kwa ajili ya kulima. Hii ni dhahiri haiwezi kusaidia kuongeza tija katika kilimo hiki cha zao la Pamba. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na juhudi zake za kutafuta njia mbalimbali kuhakikisha kwamba kilimo hiki kinatumia zana za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Wizara kupata masoko ya uhakika ya pamba. Serikali pia inaendelea kuhakikisha kwamba pamba inaongezwa thamani hapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

nchini kwa kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya nyuzi na nguo. Uwekezaji mpya unafanyika kwa kujenga kiwanda cha nyuzi na nguo cha Dahong Mkoani Shinyanga na pia mradi mkubwa wa kuzalisha pamba, kuchambua, kutengeneza nyuzi, kutengeneza vitambaa na nguo unaotarajiwa kutekelezwa na kampuni ya Kijapani (NITORI) katika wilaya ya Handeni. Kwa sasa mradi huo uko katika hatua ya umilikishwaji wa ardhi. (*Makofi*)

Vilevile, Serikali imeanzisha mafunzo ya uhandisi na ubunifu katika viwanda vya nyuzi na nguo. Pia tumeanzisha kozi ya ubunifu wa mitindo katika mitaala ya VETA na mafunzo ya shahada ya uzamili katika *textile* katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo ni kuhakikisha kuwa kuna wataalaamu wa kutosha katika mchakato wa kuongeza thamani ya pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tofauti za ubora wa mbegu za pamba manyoya na *De - linted*. Sina shaka watanzania wameshasikia kuwa kwa sasa tunayo aina moja kuu ya mbegu ya Pamba ambayo inazalishwa katika kituo chetu cha utafiti cha Ukiriguru. Pamba hii kwa sasa imekuwa ikitumika zaidi kwa ajili ya kupanda katika mashamba ya wakulima ikiwa katika mfumo wa manyoya. Hivi karibuni tumepata kiwanda ambacho sasa kinaondoa manyoya na kupanga viwango vya mbegu hiyo yaani (*De-linted*). Hivyo, wakulima sasa wana uhuru wa kutumia Pamba yenye manyoya na pamba ambayo haina manyonya. (*Makofi*)

Aina hizi mbili zinatofautiana sana kwa ubora na bei. Mbegu ya manyoa ina uotaji wa chini ya asilimia 50 wakati ile ambayo haina manyoya ni zaidi ya asilimia 90. Mbegu ya manyoya hutumika nyingi kwa eneo yaani kilo 25 kwa ekari moja wakati ile iliyoondolewa manyoya inakuwa ni kilo 6 hadi 7 katika ekari moja.

Mbegu ya manyoya ina tija ndogo sana (inazalisha kati ya kilo 250 na 300 kwa ekari) ikilinganishwa ya mbegu isiyokuwa na manyoya inayozalisha kilo 450 – 1200 kwa ekari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Isitoshe mbegu ya manyoya ina uwiano mdogo wa pamba nyuzi (asilimia 33) ikilinganishwa na mbegu ambayo imetolewa manyoya ambayo uwiano wake ni asilimia 36.

Mheshimiwa Spika, jitihada za Wizara kupunguza bei ya mbegu bora. Ili kuwawezesha wakulima kutumia mbegu bora (de-linted) Serikali imetoa ruzuku ya shilingi billioni 4.8 ili kufanya mbegu hiyo ipatikane kwa shilingi 600 kwa kilo kwa mkulima badala ya shilingi 1,200 kwa kilo iliyotumika mwaka 2012/2013. Serikali pia inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutoa elimu kwa wakulima wa pamba kuhusu mbegu bora. (*Makofi*)

Kwa mfano, viongozi wa maeneo yanayolima pamba (Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na baadhi ya Madiwani) wamepelekwa katika kiwanda cha kuchakata mbegu bora za Pamba cha Kampuni ya Quton ili kupata maelezo na kujionea hali ya utendaji wa mbegu bora katika kilimo. Kupitia programu ya kuendeleza zao la pamba wakulima wawezeshaji yaani *lead farmers* 3000 wa vikundi vya Kilimo cha Mkataba wanaendelea kupewa mafunzo ya kilimo bora na matumizi ya mbegu bora ili watumike kupeleka elimu hii kwa wakulima wenzao.

Mheshimiwa Spika, katika msimu huu wa kilimo wa 2013/14, Serikali imejipanga kusimamia utekelezaji wa Kilimo cha Mkataba kwa lengo la kuleta ufanisi katika kilimo cha pamba nchini. Hatua hii inahusisha pia kutoa elimu ya kutosha na kushirikisha kwa karibu wadau katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo kwenye utaratibu mzima wa kilimo hicho ambacho kina manufaa makubwa iwapo kitaeleweka na kutekelezwa vyema kwa misingi ya haki miongoni wa wadau. Baadhi ya manufaa hayo ni:-

Moja, nihakika wa upatikanaji wa pembejeo kwa mkulima kwa mkopo, kuongeza tija kutokana na kupata pembejeo na huduma za ugani, kuongeza ubora wa pamba kutokana na matumizi makubwa ya pembejeo na huduma za ugani pamoja na vikundi kutumika kama mawakala wa kununua Pamba ya wanachama wake hivyo kusimamia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

ubora, uhakika wa soko la pamba ya mkulima, kupunguza wizi kupitia mizani ya mawakala, wakulima kupata teknolojia kupitia uwekezaji na kujenga na kuimarisha mfumo wa ushirika kupitia vikundi vya wakulima.

Mheshimiwa Spika, elimu ya kilimo cha mkataba kwa wakulima. Kupitia programu ya kuendeleza zao la pamba, wakulima wawezeshaji zaidi ya 3,000 wamekwisha pokea mafunzo ya kilimo cha mkataba wanao tumika kupeleka elimu hii kwa vikundi vya wakulima. Wagani wa Halmashauri wapatao 560 wameshapata mafunzo haya. Chini ya mpango huu kila mgani anaweza kuhudumia vikundi hadi 20.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwaagiza viongozi na wataalamu wa kilimo waendeleo kutoa elimu ya matumizi na faida ya mbegu ambazo hazina manyoya (*De-linted*) kwa wakulima wa pamba nchini. Aidha, mashamba darasa yatumike ipasavyo kuonesha tija inayotokana na aina hiyo ya mbegu za pamba inapolinganishwa na mbegu ambayo ina manyoya.

Vilevile, viongozi na wataalamu wa kilimo waendeleo kuwakumbusha wakulima wa pamba wa Tanzania kuwa utaratibu mpya wa kilimo cha mkataba una manufaa mengi na makubwa. Tuendeleo kuwashawishi wakulima kujiunga na kilimo cha mkataba bila kuwashurutisha, isipokuwa tukazanie zaidi kuwapa elimu na hasa kwa kutumia mashamba darasa. Wale watakaoshawishika kuingia katika utaratibu huu wasaidiwe kwa kila hali ili wanufaike na kilimo hicho huku wakisaidia kutoa elimu kwa Wakulima wengine ili wajunge na aina hii ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba hatua zote hizi zikifanyika kwa nia njema, wakulima wa pamba ndani ya muda mfupi watapata elimu inayotakiwa na watanufaika na matumizi ya teknolojia hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la korosho, azma ya Serikali ni kuimarisha viwanda vya korosho na kufufua vile vilivyopobinafsishwa ili viweze kusaidia kukuza soko kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wakulima wa korosho. Ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imefanya tathmini na kubaini kuwa wawekezaji wengi katika viwanda vya korosho vilivyobinafsishwa wameshindwa kutekeleza mikataba ya ubinafsishaji wa viwanda hivyo kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa fedha za uendeshaji, ukosefu wa nishati ya uhakika na viwanda kutumia teknolojia zilizopitwa na wakati. Ili kukabiliana na hali hiyo, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kushirikiana na Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma (CHC) pamoja na Wadau wengine, inaandaa mapendekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya wawekezaji walioshindwa kuendeleza viwanda hivyo.

Dhamira ya Serikali ni kwamba mwekezaji ambaye ameshindwa kuendeleza kiwanda alichonunua kwa kuzingatia makubaliano ya ununuzi na Serikali, mali hiyo irudishwe Serikalini na ifanyiwe tathmini na itangazwe upya ili kupata wawekezaji mahiri na wenye nia thabiti ya kuendeleza viwanda husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hiyo, Bodi ya Korosho Tanzania imeandaa mpango wa ubanguaji wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2012/2013 ambao umelenga kuwasaidia wabanguaji wadogo na wa kati kuendesha shughuli za ubanguaji kwa ufanisi kwa kuwapatia mafunzo, vifaa vya kubangulia, na kuwatafutia masoko ya ndani, masoko ya kanda na masoko ya nje.

Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kwamba, Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Korosho kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania, umetenga fedha kwa ajili ya kujenga viwanda vitatu katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara, na Pwani kwa ajili ya kuwawezesha wabanguaji wadogo na wa kati kumaliza baadhi ya hatua za ubanguaji katika viwanda hivyo kwa ajili ya kukidhi matakwa ya masoko makubwa ya korosho duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha kilimo cha korosho, katika mwaka 2013/2014, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya dawa, kutoa huduma za ugani na kuhamasisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

wakulima wahudumie mikorosho na kupuliza dawa mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa korosho, katika msimu huu wa 2013/2014 ununuzi wa Korosho utaendelea kwa kutumia mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani. Ukusanyaji wa korosho kutoka kwa wakulima umeanza katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa mfano, katika mkoa wa Mtwara, mnada wa kwanza wa korosho ulianza tarehe 25 Oktoba, 2013 ambapo ulihusisha vyama vya msingi vya mkoa wa Mtwara. Korosho zote zilizokuwa zimekusanywa na kutangazwa katika kila mnada zilinunuliwa. Bei ya korosho katika mnada wa kwanza ilikuwa kati ya shilingi 1,402/= na 1,520/= kwa kilo ikilinganishwa na bei dira ya shilingi 1,000/= kwa kilo. Mnada uliofuatia bei ziliongezeka na kuwa kati ya shilingi 1,481/= na 1,570/= kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mkoa wa Lindi, vyama vya msingi vilivyobaki chini ya ILULU vilifanya mnada wa kwanza tarehe 2 Novemba, 2013 ambapo jumla ya Tani 783.593 ziliuzwa. Vyama vingine 51 vya kutoka wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale ambavyo vilijiiondoa kutoka usimamizi wa Chama Kikuu cha ILULU vitafanya mnada baada ya taratibu za kupata kamati itakayowasimamia zitakapokamilika. Vyama hivyo vimeomba kufanyiwa minada yake katika wilaya ya Nachingwea ambako ndiko walikoweka ofisi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wilaya ya Tunduru, bado haijapata mkopo mpaka sasa na juhudi za kufuatilia zinaendelea. Taarifa kutoka benki ya *NMB* inaonyesha kuwa kuna uwezekano mkubwa wa vyama vya msingi vya *TAMCU* kupata mkopo msimu huu kwani deni ambalo *TAMCU* walikuwa wanadaiwa na benki hiyo ya *NMB* limelipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mkoa wa Pwani, uwezekano wa vyama vilivyo chini ya chama kikuu cha *Coastal Regional Cooperative Union (CORECU)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

kupata mkopo ni mdogo kutokana na kudaiwa fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 7 za msimu wa mwaka 2010/2011. Serikali imefanya ukaguzi maalum katika vyama hivyo na kubaini kwamba madeni hayo kwa kiwango kikubwa yamesababishwa na ubadhirifu wa viongozi na watendaji wa vyama hivyo. Hivyo, kupitia ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, hatua za kisheria zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwataka wahusika wa ubadhirifu huo kufidia hasara hiyo.

Kwa upande mwingine, wahusika wamekata rufaa, lakini mamlaka yenye dhamana imezitupilia mbali rufaa hizo zote 434, na kuwataka wahusika walipe kiasi cha fedha kinachodaiwa na vyama vyao. Kutokana na hali hiyo, wakulima wa mkoa wa Pwani wanashauriwa kupeleka mavuno ya korosho katika maghala yaliyoteuliwa. Minada ya Korosho itafanyika katika maghala hayo na wakulima watalipwa mara moja baada ya minada kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada za Serikali zinazoendelea natoa wito kwa Bodi ya Korosho na Wakuu wa Mikoa husika kuendelea kusimamia kikamilifu taratibu wa ununuzi wa korosho ili kuhakikisha kwamba Wakulima wanauza korosho zao walizovuna na kulipwa malipo yao halali kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hali ya mwenendo wa mvua za vuli mwaka 2013 na athari kwa mazao ya vuli. Taarifa ya utabiri wa mwelekeo wa hali ya hewa hususan mvua katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2013 iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini inaonesha kuwa mvua za vuli zinatarajiwa kuwa chini ya wastani katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Kaskazini mwa Morogoro, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na baadhi ya maeneo katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Geita na Mara. Pamoja na kwamba mvua za msimu wa vuli zimechelewa kuanza katika maeneo mengi ambayo yalitarajiwa kupata mvua za vuli, mvua hizi hazitarajiwi kuwa na mtawanyiko wa kuridhisha.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, athari za mvua za vuli zinazonyesha chini ya wastani. Kutokana na utabiri huo wa hali ya hewa, tathmini ya awali iliyofanyika katika maeneo yaliyotarajiwa kupata mvua za vuli inaonesha kuwa:-

Kwanza, hali ya mazao hasa katika Nyanda za juu Kaskazini na ukanda wa Pwani Kaskazini si ya kuridhisha;

Pili, mategemeo ya mavuno ya vuli ni kidogo isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria hususan katika Mikoa ya Kagera na Geita ambayo yamepata mvua za wastani hadi chini ya wastani;

Tatu, mchango wa mavuno ya vuli ambao ni kati ya asilimia 28-30 ya chakula kinachozalishwa katika maeneo yanayopata mvua hizo au asilimia 18 kitaifa hauwezi kufikiwa katika hali hii ya mvua; na

Nne, hali hii inaashiria kuwa kutakuwepo na upungufu wa Chakula katika maeneo hayo niliyotaja hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, natoa wito kwa Wakulima katika maeneo haya kuzingatia ushauri wa kupanda mazao yanayostahimili ukame na yanayokomaa kwa muda mfupi. Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika halmashauri husika wasimamie suala hili kwa ukamilifu; ili kuepusha upungufu wa chakula unaotarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa upatikanaji wa nishati vijijini yaani miradi ya *REA* na hali iliyofikiwa. Wakati wa kuhitimisha Mkutano wa Kumina Mbili wa Bunge nilieleza mikakati ya Serikali katika kueneza umeme vijijini na matarajio ya baadaye. Napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tumeweza kupiga hatua katika baadhi ya maeneo katika kuelekea kwenye malengo tuliyojiwekea.

Tayari Wakala wa Nishati Vijijini yaani *REA* ulitangaza zabuni mwezi Desemba 2012 kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa kupeleka umeme Vijijini na kujenga vituo vya kupoozea umeme. Baada ya tathmini kufanyika, zabuni

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

15 za kupeleka umeme vijijini zilipata Wakandarasi. Mikoa ambayo ilipata Wakandarasi katika awamu hiyo ni pamoja na Arusha, Dodoma, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Mara, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora. Aidha, Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupozea umeme vya msongo wa Kilovoti 11 na 33 vya Ngara, Kibondo, Kasulu, Kigoma, Tunduru na Mbinga walipatikana.

Kwa sasa wakala unaendelea na kulipa malipo ya awali yaani *advance payments* na Wakandarasi wanaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuanza kazi. Miradi hii yenye thamani ya shilingi bilioni 430.82 inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Mei, 2013 zabuni nyingine 10 ya miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 450 zilitangazwa kwa ajili yakuwapata Wakandarasi wa kupeleka umeme vijijini katika Mikoa ya Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Rukwa na Tanga. Kwa sasa tathmini ya zabuni hizo inaendelea. Inatarajiwa kwamba wakandarasi kutokana na tathmini hiyo watajulikana ifikapo tarehe 15 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia, sera; na miongozo ya usambazaji umeme vijijini. Ili kuharakisha maendeleo ya upatikanaji wa nishati vijijini, suala la wananchi kuchangia nguvu kazi na kutoa njia na maeneo ya kupitisha nyaya za umeme bila fidia pale inapowezekana limekuwa likisitizwa na Serikali kutokana na ufinyu wa bajeti. Upo ukweli kwamba, miradi mingi imechelewa kutekelezwa kutokana na wananchi kudai fidia ya miti na mazao ya msimu yanayokutwa kwenye njia ya umeme. Kwa mfano miradi ya awamu ya kwanza katika mkoa wa Pwani imechelewa kuanza na kukamilishwa kutokana na wananchi kudai fidia ilipwe kwanza ndio ujenzi uendeleee. Pia, kwa sasa ujenzi umesimama katika maeneo ya Bungu-Nyamisati na kisiwa cha Mafia kutokana na wananchi kudai fidiwa kwanza.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kulingana na sheria zilizopo kama katika njia ya kupitisha umeme yapo mazao yanayostahili kulipwa fidia. Hata hivyo kutokana na bajeti finyu Wakala wa Nishati Vijijni unashindwa kutoa fidia inayohitajika na kuona ni bora wale wanaojitolea maeneo yao wapelekewe umeme haraka kuliko kusubiri bajeti kwa ajili ya fidia. (*Makofi*)

Serikali inatoa rai kwa Viongozi na Wananchi kuona umuhimu wa kujitolea maeneo yao ili waweze kupata huduma hii muhimu mapema. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika kuwahamasisha wananchi katika maeneo yetu kuhusu umuhimu wa kupata umeme mapema kwa maendeleo ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. Shughuli za ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam zinaendelea vizuri. Mpaka sasa usafishaji wa njia ya kulaza bomba unaendelea na tayari kilometa 484.17 kati ya kilometa 517 zimekamilika. Aidha, jumla ya mabomba 20,491 yanayotosheleza kulazwa umbali wa Kilometa 243.8 yamekwishawasili nchini. Kazi ya kuchimba mtaro, kuyapanga mabomba katika mstari mmoja kwenye mkuza na kuyaunganisha pamoja kwa kuchomelea inaendelea na hadi sasa kilometa 124.3 zimeshaunganishwa. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa kambi, nyumba za wafanyakazi katika maeneo ya Songo Songo na Madimba, pamoja na maandalizi ya ujenzi wa mitambo ya kusafirishia gesi asilia.

Tutaendelea kutoa taarifa ya hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa Mradi huu muhimu kwa Taifa letu mara kwa mara. Aidha, katika kuhakikisha kwamba miradi hii inatekelezwa na kuleta manufaa katika nchi yetu, ninayo furaha kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ilipitisha sera ya gesi asilia tangu tarehe 10 Oktoba 2013. Utaratibu wa kuichapisha sera hiyo katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza unaendelea. Vilevile, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini imeandaa Mpango Mkakati wa Miaka

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

Mitano wa Utekelezaji wa Sera ya Gesi na imeanza kutayarisha Rasimu ya Sheria ya Gesi. Ni matumaini yangu kwamba vitu vyote hivi vikikamilika sekta ya gesi asilia itaimarika.

Mheshimiwa Spika, mifugo. Operesheni Ondoa Mifugo Katika Maeneo Mbalimbali Nchini. Kwa muda mrefu sasa maeneo mbalimbali hapa nchini yamekuwa yakikumbwa na migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi hasa kwa wafugaji wanaohama kutoka maeneo yaliyokatazwa kisheria kwenda maeneo mengine pasipo na maandalizi ya kutosha ya kuwapokea. Utafiti unaonesha kuwa, migogoro ya ardhi hapa nchini ina sura nne.

Moja, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, Pili, migogoro kati ya wananchi na wawekezaji, Tatu, migogoro kati ya wananchi na Serikali, na Nne, migogoro kati ya mamlaka moja na mamlaka nyingine ndani ya Serikali inayotokana na migongano ya kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, kuna ukweli kwamba, kuongezeka kwa idadi ya watu na kuongezeka kwa matumizi ya ardhi kutaendelea kuongeza kasi na vipaumbele katika kugawa maeneo yaliyoko wazi. Hali hii imeanza kuonekana katika maeneo ya wafugaji ambayo yameendelea kupungua siku hadi siku. Aidha, shughuli za kilimo, maendeleo ya makazi, na matumizi mengine ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa Vijiji kunakotokana na ongezeko la idadi ya watu kumeendelea kupunguza eneo la malisho.

Mheshimiwa Spika, kuna ukweli pia kwamba, mabadiliko ya tabianchi na kuongezeka kwa mifugo katika maeneo ya nchi kwa ajili ya kutafuta malisho na maji kumeendelea kuchangia migogoro mingi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Kati ya mwaka 2005 na sasa, tumeshuhudia uhamiaji wa mifugo kutoka mikoa ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa kwenda katika Mikoa ya Kusini na Mashariki mwa nchi. Uhamiaji huo licha ya kusababisha migogoro kati ya watumiaji wengine pia imesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye maeneo ya vyanzo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

vya maji na hifadhi za Taifa. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na hifadhi za Wanyama pori za Burigi, Maswa na Meatu, Bonde la Usangu na Bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba maadamu sasa jambo hili limefikia mahapi pazuri, Bunge nalo limepewa jukumu la kuangalia namna gani tunaweza kushirikiana na Serikali katika kulipatia ufumbuzi wa muda mrefu, basi tuwasahi Watanzania wote popote pale watoe ushirikiano wa kutosha kwa Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa katika jukumu hilo kubwa ili waweze kusaidia kupata taarifa za kutosha zitakazotuwezesha kuweza kufanya kazi yetu kuwa nyepesi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama nchini. Kwa ujumla hali ya ulinzi na usalama nchini imeendelea kuwa shwari, isipokuwa katika maeneo machache ambako kulijitokeza vitendo vinavyoashiria kuwepo kwa vikundi vya uhalifu na ujambazi. Serikali kupitia jeshi la Polisi imeendelea kujipanga kukabiliana na matishio mbalimbali ya kiusalama ikiwemo ugaidi.

Tukio lililotokea nchini Kenya hivi karibuni na matukio ya kukamatwa kwa vijana 12 kule Mtwara na lile lililotokea wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga hivi karibuni ambapo zaidi ya watuhumiwa 46 wamefikishwa mahakamani kwa makosa mbalimbali, yanaashiria kwamba ugaidi hauna mipaka unaweza kutokea katika nchi yoyote.

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha kuwa amani na utulivu vinaendelea kudumu Nchini, Serikali imejipanga katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha Vikao vya Kamati za Ulinzi na Usalama vya Mitaa, Vijiji na Vitongoji vinafanyika mara kwa mara kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Serikali za Mitaa katika kila Kata/Shehia kwa kuwashirikisha madiwani ili kujadili na kubaini kero mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

(ii) Kufufua mpango wa Daftari la Wakazi na Wageni katika kila Mtaa/Kitongoji kwa Tanzania Bara na Zanzibar ili kila Kiongozi wa Mtaa, Kijiji na Kitongoji ajue Watu wanaoishi katika himaya yake. Zoezi hili litasaidia kuepuka tatizo la wageni wasiojulikana au wahamiaji haramu. Aidha kamati za Ulinzi na Usalama za Serikali za Mitaa na Vijiji zinahimizwa kutekeleza mkakati wa Halmashauri wa kuzuia uhalifu kwa kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi/ulinzi jirani, kwa kuzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa na Sheria Ndogo zilizotungwa ili kuimarisha usalama katika Halmashauri husika.

(iii) Kuhimiza wafanyabiashara wasaidiane na vikundi vya ulinzi shirikishi/ulinzi jirani vilivyo kwenye maeneo jirani na biashara zao kama sehemu ya kuimarisha usalama wa maeneo yao ya biashara. Pia, kwa wafanyabishara wenye biashara kubwa zenye mikusanyiko ya Watu wengi wanaagizwa kufunga “*CCTV Camera*” na kuziunganisha kimtandao na “*Control Room*” ya Polisi ili kutoa msaada wa kuzuia na kutanzua mapema uhalifu wowote utakaojitokeza.

(iv) Kuendelea kuunda Zonal Task Force za Jeshi la Polisi katika kila Tarafa/Jimbo ili kukusanya taarifa za uhalifu na kufanya operesheni za kuzuia uhalifu katika kila Kata au Shehia zilizo ndani ya Tarafa au Jimbo husika sambamba na kutoa elimu na kusimamia uundwaji wa Kamati za Ulinzi na Usalama maeneo ya Ibada katika Kata au Shehia na hatimae kufikisha huduma ya usalama katika ngazi ya familia.

(v) Kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu mbinu mbalimbali za kuzuia na kupambana na uhalifu kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari, mihadhara, mikutano, maonesho na usambazaji wa machapisho na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kuhakikisha Ulinzi na Usalama katika Nchi yetu ni letu sote. Kila Mwananchi popote alipo anawajibika kushiriki kwa vitendo kwa kubaini vitendo vyovyote vya uhalifu katika sehemu za kazi,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI MKUU]

biashara na maeneo tunamoishi. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote, ni kuwaomba tuwahimiza Wananchi kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha Nchi yetu inadumu katika hali ya Amani na Utulivu.

‘Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, naomba nitumie nafasi hii ya mwisho kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Kipekee nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri. Niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri ya kuongoza vikao vya Bunge lako Tukufu. Aidha, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri na kwa michango mbalimbali wakati wa Mkutano huu. Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote pamoja na Wataalam wote wa Serikali na Taasisi zake ikijumuisha Taasisi za Sekta Binafsi, kwa misaada ya Kitaalam na huduma mbalimbali za kufanikisha Mkutano huu. Niwashukuru pia Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri walizofanya kuhakikisha kuwa taarifa za majadiliano na maamuzi mbalimbali ya hapa Bungeni zinawafikia Wananchi.

Niwashukuru madereva kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuwasafirisha kwa usalama Waheshimiwa Wabunge, Wataalam na Wasaidizi wote walioshiriki katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, Nimalizie kwa kuwatakia wote safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi na katika majimbo yenu. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 3 Disemba, 2013 saa 3.00 Asubuhi litakapokutana katika Mkutano wa 14 kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

SPIKA: Kwanza kabisa naomba tumshukuru Waziri Mkuu kwa maelezo ya kina kuhusu hali halisi katika nchi nadhani mnaondoka mkifahamu kwamba hali ya nchi iko kama hivi.

Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba tumesogeza mapema sana Kikao cha Bunge lijalo kutokana na kwamba tunaweza kukuta tunaingia kwenye Mkutano wa Katiba itakapofika mapema Januari. Kwa hiyo ilikuwa mapema Januari ndiyo kikao chetu hiki cha 14 kilipaswa kuwepo, lakini tutakuwa na Bunge la Katiba.

Kwa hiyo tumesogeza vikao vyetu vya Bunge mapema ili kusudi wakati huo tuache nafasi kwa shughuli za Katiba ndiyo sababu tumebadilisha tarehe hizi ili tuweze kufanya hivyo. Tunaamini kwamba mambo yataendelea vizuri ya Katiba basi tutakapoendelea kikao kingine tutakuwa tunaingia labda kipindi cha bajeti. Kwa hiyo mabadiliko haya maana yake ni kwamba mtakwenda kukaa kwa muda mfupi sana nyumbani pengine wiki moja tu kwa sababu mlolongo mzima wa shughuli za Bunge zitafanyika kama kawaida.

Waheshimiwa Wabunge kama tulivyoeleza kikao kijacho kitakuwa zaidi kwa ajili ya kupokea taarifa za Kamati mbalimbali ndiyo hasa kazi kubwa, kwa hiyo ninaaminikabisa Wenyeviti wa Kamati mbalimbali mtaziandaa Taarifa zenu ziweze kuwa rafhisi kujadiliwa. Kwa hiyo hiyo ndiyo kazi moja itakayofanyika.

Waheshimiwa Wabunge tunayo matangazo machache kwa ajili ya wageni waliopo hapa. Tunaye Waziri wa Sheria na Katiba wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar, tunaye pia Msajili wa Vyama vya Siasa Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, tunaye pia Mama Tunu Pindi kwa ajili ya kutusaidia kumaliza kazi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

Msinishawishi tutunge Kanuni namna ya kupiga vigelegele maana vinakuja kwa namna namna tu *(Kicheko)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni wengine ambao wamekuja kwa mafunzo ingawa ni siku ya mwisho, wapo wanafunzi 65 na walimu 7 kutoka shule ya Sekondari ya Msalato hawa ni majirani zetu wasimame mahali walipo. Ahsante, ninyi ndiyo hazina ya akina mama kwa hiyo msome kwa bidii tunawategemea, ukombozi wa mwanamke utakuja kwa elimu zaidi. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wengine 70 kutoka shule ya Silesian Seminary Dodoma wako wapi, ahsante sana tunawatakieni masomo mema na msome kwa bidii, dunia ni ya mashindani kwa hiyo mjitahidi kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba tunaahirisha Bunge lakini naomna Wenyeviti wa Kamati mbalimbali wanaomba Kamati zao zifanye kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Mheshimiwa James Lembeli anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba mara baada ya kuahirisha kikao hiki kutakuwa na kikao chao chumba Na. 227. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Pindi Chana anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake baada ya kuahirisha kikao hiki kuwepo kwa kikao katika Ukumbi Na. 231 alisema saa saba na sasa ni sasa saba.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa Mheshimiwa Rajab Mbarouk anaomba niwatangazie Wajumbe wa PAC na LAAC kwamba wanaombwa kuhudhuria mafunzo kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali yatakayofanyika Bagamoyo katika Hotel ya Oceanic Bay kuanzia kesho tarehe 10 Novemba, kwa hiyo inabidi mfanye kazi ya kusafiri.

Waheshimiwa Wabunge, jana tulitangaza kwamba jioni kutakuwa na tafrija saa kumi na mbili na nusu katika viwanja vya Bunge, kwa hiyo Wabunge wote mnakaribishwa.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge nilisahau kutangaza wageni wa Mheshimiwa Esther Matiko, nilisahau kwa sababu ya vikaratasi ungeandika vizuri, hawa wageni wanatoka Nyamongo na wengine Nyabasi, wageni wetu kutoka Nyamongo na Nyabasi wako wapi? Wale pale, wanaongozwa na Ndugu Maswi Marwa Nchama. Karibuni sana jana hatukuwaona nadhani mlkosa nafasi. Ahsanteni sana Wazee wetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 29(1), baada ya kumaliza kuwahoji tutasimama tutaimba wimbo wa Taifa halafu mimi nitasema tunahaihirisha Bunge mpaka tarehe fulani, maana yake najua siku hizi wasomi ni wengi kwa hiyo inabidi tuambizane, ili kusudi tusiwe na maneno mengine ya kuweza kusema.

Waheshimiwa Wabunge kwa moyo wa dhati ninawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyoifanya katika kipindi hiki. Mmefanya kazi nzuri sana, najua kuna wengine wamefanya kazi kwa muda zaidi kuliko wengine na ndiyo inavyokuwa. Katika kundi kubwa hili kuna wengine watachangamka zaidi, kuna wengine watakuwa wanawasikiliza wale lakini wapo waliofanyakazi kwa dhati na kwa nguvu sana na kwa kutumia muda mrefu sana.

Kamati ya Katiba na Sheria safari hii ilikuwa imebanwa sana, nadhani wamekesha sana lakini tunashukuru imekwenda vizuri. Wapo akina Mheshimiwa Mnyika wamefanyakazi sana, lazima mmpongeze Mnyika maana yake ni vijana ambao tunawashukuru sana kwa kufanyakazi vinginevyo Bunge letu lingekuwa linazubaa. Kwa hiyo mimi nawashukuru sana wote mliofanyakazi kwa bidii sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mfahamu kwamba tunafanya hapa kazi kwa kweli kwa niaba ya wananchi, na ninaomba kila tunapokwenda tukiwepo humu ndani tunafanyakazi kwa niaba ya wananchi tusifanye vinginevyo, tubishane mimi hata sina matatizo na kubishana, hata kwenye Kamati zenu mbishane mkishindwa mnaendelea na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

kesho yake huko huko mkirudi mnakuwa kitu kimoja kama nilivyosema, ndiyo Mabunge ya namna hii ya Kidemokrasia. Mnabishana kabisa lakini hubishani na mtu kama mtu unatumia mawazo yake kubishana kwa umuhimu wa hoja.

Kwa hiyo naomba tabia hii tuendeleo kujenga kwa sababu wanaotuona na kutuangalia, bahati nzuri wanatuona, wanajua tunafanya kazi kwa niaba yao.

Kwa hiyo, ninawashukuru sana kwa kazi nzuri sana mliyoifanya na ninawatakiwa safari njema huko mnakokwenda, mkafanye wajibu wenu kama inavyostahili, bahati mbaya hamtakaa sana huko nyumbani inabidi mrudi tena kwa ajili ya kazi zinazofuata. Kwa hiyo ninashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba niwahoji kuhusu kuahirisha Bunge. Kama alivyosema Waziri Mkuu ametoa hoja kwamba tuahirishe Bunge mpaka tarehe 3 mwezi wa Disemba, 2013 Siku ya Jumanne katika Ukumbi huu wa Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mnaweza kuendelea mpaka tarehe tatu hapa hapa, lakini waliosema Ndiyo wameshinda. Naomba tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa. *(Kicheko)*

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)

(Saa 6.52 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 3 Disemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)